

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

- | | |
|---------------------------------------|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu. |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10. Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani. |
| 12. Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |
| 13. Mhe. Juma Duni Hajji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14. Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15. Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16. Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17. Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19. Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20. Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21. Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22. Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpandae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope

55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad

Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 26 Machi, 2015

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, Kwa heshima na taathima naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Baraza, yaliyotokana na Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Mashirika PAC ya mwaka 2013/14. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC): Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha mezani hotuba ya kuwasilisha ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya mwaka 2014/2015. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 68

Mrejesho wa Ripoti ya Fedha za Mfuko wa Jimbo

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Aliuliza:-

Naamini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina nia njema kwa watu wake na kama hivyo ni sawa, ndio maana wawakilishi wetu wa majimbo wakapewa kipaumbele cha kupawa mfuko wa jimbo ili uwasaide katika kuwasaidia wananchi wake matatizo madogo madogo ya jimbo. Lakini jambo la kusikitisha wawakilishi hao wanashindwa kuwasilisha ripoti zao za fedha hizo hadi leo hii, mrejesho hayo ni Jimbo la Chambani na Mtoni.

Je, ni hatua gani zinazochukuliwa na Serikali kwa wale wote walioshindwa kufanya hivyo?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 68 kama ifuatavyo:-
Mhe. Spika, ni kweli hadi leo majimbo mengi bado hayajafanya mrejesho ya matumizi ya fedha ya mfuko kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Hata hivyo, napenda kutoa pondezi zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wawakilishi wa majimbo matatu ya Mtoni, Donge na Chambani, pamoja na Kamati zao kwa kufanya mrejesho ya mwaka 2013/2014 kwa wakati.

Mhe. Spika, napenda kusisitiza kwamba kwa mujibu wa sheria hiyo, majimbo ambayo yatashindwa kufanya mrejesho ya matumizi ya fedha kwa mwaka husika, hakuna fedha zitakazotolewa kwa mwaka wa fedha unaofuata, hadi pale mrejesho yatakafanyika kwa majimbo hayo.

Aidha, Serikali kwa kuitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, inawataka Waheshimiwa Wajumbe watekeleze matakwa ya sheria, ili lengo lilokusudiwa liweze kufikiwa kwa nia ya kuwaletea maendeleo wananchi katika maeneo husika.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa fedha za jimbo zinatolewa kwa ajili ya kusaidia shughuli za maendeleo ya wananchi katika majimbo.

Je, wawakilishi katika majimbo kama la Mji Mkongwe wamekataa kuchukua fedha hizo, hawaoni ni kurudisha nyuma maendeleo ya wananchi katika jimbo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kwamba nia na madhumuni ya mfuko wa jimbo, ni kusaidia miradi ya maendeleo ama miradi ya jamii mbali mbali, inayoibuliwa na wananchi katika maeneo yao. Serikali imefanya hivyo kutokana na

malalamiko ya wananchi wetu ambao wangependa wapate msaada huo kwa ajili ya kuendeleza shughuli za maendeleo katika majimbo yao.

Kwa kweli ni jambo la kusikitisha kwa Jimbo la Mji Mkongwe, toka ulipoanza utaratibu huu bado hawajachukua fedha kwa ajili ya maendeleo ya jimbo katika eneo husika. Hapa inafaa Mhe. Mwakilishi awe na sababu za msingi za kuwaelezea wananchi wake ni kwa nini amekataa, kwa sababu fedha hizo zipo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, swali mama linasema, je, ni hatua gani zitachukuliwa na Serikali kwa wale wote walioshindwa kufanya hivyo yaani kuleta marejesho. Swali langu ni kuwa, wawakilishi ni kweli wamechukua fedha za mfuko wa maendeleo ya jimbo na fedha zimetumiwa kwa utaratibu uliowekwa na ni wajibu wao kuleta marejesho ya matumizi hayo.

Mhe. Spika, lakini bahati mbaya hapajatolewa tarehe maalum kuwa tarehe hii ndio wote wawe wamesharejesha. Swali ni kuwa;

- a) Je, hawa wanashindwa au ni kwa sababu hapajarejeshwa tu na kazi ya wizara ni kuhimiza warejeshe. Hilo ni swali la kwanza.
- b) Tumepata taarifa kuwa Mhe. Mwakilishiwa Jimbo la Mji Mkongwe ni mara mbili hajachukua fedha za mfuko wa maendeleo ya jimbo na Mhe. Waziri hakuridhika na hivyo akasema kuwa awe na sababu maalum za kueleza kwa nini hakuchukua mfuko wa maendeleo ya jimbo. Je, Mhe. Waziri amefuitalia. Pamoja na kuwa Mhe. Mwakilishi hajachukua mfuko wa maendeleo ya jimbo, hakuna maendeleo anayoyafanya kule kutokana na mbinu zake mwenyewe, pengina zinaweza kushinda hata hizo fedha za mfuko wa maendeleo ya jimbo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi aliyeuliza swali la msingi ni kweli alitaka kujua ni hatua gani zinachukuliwa. Mimi nimeeleza kwa mujibu wa sheria hatua zinazochukuliwa ni kwamba kama hukurudisha marejesho, basi hizo nyengine huzipati. Kwa hivyo, hizo ndio hatua ambazo zinachukuliwa.

Kwa msingi huo basi...

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, hatukupewa tarehe maalum ya kurejesha na bado hatujachelewa mpaka hivi sasa kurejesha. Je, ni kuwa ndio wale ambao hawajarejesha wameshindwa au hawajarejesha tu na wajibu wa Mhe. Waziri ni kuhimiza.

Mhe. Spika: Mwacha Mhe. Waziri ajibu kwa mtiririko alivyojipanga. Mhe. Waziri, majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunisaidia naona Mhe. Salim Abdalla ana kiherehere.

Mhe. Spika, kama nilivyosema utaratibu unafuata sheria na sheria inaeleza wazi kwa yale majimbo yatakayoshindwa kurejesha marejesho, basi ule mwaka unaofuata hizo fedha hazitotolewa. Pia, sheria inaeleza ambayo tumeitunga wenyewe, tunapaswa sote tuilewé wajumbe, kwamba haikuweka kiwango cha mwisho, kiwango cha mwisho ni pale ambapo ile awamu nyengine inayofuata. Kwa hivyo, kinachotakiwa ukirejesha marejesho kwa wakati, itatusaidia zaidi kupanga mipango ya fedha zitoke mapema zaidi, pale inapochelewa kutoka fedha, vile vile, kuja marejesho kunachelewesha pia kupanga mipango ya kupatikana fedha nyengine ambazo tayari zimewekwa ndani ya bajeti. Kwa hivyo, bado hujachelewa kufanya marejesho, unatakiwa ufanye marejesho ili upate fedha hizo za awamu nyengine.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, wito wangu hapa ni kuendelea kufanya marejesho haraka iwezkanavyo, kwa sababu naamini wawakilishi wengi wamefanya vizuri katika majimbo yao na marejesho wanayo na hata ukiwasiliana na Kamati husika za maendeleo katika majimbo zinatoa taarifa nzuri, wakati waratibu wetu wanapokwenda kufuitalia huko.

Kwa hivyo, naamini Waheshimiwa Wawakilishi, marejesho wanayo, cha kufanya ni kuleta mrejesho ili wachukuwe fedha zao ambazo Mhe. Waziri wa Fedha anazo tayari katika bajeti yetu. Ingawa Mhe. Waziri huwa hapendi kusema sana hilo, kwa sababu anasema tayari zile fedha zimo katika bajeti zetu za wizara. Kwa hivyo,

cha msingi hapa ni kuleta marejesho na fedha ziweze kuendelea kutolewa. Kwa wale ambao wameleta marejesho, fedha zao watazipata wakati wowote kuanzia sasa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuhusu hatua gani za maendeleo hatuyaoni yaliyofanyika ya Mji Mkongwe. Hicho ni kigezo cha wananchi wenyewe, wenyewe wananchi ndio wanajua kwamba yapo maendeleo yanafanyika kwa kupitia mwakilishi wao ama hayapo, kwa sababu wananchi wanajua yanayofanyika pale. Sisi tunachozungumzia hapa ni fedha za mfuko wa maendeleo, hata yangkuwa maendeleo gani yapo katika Mji Mkongwe, fedha hizi zingesaidia kuchochea maendeleo zaidi, ubaya wake ni nini kuzichukua. Kwa hivyo, wananchi wana haki ya kumuuliza mwakilishi wao, kwa mini fedha hizi hawajazichukua ambazo zingesaidia kwa njia moja au nyengine maendeleo ya Jimbo la Mji Mkongwe. (*Makofi*)

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii, pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu mazuri aliyyoatoa, swali langu mimi ni dogo sana. Kwa kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe ambaye anatokana na chama cha upinzani cha CUF, ameamua kukataa kuchukua pesa hizi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa kuwa Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa msukumo mkubwa katika Jimbo la Mji Mkongwe kwa kupeleka maendeleo, ikiwemo mradi wa maji safi na salama ambao unaendelea *project* yake, taa za barabarani kwa kupitia mradi wa ZUSP, pamoja na uwekaji wa lami katika *feeder road* zilizozunguka ndani ya Mji Mkongwe.

Je, Mhe. Waziri pesa amekataa, hii miradi ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya mwakilishi ameikubali au ameikataa?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa Serikali ina wajibu na imetoa ahadi ya kuleta maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar, kwenye hili hatushauriani na mwakilishi, tunafanya wajibu wa Serikali katika maeneo yote ya nchi yetu, bila ya kubagua kwamba mwakilishi huyu anatoka CUF au huyu anatoka CCM au chama chengine chochote. Utaratibu tuliojiwekea ni kuleta maendeleo kwa watu wetu.

Mhe. Spika, napenda nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Dk. Ali Mohammed Shein kwa kusimamia vizuri ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, pamoja na Serikali yake kwa utekelezaji mkubwa uliofanikiwa kwa zaidi ya asilimia 90 katika kutekeleza ahadi zilizopo. (*Makofi*)

Nam. 33

Malalamiko ya Kero za Baa katika Jimbo la Kiembe Samaki

Mhe. Nassor Salim Ali: (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Taarifa ya Habari ya ZBC ya tarehe 1/1/2015 ilitangaza kwa wananchi wa Kiembe Samaki, wanailalamikia Serikali kuwa na mabaa mengi katika Jimbo la Kiembe Samaki, wanafunzi pia walilalamika nao katika taarifa ya habari hiyo kuwa muziki unapigwa mpaka asubuhi.

- a) Je, la kushangaza ni kuwa baadhi ya baa hizo hazina leseni, nini adhabu yake?
- b) Je, Serikali taarifa hizo wanazo na wanawaambia nini wananchi wa Kiembe Samaki kama wenzao?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 33 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu naomba kutoa maelezo yafuatayo.

Mhe. Spika, biashara ya vimeo hapa Zanzibar inaendeshwa kwa kufuata Sheria ya Vileo ya mwaka 1928. Sheria hiyo ndio iliyoweka utaratibu wa ukataji wa leseni na adhabu kwa wanaokwenda kinyume na taratibu za leseni hizo. Kila mwaka kabla ya kutolewa leseni mpya kwa vilabu vya pombe au baa, hutolewa matangazo ili wale wenyewe vipingamizi katika mamlaka ya utoaji wa leseni na hatimaye kutakiwa kufika katika vikao vya majadiliano na wajumbe wa Mahakama ya vimeo, hoja zikiwa na uzito leseni haitolewi kwa wanaoomba leseni hizo.

Mhe. Spika, pamoja na kuwa sheria hiyo ni ya muda mrefu inafanyakazi hadi leo, bali matatizo makubwa ni wazi inahitajika marekebisho ili iendane na hali halisi ya sasa. Ofisi yangu iliwasiliana na Tume ya Kurekebisha Sheria ili kuifanyia mapitio na kupendekeza sheria mpya. Naishukuru tume ya kurekebisha sheria imeshakamilisha sheria hiyo na kupata Rasimu ya Sheria mpya, baada ya kushauriana na wahusika wengine na ofisi yangu inaifanyia kazi na muda sio mrefu mswada wa sheria hiyo utaletwa katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama hivi ifuatavyo.

a) Jimbo la Kiembe Samaki kwa mujibu wa kumbukumbu tulizonazo, kuna baa 11 ambazo zote hizo zimepewa leseni kwa mujibu wa taratibu za kisheria na ofisi yangu haina taarifa ya kuwepo kwa baa ambazo hazina leseni na zinafanyakazi ndani ya Jimbo la Kiembe Samaki.

Aidha, kwa sheria hiyo adhabu ya kuendesha biashara hiyo bila ya leseni ni faini au kifungo kisichozidi miezi 12 na Mahakama imepewa uwezo wa kufilisi vinywaji vyote vitakavyokutwa ndani ya baa hiyo.

b) Ofisi yangu haina taarifa hizo endapo kuna wananchi wenyne malalamiko, watumie utaratibu uliowekwa na sheria, kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya awali na mamlaka husika zitachukua hatua zinazostahiki.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake ya kutoa hata idadi ya mabaa katika jimbo la Kiembe Samaki ikiwa ni mabaa 11.

Mhe. Spika, mimi swali langu nataka nielezwe kwa sababu kuwa na majengo ya ulevi sio jambo jema.

Ni sababu zipi hasa zilizosababisha hapa Kiembe Samaki kuwa na mabaa yote hayo 11, tena ni mabaa ya ulevi. Wakati kurundikana kwa mambo kama haya yanahatarisha dini yetu, usalama na hata athari ya kuongeza maradhi ya ukimwi. Kwa sababu mtu akishakulewa lolote anaweza akalifanya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum: Mhe. Spika, ni sababu zinazofanya hivyo ni:

- 1) Wenyne maeneo kukubaliana na wale wanaofanya biashara za baa.
- 2) Mwenye eneo akishakubaliana na anayetaka kufanya biashara ya Baa anakwenda kwenye mamlaka husika anaomba leseni kwa mujibu wa sheria kama nilivyosema.
- 3) Utaratibu wa kuwepo baa ndani ya eneo lolote lile unategemea na hali halisi ya wenyeji wa eneo lile. Wakikubaliana na utaratibu huo basi baa zitakuwepo kwa mujibu wa sheria. Wasipokubaliana na utaratibu huo Mamlaka husika haiwezi ikaruhusu kuwepo kwa baa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi na mimi kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri, kwa kuwa swali lake mama alisema kwamba kuna baa 11 Kiembe Samaki. Lakini nimuulize Mhe. Waziri kwa kuwa kuna wanafunzi ambao wanalamika kwamba wanapigwa kelele kuhusu magoma yanayofanywa pale usiku. Wanafunzi hao tunawategemea kuwa na elimu yao nzuri baadae ambayo itawafaa wao pamoja na wazee wao.

Je, Mhe. Waziri ni lini umewahi kulitembelea jimbo la Kiembe Samaki na kuhakikisha kuwa hakuna baa zilizoongezeka. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum: Mhe. Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu mama, kama kuna kelele au kuna nini ni suala la wakaazi wenywewe kwenda kwenye mamlaka husika wakatoa malalamiko yao ili mamlaka husika iweze kufanya hivyo.

Mhe. Spika, mimi ili niweze kutembelea lazima nipata taarifa kutoka kwa wananchi wenywewe au mamlaka husika kama kuna kadhiya hiyo. Sasa mpaka hivi ninavyojibu swali hilo bado sijapata malalamiko hayo, wala sijapata kadhiya hiyo.

Mhe. Spika, niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi kama tunataka kutekeleza hilo basi ni vizuri kwanza tufuate ule utaratibu wa kisheria tuliojiweka au uliowekwa. Bila ya kufuata taratibu za kisheria mambo mengine yatashindikana kuweza kuyafanyia kazi.

Nam. 62

Tatizo la Vifo kwa Akinamama Wakati wa Kujifungua

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Aliuliza:-

Akinamama wengi hupoteza maisha wakati wa kujifungua kutokana na kifafa cha mimba na tatizo hili lipo Zanzibar kwa kiwango kikubwa.

Je, wizara imejipanga vipi kukabili ana na tatizo hili ili akinamama wawe salama wakati wa kujifunguwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa hapa katika Baraza hili tukufu la Wawakilishi kwenye afya na uzima katika jukumu la kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 62 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba nikubaliani nae kwamba akinamama wengi hupoteza maisha yao wakati wa kujifungu kutokana na sababu moja kubwa kabisa mionganoni mwa sababu nyingi nyinginezo ni sababu ya kifafa cha mimba. Tatizo hili kweli lipo Zanzibar, lakini tatizo hili linatokana na sababu moja tu, sio sababu ya Wizara ya Afya, sio sababu ya madaktari na sio sababu ya manesi ambao wanaohudumia kliniki za waja wazito, lakini ni sababu moja kubwa ya akinamama aidha kutokwenda *clinic* mapema kwa kupima ujauzito.

Sababu ya pili kupililiza vile vipindi vyao ambavyo wanapangiwa kwa ajili ya kupima ujauzito, nitaeleza sababu kwa nini.

Kifafa cha mimba kinaitwa *Eclampsia*. *Eclampsia*, hajji mara moja inakuja na dalili au alama za maonyo yake yanachukua miezi sita. Kwa hiyo, ndiyo maana mwanamke mjamzito anatakiwa aende *clinic* kuanzia na ujauzito wa miezi miwili na nusu ndio anapotakiwa kwenda *clinic*. Sasa akipitiliza hilo basi dalili mbali mbali hutokeza na kifafa cha mimba hakiwezi kumtoa roho mtu mpaka hiyo miezi sita zile dalili ziwe zimedharauliwa. Kwa hiyo, zikidharauliwa zile dalili zake miezi sita ndipo hapo kinapotokea kifafa cha mimba.

Mhe. Spika, nchi zilizoendelea hivi sasa wameweza kuepukana na tatizo hili la kifafa cha mimba kwa sababu kuwa kinatambuliwa mapema sana, tokea ujauzito wa miezi mitatu. Dalili zenyewe ni kama ifuatavyo:-

Baada ya miezi mitatu mwanamke anaweza kupata dalili zifuatazo yaani kila mwezi anapokwenda *clinic*.

- 1) Miguu kuvimba, yaaani miguu inapovimba pale daktari au muuguzi wa *clinic* ya mama na mtoto anatakiwa achukue hatua ya kwanza kabisa ambayo ni ya kupima mkojo na damu, Iikidharauliwa hilo,
- 2) Kutoka *protein (protein urine)* kwenye mkojo. Hapa ina maana ile hatua ya mwanzo imedharauliwa ya kutopimwa mkojo wake ndiyo imefikia mpaka *protein* sasa kutoka ndani ya mkojo. Ikishamalizika *protein* kutoka ndani ya mkojo *protein* huingia katika mfumo wa damu ambayo pia huleta athari.
- 3) *Protein* inapoingia katika mfumo wa damu huleta athari ya kupandisha *pressure*, yaani *Hypertension*.
- 4) *Hypertension* ikishamalizika nayo hupeleka athari nyengine yakupelekea shinikizo la damu, yaani *temporary blood pressure* kwa kipindi kile cha ujauzito na hapo huendelea hizo dalili hutokeza *gestose epimer* na mambo mengine yote yanafatia mpaka hufikia kifo cha mama mjamzito.

Kwa hivyo, njia pekee sio Wizara ya Afya, sio madaktari na sio wauguzi, bali ni mama mjamzito na hilo tunahimiza kila siku, anatakiwa kachelewa kabisa afike *clinic* kuanzia mwezi wa tatu wa ujauzito wake. Baada ya hapo anatakiwa aendelea na *clinic*, ndio maana kuna ile kadi mpaka anapomaliza na kujifungua. Tukifanya hivyo basi tutakuwa tumeepuka kifafa cha mimba kwa asilimia zaidi ya 95%. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, lakini naomba nimuulize swali langu kama hivi. Kwa kuwa Wizara imeshindwa kukabiliana na tatizo kwamba hatuna wataalamu, kwa nini tusiombe wataalamu kutoka nje ili kuokoa maisha ya akinamama hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, katika jibu langu mama nimesema hivi Wizara ya Afya haikushindwa na tatizo hilo na mionganoni mwa maeneo makuu ambayo Wizara ya Afya pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imewekeza sana kibajeti kwa idadi ya wafanyakazi, kwa idadi ya nguvu ya utendaji ni eneo la mama na mtoto. Hata ufadhili mkubwa unaotokana na *WHO, UNFPA, USAID, CDC* na mashirika mengine yote ya maendeleo nguvu kubwa imeelekezwa kwenye (*Child and Mother Mortality Rate*) yaani kupunguza vifo vyta mama na mtoto.

Kwa hiyo, Wizara ya Afya, naamka tena haikushindwa kabisa na huduma hizo zinapatikana mpaka vijiji hivi sasa zimeshuka mpaka *PHCU*. Tatizo lililokuwepo ni kutoa elimu kwa jamii nini, Wizara ya Afya inafanya. Lakini haiwezi Wizara ya Afya ikenda majumbani kuwatoa akinamama kwa nguvu kuja kupima ujauzito ume, haiwezekani.

Mhe. Spika, ndio maana tunasisitiza tena na hili pia nasisitiza kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mtusaidie hasa wale wanaotokea maeneo ya *PHCU* zizokuwepo vijiji, tumezitembelea mbali mbali, ipo moja pale Bumbwini ambapo akinamama wanakwenda wengi kupima ujauzito, vipo vituo vya Nungwi, Tazari pamoja na kile chengine cha Kidoti kama Kijini. Mfano Kijini wana siku maalum. Wakina mama wajitokeze kwa wingi kwenda kupima ujauzito mapema na katika *clinic* zile tunahakikisha kunakuwa hakuna upungufu wa aina yoyote mpaka zile *stick* za kupimia mkojo ili kuhakikisha kwamba tunaepukana na kifafa cha mimba.

Pia, tunatakiwa na Umoja wa Mataifa, yaani *WHO*, Zanzibar ikiwa moja wapo ambayo imeshiriki pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutia saini kwamba huduma za mama na mtoto *basic* zitatolewa na kupunguza hasa haya maradhi ya (*Eclampsia*) kifafa cha mimba ama kifafa cha ujauzito kwa kiasi kikubwa.

Kwa hiyo, Wizara ya Afya kwa upande huu hatuna kasoro ukiacha zile kasoro ndogo kama lifti juzi nilieleza. Lakini kwa upande wa mama na mtoto hakuna kasoro ya aina yoyote sio ya dawa, sio ya chochote.

Mama njamzito sasa hivi anatakiwa ahimizwe popote alipo kwenda *clinic* kila mwezi, yaani kwa kiwango cha chini kabisa ni kila mwenzsi. Wengine wanapangiwa mpaka kila baada ya wiki mbili, ili hizi dalili zinapotokeza dalili sita nimezitaja, basi ile dalili ya mwanzo ndiyo alama ya mwanzo ya onyo inaweza kugunduliwa ili kuepukana na kifafa cha mimba. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Salma Muhammed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa amesema sababu kubwa ya kifafa ni wajawazito kutohudhuria *clinic*. Kuna vijiji ambavyo vituo vya afya viko mbali kama kijiji cha Vikunguni, Dutani, Magome, Mgenikage na wananchi wake wamejitätidi kujenga kituo cha Afya. Kwa bahati mbaya Makamu wa Pili wa Rais aliahidi kituo kile kimalizwa katika Sheria za Mapinduzi zilizopita wakati wa kufunguliwa.

Je, Mhe. Naibu Waziri huoni kwamba sababu ya kutomalizwa kituo kile na kikafunguliwa ndio kinachosababisha wajawazito wa Vikunguni kutohudhuria *clinic* na kusababisha hicho kifafa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, kweli nimesema kwamba kutohudhuria *clinic* kwa wakati ndio sababu kuu. Lakini pia nimeshawahi kutamka katika Baraza lako tukufu kuwa Zanzibar sasa hivi tunaongoza katika Afrika nzima kwa kuwa na idadi ya *clinic* nyingi kwa wastani wa mraba wa kilomita tatu, huwezi kwenda zaidi ya kilomita tatu kuna *clinic*. Wenzetu Tanzania Bara bado hawajafikia hata hilo bado, wao wapo zaidi ya kilomita tano au sita maeneo mengine. Sisi tunaongoza katika hilo.

Mhe. Spika, naomba nilitamke wazi kwamba katika zile takwimu hata za Umoja wa Mataifa, sisi tumepitiliza na hakuna *clinic* yoyote iliyokuwa zaidi ya kilomita tatu, pamoja na ile ya pale pahala nilipokwenda juzi panaitwa Muachealale maana ipo *less than three kilometers*. Isipokuwa tatizo lao, mfano natoa wa Mwachalale, tatizo lao kubwa ni usafiri kwa sababu hakuna daladala zinazokwenda na njia sio nzuri.

Mhe. Spika, wao Mwachalale wapo chini ya kilomita tatu, lakini usafiri na njia. Lakini kwa hivi vituo alivyovitaja na mimi bahati nzuri nimevitembelea vyengine, usafiri ni mzuri katika eneo hili na maeneo mengine lami ipo.

Mhe. Spika, lakini naomba kutamka kwamba kutofunguliwa kwa baadhi ya vituo hivi kama ilivytotolewa ahadi na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika Sherehe za Mapinduzi naamini Sherehe za Mapinduzi yajayo vituo hivi vitafunguliwa. Kwa sababu kuna mradi mkubwa ambao unaendelea sasa hivi Kisiwani Pemba, ambayo ni miradi miwili hii, tukishirikiana na *Milele Foundation* baadhi ya vituo wamechagua Pemba wanatengeneza. Hawa ni wale Wazanzibar waliokuwa katika *Diaspora* wanaoishi nje ya Zanzibar hasa wanaoishi nchini *United Arab Emirates*.

Mhe. Spika, mradi wa pili ni *Orio*, wamechagua pia baadhi ya vituo kuvifanyia *upgrading* kwa kule Kisiwani Pemba.

Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa anipatie majina ya vituo hivyo husika tuangalie tena kama mraba wa kilomita ni zaidi ya kilomita tatu ili tuweze kufatilia kwa karibu zaidi, lakini pia nitathibitisha katika *list* ya *Orio* na miradi ya *Milele Foundation* kama vituo hivyo vipo. Naamini kama vitakuwepo basi ndani ya muda mfupi *Inshallah* vitafunguliwa.

Hivi majuzi tu Wizara ya Afya ilikuwa na kituo kimoja na nyumba za madaktari mbili ambazo zimefunguliwa katika Sherehe za Mapinduzi zilizopita. Tulikuwa tuna vitu zaidi ya hivyo tunataka kufanya lakini ile ratiba ya Sherehe ya Mapinduzi nayo ilikuwa imebanwa, kwa hiyo, Wizara ya Afya tumekosa vitu vyengine kuvifungua. Naamini Sherehe zijazo tutapata muda wa kutosha kufungua vitu vingi zaidi. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kuuliza swali hili la pili kwa leo. Napenda nimuulize Mhe. Naibu Waziri kuwa mara nyingi tunapiga kelele kwamba madaktari wetu tuwapeleke kwenda kusoma kujua matatizo ya maradhi ambayo yanaweza kutokea, yaliyokuwa yanasaababishwa na aina fulani au maradhi yanayokuwa sio ya kuambukiza.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri hapa alisema kwamba kuna sababu sita ambazo zinajitokeza katika ugonjwa huu wa kifafa, sijui kama nimeelewa vizuri kama sivyo basi atanifahamisha au kuna alama sita.

Lakini je, katika alama hizo sita, mimi niulize hichi kifafa hasa kinasababishwa na nini au chanzo chake hasa ni nini? Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba tena nijaribu kutoa ufanuzi, halafu niende kwenye swali hili alilouliza Mheshimiwa.

Dalili sita ambazo ni onyo zinazotokea, mmoja humfata mwenzake, kwa hiyo, ukishaidharau ya kwanza inakuja dalili ya pili, dalili ya pili ukiidharau inakuja dalili ya tatu na kila dalili inayomfuata mwenzake inakuwa ni mbaya zaidi na kali zaidi na inamuathiri mwanamke zaidi.

Sasa sababu Kuu inakuja kwenye ile dalili ya kwanza. Wakati mwanamke ni mjamzito *body system* ndani hubadilika, yaani anapata *hormonal change, hormonal in balance*, yaani *hormones* kwa Kiswahili vichocheo, kwa hivyo, hizi *hormones* katika mwili huwa kunatokea *imbalance* kubadilika na mfumo mzima na nishawahili kueleza hapa mambo ya kichefu chefu ni *hormonal imbalance*, kujisikia kutapika, kwa sababu kuna kiumbe kipywa ambacho kinafanyika ndani ya mwili wa binadamu na zile *nutrients*, yaani vitu muhimu, vimelea muhimu vinaelekezwa kwa yule mtoto, kwa hivyo, kunakuwa na *body imbalance*.

Sasa panapotokezea *body imbalance*, panapotokezea *body imbalance* wakati mwengine hizi *protein, sugar, carbohydrates* nazozinakuwa *imbalance* na ndio maana dalili ya kwanza inajulikana kwa mwanamke mjamzito mkojo wake unakuwa tofauti. Na ndio maana kitu cha mwanzo kabisa mwanamka akipata ujauzito anafanywa nini, anapimwa kupitia mkojo, kwa sababu mkojo ndio unaojulisha ujauzito mwanzo hata kabla ya damu kutokana na ile *hormonal imbalance* inayotokea. Na siku hizi bahati nzuri teknolojia imeendelea mkojo kuna utumiaji wa *stick* tu, wanaita *pregnant test* ile, ukiingiza tu pale pale matokeo unapata ndani ya sekunde 5 au 10, huchelewi.

Sasa sababu kubwa kabisa ni *hormonal imbalance* na ndio dalili zake huonekana katika mkojo, ukiacha hiyo *hormonal imbalance* kama hajasaidiwa na kupewa dawa, huelekea kwenye kuvimba miguu na inapoishia

kuvimba miguu ina maana damu inakuwa haipandi juu, ndio anaelekea kwenye *pressure* na mambo mengine mpaka sindikizo la damu mpaka kifo hutokeea.

Kwa hivyo, na hiyo haichukui muda wa siku moja au siku mbili, inachukua miezi mitano mpaka sita jumla yake. Kwa hivyo, sababu kuu ni *protein* kuingia kwenye mkojo halafu kuingia kwenye damu. Ahsante sana.

Nam. 66

Uhaba wa Wafanyakazi katika Kituo cha Afya cha Bwagamoyo

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Kabla ya kuuliza kwa ruhusa yako naomba kutamka yafuatayo:

Kwanza nitoe shukurani za dhati kwa wale wote waliosaidia katika ujenzi wa kituo hiki, ikiwa ni pamoja na Mhe. Omar Yussuf, Mzee Waziri wa Fedha, kwa kutoa mchango wako wa shilingi milioni tano taslim, Mhe. Haji Omar Kheir Waziri wa Nechi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum kwa kutoa rangi ya kuingiza katika kituo hicho. Vile vile, Wizara ya Fedha kwa kumaliza mambo yaliyobakia na Kamati zake tukufu za Baraza la Wawakilishi za kudumu, Kamati ya *PAC* na Kamati inayohusika na Uwezeshaji, Mifugo na Habari.

Baada ya hayo Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba swalı langu nambari 66 lijibiwe.

Kituo cha Afya cha Bwagamoyo (Shehia ya Piki) ya Jimbo la Mtambwe ambacho kilifunguliwa rasmi na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi hivi sasa kimekabiliwa na upungufu mkubwa wa wafanyakazi.

Je, Wizara imelichukulia vipi tatizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe swalı lake Nam. 66 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla sijamjibu naomba na mimi niungane nae kumpongeza sana Mhe. Omar Yussuf Mzee Waziri wa Fedha, nafasi maalum Ikulu, Mhe. Haji Omar Kheir Mwakilishi wa Jimbo la Tumbatu CCM, pamoja na Wizara ya Fedha na Kamati ya *PAC* na wengineo wote waliochangia katika kituo hiki. Ninawapongeza kwa sababu kituo hiki kimeshaanza kuleta sura ya jamii mapema, sio tena kinaonekana kama kituo cha Wizara ya Afya lakini ni kituo cha jamii ya wananchi wa hapo panapoitwa Bwagamoyo Mtambwe.

Nitaeleza sababu kwa nini nasema hivyo kwamba kwa sababu sisi Wizara ya Afya tunapeleka wafanyakazi tunalipa mishahara yao, tunapeleka vifaa na tunapeleka dawa, lakini jamii imekuwa ikishirikiana zaidi, kwa hivyo, naomba pia nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Salim Abdalla Hamad, kuwa mstari wa mbele katika suala hili.

Sasa Mhe. Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa kuwa Kituo cha Afya cha Bwagamoyo ni mionganoni mwa vituo vitano katika Jimbo la Mtambwe ikijumuisha Kituo cha Afya cha Kisiwani kipo, pia chini ya kilomita tatu, Mtambwe Kusini, Mtambwe Kaskazini na Mzambarauni.

Mhe. Spika, ni kweli Kituo cha Afya cha Bwagamoyo ambacho kimo katika Shehia ya Piki ndani ya Jimbo la Mtambwe kilifunguliwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Idd, kwa ajili ya kutoa huduma za Afya kwa wananchi.

Mhe. Spika, kwa sasa kituo cha Afya cha Bwagamoyo kina jumla ya wafanyakazi watatu (3) na mimi nilibahatika kufanya mawasiliano moja kwa moja na baadhi ya wafanyakazi kwa sababu nimetaka kujua hali halisi iliyokuwepo pale. Wafanyakazi hao ni pamoja na *General Nurse* mmoja (1) huyu anaitwa Bi Asha Khamis ambaye yeye ana jukumu la kutoa huduma za tiba, elimu ya afya ya magonjwa mbalimbali pamoja na ushauri nasaha kwa wagonjwa wote wanaofika hapo katika Kituo hicho cha Afya cha Bwagamoyo.

Mhe. Spika, mfanyakazi mwengine anaitwa Bi Safia Khamis yeze *grade* yake ni *PHNB*. yaani *Public Health Nurse Grade B* ambaye yeze hutoa huduma za kinga kwa watoto na mama wajawazito ikiwemo chanjo kwa watoto waliofika muda wa chanjo chini ya miaka 5.

Mhe. Spika, wa tatu. anaitwa *Alhajj* Sheikh Ali Kombo Faraji ambaye yeze ni *Orderly* na yeze jukumu lake ni kutunza usafi wote na ndani ya kituo pamoja na eneo lote lililozunguka kituo na usafi wa mazingira ya pale yote pamoja na vifaa vinavyotumika kwa wagonjwa.

Mhe. Spika, Wizara itajitahidi kuongeza wafanyakazi katika kituo hicho tutakapopata idhini ya kuajiri wafanyakazi wapya zaidi na kwa mujibu wa hali itakavyoruhusu, lakini kwa sasa wafanyakazi hao kwa uchunguzi wetu na idadi ya wagonjwa wanaofika pale inakidhi haja kabisa. Ahsante sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, ninashukuru kwa kupata kuuliza swali la nyongeza. Lakini kabla sijauliza swali la nyongeza, napenda kutoa taarifa kuwa muekaji wa msingi wa kituo hiki na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hivyo, kituo hiki kimepata baraka kubwa. Lakini kwa sababu siku ya ufunguzi risala iliyosomwa baada ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kukitembelea kituo kile ni kuwa kipate idadi ya wafanyakazi 12 ili kiweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Kwa kuwa wafanyakazi wa tatu ni sawa na kusema kuwa kinafanya kazi iliyohitajiwa kwa asilimia 25 tu. Na kwa sababu Chuo chetu cha Afya kimeshatoa wanafunzi wengi na katika Jimbo langu wapo na wana uwezo wa kujaza mapengo pale haoni kuwa Mhe. Waziri kwa sababu ya umuhimu wa kituo hiki kwa maslahi ya wananchi na historia yake ipo haja ya kuona kuwa tufanye dharura ya ajira ili kituo kile kipate hawa wafanyakazi 9 walipungua na huduma ipatikane kama ilivyofikiriwa au ilivyokusudiwa hapo mwanzo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, vituo vyote hivi vyenye *grade* ya *PXU* vina *average* wastani wa wafanyakazi 3 hadi 5, baadhi ya vituo ambavyo hutoa huduma zaidi kuwa na wafanyakazi 6 mpaka 7. Kwa kweli idadi ya wafanyakazi 12 hata hiyo nafasi ya kufanya kazi kwa kituo hiki itakuwa haipo. Naomba niseme tena kwa *grade* ya kituo hiki cha *PXU*, basi wafanyakazi hawa watatu mpaka sasa wanakidhi haja, lakini sisi tumo mbioni, narudia tena tumo mbioni ikiwa za riadha au muda mfupi *relay*, lakini tumo mbioni kukififikishia kupata wafanyakazi 5 na hili niliuliza kutokana na hili suala nalifuatilia kwa karibu sana suala hilo. Lakini pia nikaelezwa kwamba nafasi yenye si kubwa, yeze Mheshimiwa anajua pana vyumba vingapi pale.

Kwa hivyo, *maximum* tutakuwa kwa *grade* ya kituo hiki tuna wafanyakazi 5. Kingekuwa *PXU plus* kinazalisha, kina huduma ya uzazi moja kwa moja basi hapo tungeweza kuelekea baina 7 mpaka 9, lakini 12 hicho kituo ni cha *grade* kubwa sana ambacho kituo hiki bado hakijafikia. Nakubaliana na hadhi kwamba kimewekwa jiwe la msingi na Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kimefunguliwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Idd, yote nakubaliana nayo, hadhi ni kubwa sana. Lakini sisi upande wa afya kiufundi tunaangalia zile huduma zinazotolewa.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri wa Afya swali lifuatalo.

Mhe. Spika, waswahili wanasema ukisema wewe umeungua mwenzako ni makaa, kituo kama hiki Bwagamoyo kiko kule mjini Kiuyu. Kituo hiki kilijengwa katika hali ngumu sana mpaka wananchi wa mjini Kiuyu wakasema kwamba bora tuchangishane hata nusu shilingi shilingi nyumba kwa nyumba, lakini hatimaye kituo hiki kimejengwa na ni kizuri.

Huu ni mwaka tangu kituo kile kimalizike kujengwa na Wizara ya Afya wanajua hili, hakuna chochote kilichofanyika ni ahadi tu, tutaleta mfanyakazi, tutaleta hiki tutaleta hiki. Sasa kwa niaba ya wananchi wa mjini Kiuyu na mjini Kiuyu ilipo na kituo chengine cha afya kilichopo ni kama kilomita nne, kwa hivyo Mhe. Naibu Waziri namwambia kabisa yako maeneo ambayo masafa kutoka walipo mpaka kukiona Kituo cha Afya ni zaidi ya kilomita tatu moja ni mjini Kiuyu. Ni lini atakwenda kukitembelea kituo kile na kutimiza ahadi ambazo zilizoekwa kwamba karibuni kituo kile kitapata wafanyakazi na mambo yanayohusika ili kifanye kituo kile.

Mhe. Spika: Haya ndio katika yale masuala ya kuchomeka chomeka, Naibu Waziri saidia jibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa bahati nzuri kituo hiki wananchi wa pale walibahatika kuonana na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein nao pia wakatoa kilio chao. Mnamo mwezi wa 9 ndio kwanza nakanyaga Wizara ya Afya ndani, agizo la mwanzo nililolipata mezani kwangu lilikuwa na jina ya kituo hiki kwa hivyo kiko kwenye *memory* vizuri sana,

mionganoni mwa ahadi nyengine zilizokuwa zimetolewa pia na mwenyewe Mhe. Rais wakati akiwaomba wananchi ridhaa ya kura zao akiwepo Kisiwani Pemba ambao walimpa ridhaa ya kutosha mpaka akawa Rais wa Zanzibar, basi kituo hiki kilikuwa ni kimojawapo mionganoni mwa orodha ya mambo ambayo mimi nimetakiwa nitemeleee na kusimamia.

Kwa hiyo, bahati nzuri nilifika na bahati nzuri nilifika na Dr. Mohammed Saleh Jidawi ambaye ni Katibu Mkuu, Wizara ya Afya. Sasa kuna mambo ambayo sasa hivi tunafanya kiserikali, kufuatilia pamoja na ahadi kuna ahadi pia Mhe. Rais ambayo aliitoa hapa tunafatilia kwa karibu sana na ninaamini kabla ya bajeti kuja mambo mengi tutakuwa tunayakamilisha.

Na namuhidi Mheshimiwa tukimaliza tu *session* hii ya Baraza baada ya kama wiki mbili, tatu, mimi na Katibu Mkuu Dr. Jidawi tumepanga tena ziara ya kwenda Pemba na safari hii tutakaa kipindi kirefu zaidi, kwa sababu kuna orodha mpaka maeneo ya Mkoani, kuna orodha ya Abdalla Mzee pale kwenda kuharakisha ili ifikie *stage* nzuri ifikapo 12 Januari na kadhalika. Kwa hivyo, naomba Mheshimiwa tuwe tunakumbushana lakini hili lipo mionganoni mwa orodha ambayo mimi nimepata agizo kusimamia. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tutaendelea kulifatilia hili kwa karibu. Ahsante.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya mwaka 2014/2015

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaendelea majadiliano na leo tuna wageni pale juu wageni wetu wa leo ni viongozi wa Serikali ya wanafunzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Chukwani, jumla yao ni wanafunzi 35 wakiongozwa na Ndugu Spika, Salum Hassan Salum. Karibuni sana. Hebu nimuone Ndugu Spika, Salum Hassan Salum. Karibu Mhe. Spika. (*Makofii*)

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia maagizo ya Kamati. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake kwa kutufikisha hapa leo.

Mhe. Spika, mimi katika mchango wangu naanza katika ukurasa wa 6 sehemu inayosema Mipango Miji. Mipango Miji katika nchi yetu ya Zanzibar, Serikali pamoja na wizara inayohusika ilighafilika sana kuweka mipango miji, mipango miji ya nchi yetu mimi sielewi inasimamiwa na nani kwa sababu nchi yetu ya Zanzibar ndani ya ujengaji wa nyumba zimejengwa nyumba hazimo katika mipango miji. Nyumba zinajengwa kila mmoja ana uwezo wa kutoa kiwanja, ukenda kwa Sheha unapata kiwanja, ukenda kwa balozi ya nyumba kumi unapata kiwanja, ukenda kwa diwani unapewa kiwanja hata Mwenyekiti wa Umoja wa kinamama nae pia akiwa na uwezo anakupa kiwanja.

Sasa mimi nashangazwa sijui nani mwenye dhamana ya kumpa mwananchi kiwanja kujenga nyumba. Kwa hiyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuhakikishie nani mwenye dhamana ya ujenzi katika nchi hii. Kwa sababu tukitizama katika mji wetu kuna miji inaitwa Mtapepo, Chumbuni, Nyarugusu, Kwamtipura, Tomondo humu mote mna majumba yamo ndani ya mashimo ya maji, hata msikiti wetu pale Kwamtipura hivi sasa hata kusaliwa hausaliki, kwa sababu umejengwa ndani ya ziwa la maji.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mipango miji Zanzibar bado haijakamilika, kwa sababu kwa nchi za wenzetu tunapokwenda tunaona nchi za wenzetu miji imejengwa kwa ma-blocks hapa barabara inapita, hapa barabara yaani ukiwa na mgonjwa wako basi *ambulance* haipati tabu ya kuingia katika kijiji, lakini sasa hivi nenda Mtapepo uwe na mgonjwa basi labda hiyo *ambulance* ikaingie ndani ya shimo ndio apatikane mgonjwa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, bado mipango miji nchi yetu hajakuwa na usimamizi mzuri.

Mhe. Spika, nikienda katika Mahakama ya Ardhi, Mahakama ya Ardhi bado wananchi wengi sasa wanalamika kwenye Mahakama ya Ardhi.

Mhe. Spika, hivi sasa ukienda katika Mahakama ya Ardhi utakuta watu wamenyanganyana, sasa yule anayenyanganywa wakati anapokwenda kupeleka mashtaka yake jaji anaweza akasema huyu ameshinda, lakini uamuzi pale pale unabatilishwa kesi inarejea tena. Na ushauri huo kule katika jimbo langu kuna kijiji cha Pwani Mchangani kuna vijana wawili hata Mhe. Makamu wa Pili wa Rais vijana hao wameshamfika; Jaji anahukumu baada ya kwishakuhukumu anatoa *judgment* kwamba huyu ameshinda, baadae yule yule badala ya kupewa haki ile kesi inarudishwa tena anambiwa sasa uende tena. Sasa hii Mahakama ya Ardhi inahukumu vipi?

Mhe. Spika, bado kuna ubadhirifu katika Mahakama na ndio ikatokea ugomvi na mashaka katika nchi yetu kwa zile Mahakama hazihukumu kisheria. Sasa inakuwa kama ule usemi wa kileo "mwenye nguvu mpishe na ukiwa na nguvu ndio utapata haki" kama huna nguvu huna haki. Kwa hivyo, naiomba Mahakama ya Ardhi irekebishe, irekebishe mfumo uliokuwa nao.

Mhe. Spika, nakwenda katika sehemu hii ya Wizara ya Miundombinu.

Mhe. Spika, humu muna maagizo ya Kamati kurekebisha ujenzi wa bandari, lakini kuna mambo mengine humu Kamati imeghafilika kurekebisha barabara. Mimi naongeza marekebiso ya barabara, barabara zetu Zanzibar hivi sasa ni barabara ambazo zimeshazidiwa na magari, ni nyembamba na mbovu hasa ukienda barabara yetu ya upande wa Kaskazini Unguja utaikuta sasa hivi barabara madaraja kama makaburi, madaraja yamekuwa kama kaburi. Kwa hiyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aangalie madaraja ya upande wa Kaskazini yanahatarisha sana, madaraja mabovu na njia mbovu.

Mhe. Spika, kwa kuheshimu muda wako nakushukuru. (*Makofî*)

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii asubuhi hii ili niweze kutoa mchango wangu kwenye taarifa makini sana ya kaka yangu Mhe. Mahamoud, Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Miundombinu, ripoti ambayo nadhani ni ripoti mwanana kwa kweli na ni lazima tutoe maoni yetu kwa lengo la kusaidia Kamati na kusaidia Serikali kwa ujumla.

Mhe. Spika, nashukuru Wajumbe wa Kamati kwa jinsi walivyofanya kazi nzuri na hata ukiangalia uandishi wa hii ripoti yao ina tofauti kidogo na uandishi wa ripoti nyengine, kwa kweli wametia vitu vya maana sana, jambo ambalo nadhani wajumbe wenzangu watakubaliana na mimi kwamba hii ni ripoti ambayo imeandikika vizuri.

Mhe. Spika, nianze ripoti hii kwa kusema kwamba zipo changamoto nyingi ambazo wenzetu wametuonesha na changamoto ambazo wameeleza ni changamoto hasa katika maeneo ya huduma za wananchi. Kwa mfano, wameeleza changamoto kwenye Mamlaka ya Maji (*ZAWA*), wameeleza changamoto kwenye Shirika la Umeme (*ZECO*).

Mhe. Spika, mimi naomba niseme kwamba Wizara ya Maji ina watoto wawili ambao wote ni muhimu, ina mtoto *ZAWA*, ina mtoto Shirika la Umeme.

Mhe. Spika, Serikali naishauri sana kwamba iwache kuwagombanisha Mamlaka ya Maji na *ZECO*. Kwa nini nasema hivyo?

Mhe. Spika, haya ni mashirika ya Serikali ambalo lengo la mashirika haya ni kutoa huduma na hatimae mbeleni huko kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Lakini mzigo ambao mashirika haya tunawabebesha huku tukiendelea kuwanyima fedha Mhe. Spika, nadhani ni kuwadhalilisha hawa watu na tunawapa mzigo mkubwa.

Mhe. Spika, hivi sasa Mamlaka ya Maji kwa mfano wamelazimika kutotoa huduma kwa visima 31 vipyta ambavyo vimejengwa kwa gharama kubwa kwa sababu ya gharama ya umeme. Kwa hiyo, tumefanya utafiti Mhe. Spika, kwamba ili tuweze ku-*operate* maji kisima cha kawaida tu kidogo, kwa masaa 24, *ZAWA* wanahitaji kutoa umeme wa shilingi 250,000 kwa siku. Maana yake visima 31 ambavyo wangehudumia maji kwa siku ni zaidi ya milioni 1.50 mpaka milioni 2,000,000.

Sasa Mamlaka ya Maji ambayo inashindwa kutoa huduma kwa wananchi, lakini fedha ya kutoa huduma inashindika Mhe. Spika, nadhani imekuwa si wanyonge sana watendaji wa *ZAWA* na ni lazima Serikali sasa ifikie maamuzi ya kutafuta namna ya kuwasaidia *ZAWA* ili waweze kutoa huduma za maji Mjini na Vijini. Na hatuwezi kuwalazimisha *ZECO* kwamba lazima waweze kusaidia *ZAWA*.

Mhe. Spika, *ZECO* kwa upande wake ni shirika ambalo lazima litoe huduma lakini huduma zake ni za ghali mno hatuwezi kupata umeme ikiwa hatukulipa bili za umeme. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ushauri wangu ni kwamba *ZAWA* na *ZECO* kila mmoja lazima afanye wajibu wake kwa maeneo yake na ni lazima Serikali na wananchi wachangie maeneo haya ili taasisi zote hizi mbili ziweze kuchangia.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, mimi rai yangu kwa hoja hii ni kwamba sasa tuangalie uwezekano ikiwa wa tatizo la sheria, tuangalie uwezekano wa kuwapatia ruzuku za moja kwa moja Mamlaka ya Maji ili waweze kumudu kulipia gharama za umeme. Sio busara hata kidogo kuwakandamiza *ZECO*, sio busara hata kidogo

kuwakandamiza *ZAWA*, ni lazima Serikali ifidie gharama hizi za huduma za umeme na maji ili kila shirika lifanye kazi na liingize mapato kama ambavyo bodi zao walivyopipangia.

Mhe. Spika, jana hapa Mhe. Waziri wa Fedha alitoa mchanganuo wa fedha ambayo imepelekwa katika Wizara ya Elimu kwa ajili ya madawati, haikuleta ufanisi. Sasa ikiwa fedha ile haileti ufanisi kwa madawati ni kwa nini fedha ile isiingizwe kwenye mifuko ya *ZECO* na *ZAWA* ikaleta ufanisi na wananchi wakapata huduma nzuri za maji, wananchi wakapata huduma nzuri za umeme.

Mhe. Spika, sote hapa takribani wengi wetu wamesoma hapa bila ya kukalia madawati na sijasikia kama mtu amefeli kwa sababu hajakalia dawati. Kwa hivyo, nadhani kipaumbele ni maji kuliko dawati na hasa kwa vile wizara husika ya elimu imetuonesha kwamba hawawezi kusimamia kupatikana madawati, nashauri Mhe. Spika, wajumbe wenzangu wa Kamati zote tujenge hoja mwaka huu kwamba itafute namna ya kifungu cha fedha kingie moja kwa moja Mamlaka ya Maji kwa maana ya kufidia gharama za umeme na kingie moja kwa moja katika *ZECO* ili kuweza kulipia kwenye gharama zao.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu ukiangalia *ZECO* peke yako wana madeni ambayo wanadai makubwa tu na mdeni wao mkubwa ni Mamlaka ya Maji, ni lazima maji yapatikane. Kwa hivyo, suala la kurekebisha gharama za malipo ya umeme ili kupata maji ni suala la lazima na hatuwezi kuwaachia *ZAWA* na *ZECO* huku tukiwalaumu wakati njia ya kutatua Mhe. Spika, ipo.

Kwa hiyo, nashauri wawakilishi wenzangu bajeti hii ya keshokutwa tutafute jibu la suala hili ili tuweze kuwasaidia wenzetu wa Mamlaka ya Maji na *ZECO* ili wafanye kazi kwa mujibu wa maeneo yao na kwa ufanisi mkubwa bila ya kuwalaamu.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nizungumze ni suala la *ZMA*.

Mhe. Spika, ripoti imeeleza hapa kwamba Kampuni ya *Filtex* imefutwa baada ya kuonekana kwamba kuna udhaifu wa utendaji na bila shaka iliingiza hasara kwenye Serikali.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu naona kwamba haitoshi tu kutwambia kwamba kampuni imefutwa. Nadhani Serikali na Kamati ingetwambia ni kiasi gani cha hasara ambacho nchi imeingia kwa sababu ya udhaifu wa kampuni ile na wale walosababisha hasara kuna hatua gani ambazo zimechukuliwa. Lakini kufuta tu kampuni huku tukiri kwamba imetitia hasara Serikali bila ya kupata mchanganuo wa hasara iliyopatikana nadhani sio sahihi.

Kwa hivyo, Serikali na Kamati mimi naomba wanijibu baada ya matukio ya hasara ya Kampuni ile ya *Filtex* na mamlaka inayohusika Serikali ikaamua kufuta kampuni ile, ni jambo zuri, lakini vipi Serikali imeingia hasara na waliotia hasara wamechukuliwa hatua gani. Nadhani maamuzi ya kufuta kampuni bila ya kutueleza wananchi ni hasara gani imepatikana Zanzibar nadhani isingekuwa busara.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, nadhani akija na Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano akija basi watueleze baada ya kufutwa kampuni ile kuna hatua zipyi zilizochukuliwa baada ya kuingia hasara Serikali kwa mgongo wa kampuni ile ambayo wametia hasara kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, leo nimetembelea bandarini asubuhi, bahati nzuri bandarini asubuhi nilipotembelea ilikuwa mvua inanyesha, nimewashuhudia wafanyakazi wa *ZMA* na askari wetu pale bandarini wanakosa hata *raincoat* ya kujifichia mvua. Nilipouliza *raincoat* moja shilingi ngapi wameniambia *raincoat* ni shilingi elfu ishirini tano. Sasa *ZMA* inatarajia ifanye ufanisi wa usafiri wa baharini, lakini wanashindwa kuwashudumia wafanyakazi wa bandarini hata polisi wanashindwa kupata ma-*raincoats* ambayo gharama yake ni shilingi elfu ishirini tano. Na wale watu pale bandarini kwa siku si zaidi ya kumi, maana yake ishirini na tano mara kumi ni laki mbili na hamsini.

Namuomba Mhe. Waziri wa Miundombinu awashauri *ZMA* watafute makoti kumi yale wapatiwe wafanyakazi wa *ZMA* na askari ili ufanisi wa kazi bandarini uweze kufanyika. Wakati mvua inanyesha abiria wanapanda kwenye meli inawezekana kabisa mtu kufanya uhalifu kwa sababu ya wataalamu wa *ZMA* wa ukaguzi na askari wamejificha mvua. Kwa hiyo, Mhe. Spika, ni lazima makoti haya yapatikane ili wafanyakazi wetu bandarini waweze kuwa na makoti ya kujifichia mvua pale mvua inaponyesha.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nichangie kwenye ripoti hii ni suala zima la huduma za Viwanja vya Ndege (*Airports*).

Mhe. Spika, mimi nitaendelea kulaumu mpaka mambo yawe sawa, kwa sababu kwa kadiri ambavyo malengo ya Serikali yalivyopangwa bado hatujafikia ufanisi mzuri wa huduma za Viwanja vya Ndege, hadi hii leo Viwanja vya Ndege husani Pemba watu wanaendelea kupapaswa.

Mhe. Spika, dunia ya leo sasa ni utaratibu wa kupapasana tena basi, viko vifaa vya maana duniani kote ambavyo watu wanapekuliwa bila ya matatizo. Sasa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar hadi hii leo wanatumia *manually* watu wanapapaswa ili kuangaliwa amechukua nini, sio utaratibu mzuri.

Mhe. Spika, nadhani Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itafute vifaa vya kisasa na vilivyo makini ili watu wapekuliwe mizigo yao miili yao kwa utaratibu mzuri unalinda heshima za watu na unalinda maadili yetu kama Wazanzibari.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ningesema kwenye Viwanja vya Ndege, mtakumbuka wenzangu miaka mingi hapa tumekuwa tukilaumu kwamba Uwanja wa Ndege unakosa kampuni makini ya kufanya huduma za *handling*. Kwa muda mrefu Zanzibar tumekuwa tukitumia *ZAT* kama ndio mtoa huduma pekee kwa Viwanja vya Ndege Zanzibar.

Na nakumbuka hapa Zanzibar wamekuja makampuni mengi ikiwemo *Sea Port* ambayo Baraza hili humu ndani walikataa, walikataa kwa msingi kwamba tunataka tuwapatie uwanja mpaka wawekezaji wa ndani. Ni jambo zuri lakini nakumbuka pia ikaja Kampuni ya *Dnata* ya Dubai ambayo pia ilionesa nia ya kuwekeza katika Viwanja vya Ndege yetu, nao pia ikawa haina sifa ikakataliwa. Lengo ni kupata kampuni ambayo ina uwezo wa kutoa huduma na kuweka maslahi ya wananchi wetu mbele.

Mhe. Spika, zipo taarifa ambazo Mhe. Waziri na Mwenyekiti wa Kamati lazima naomba atwambie kwamba wakati Zanzibar wamekataa *Sea Port* na *Dnata* lakini zipo taarifa kwamba Mamlaka ya Uwanja wa Ndege na wizara kwa ujumla wametia saini mkataba na Kampuni ya *Transworld*, *Transworld* ni kampuni ambayo makao makuu yake iko Dubai. Wakati kampuni hii wanatia saini Dubai bahati mbaya wametia saini kule Dubai, hawakutia hapa Zanzibar.

Kwa hivyo, Mwanasheria Mkuu naomba utusaidie ni kwa nini kampuni hii watu wametia saini Dubai badala ya kutia saini Zanzibar, wangetia saini katika mazingira ya nchi, nadhani ingekuwa sahii. Lakini zipo taarifa kwamba mkataba wa Uwanja wa Ndege na *Transworld* umetiwa Dubai, lakini lakusikitisha Mhe. Spika, wakati mkataba huu unatiwa saini baada ya upekuzi mdogo wa ndani kampuni hii bado hajjasajiliwa hapa Zanzibar. Kuna uhalali gani wa kutia saini mkataba na kampuni ambayo hajjasajiliwa Zanzibar.

Mhe. Spika, huu ni mtihani mkubwa na ni lazima wawakilishi tukatae udhaifu huu, watu wameenda Dubai na wametia saini kampuni hata hajjasajiliwa na msajili wa makampuni hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Mwenyekiti wa Kamati na Waziri wa Miundombinu naomba watwambie nani waliohusika kutia kampuni hii saini kule Dubai na kwa nini wametia saini kampuni hii wakati si kampuni halali kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.

Mhe. Spika, nina hakika kwamba watu wamevunja sheria na mimi natoa wito kwa niaba ya wawakilishi wenzangu kwamba wakubwa wasivunje sheria, sheria za ndani lazima zidhibitiwe, ziheshimiwe na ni lazima zilindwe kwa maslahi ya Wazanzibari wetu. Kwa hivyo, wale waliohusika kwenda kutia saini kule Dubai watwambie wametia saini Dubai kwa idhini ya sheria gani, wamekwenda Dubai kwa nguvu gani.

Na zipo taarifa kwamba kampuni hii hata kwenye ushindani wa tenda haikuwa mshindi, kampuni ya kwanza, ya pili na ya tatu wameachwa wamechukuliwa kampuni ya nne, mtwambie misingi hiyo kutoka wapi, Sheria ya Manunuzi haikubali hivi, mtwambie Waziri wa Miundombinu mamlaka haya ya kuchukua mshindi wa tatu, wa nne, wa tano ambaye kuwa hakuchaguliwa na Bodi, nani katoa mamlaka hiyo, ni utaratibu wa sheria.

Mhe. Spika, mimi nasikitika inaelekea nilipoichunguza hii *Transworld* ni sawa sawa na *ZAT* ni mtu na ndugu yake, ni Mussa na Moses ni yule yule.

Mhe. Spika, ukicnhunguza *Transworld* na *ZAT* ni yule yule, yaani ni yule punda, jamaa amechukua kochi hili amelivua lakini yule ni yunda. Mhe. Spika, hili hatukubaliani na ni lazima sheria za ndani zilindwe.

Mhe. Spika, huu ni udhaifu na nini matokeo yake hayo ni matokeo ya kudharau ripoti za Kamati, Ingelikuwa Baraza hili Serikali wanazifata ripoti zetu haya yasingetokezea. Lakini mambo 10 yameacha watu wameona kwamba hakuna liwalo, yaani "*Business as usual*" ndio yale yale tu.

Mhe. Spika, hili hatuwezi kukubaliana na ni lazima Wawakilishi wenzengu tukatae udhaifu huu na tukatae Serikali kukandamizwa kwa nguvu za watu wachache amba si malengo na matakwa ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya Dr. Ali Mohamed Shein.

Mhe. Spika, mimi nimalizie kwa kusema kwamba ripoti hii naiunga mkono pale ambapo Mhe. Waziri na Mwenyekiti wa Kamati ataleta majibu sasa hasa kwa suala langu la *Transworld* na niwaombe Wawakilishi wenzangu kwamba bajeti hii tupange fedha maalum kwa ajili ya Mamlaka ya Maji na *ZECO* ili tuondoshe mgongano, *ZECO* wafanye kazi zao bila ya kukwama na Mamlaka ya maji wafanye kazi zao bila ya kukwama na wananchi wapate huduma. Mhe. Spika, nakushukuru sana. (*Makofit*)

Mhe. Salim Abdallah Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata muda mfupi huu kwa kutoa mawazo yangu kuhusu mada hizi zinazozungumzwa na moja kwa moja nianze na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Shirika la Umeme agizo namba 1(a) kutoka Kamati husika.

Mhe. Spika, Kamati imetoa maoni na maagizo yake katika kifungu hichi kuwa kamati hii inaiomba Serikali kuongeza vituo vya kuuzia umeme kwa Pemba mbali na vile viliyope vya Wete, Chake Chake na Mkoani.

Mhe. Spika, ni kweli na mimi naunga mkono hii ni kuwa tunapata tabu sana kule Pemba kwa sababu vituo hivi ni vitatu tu katika miji na wizara inaelewa kuwa imeeneza mita hizi za *TUKUZA* mpaka mashamba. Kwa hivyo, ikotokea hali ya dharura huwa tunapa tabu sana. Lakini kwa bahati mbaya utekelezaji ni kuwa Serikali kupidzia Sherika la Umeme imo katika juhudzi za kuongeza huduma za umeme ikiwemo kuongeza vituo imo katika juhudzi. Ingeliomba kujua katika juhudzi hiyo kimedhamiria kuongeza vituo maeneo gani mengine na juhudzi hiyo utekelezaji wake itaanza lini.

Mhe. Spika, nikiendelea niende kifungu cha 1(b) ukurasa huu huu wa tatu ambacho Kamati imeiangiza Shirika la Umeme kuhakikisha kwamba kila Taasisi ya Serikali ambayo hailipii umeme ikatiwe sambamba na hivyo taasisi zote ziwekewe mita za *TUKUZA* ili kulazimisha kulpia umeme kabla ya matumizi.

Mhe. Spika, mimi niipongeze sana Kamati lakini naipongeza zaidi wizara kwa mtazamo wake. Wizara kama ingeliufuta ushauri wa Kamati asilimia mia moja, kwa hivyo, nina hakika huduma nyingi sana zingelikosema, kwa mfano *ZAWA* ni taasisi katika wizara hii, inahudumikia kuwapatia watu maji safi na salama ambalo ni jambo la lazima na *ZAWA* hii inadaiwa na *ZECO* mabilioni ya fedha ikiwa ni kwa sababu ya umeme.

Lakini kama wanadaiwa watakatiba umeme maana yake kuwa Wazanzibari watakosa katika maeneo mengi na hii ni hatari. Kwa hivyo, ile taarifa ya kuwa watalifanya jambo hili kwa uangalifu kuangali na haja ilivyo. Mimi naipongeza sana wizara kwa hilo, lakini wakati huo huo naomba kutumia nafasi hii kwa sababu deni la *ZAWA* la umeme linatakiwa lilipwe na Wizara ya Fedha, naomba Wizara ya Fedha ihakikishe kuwa inalilipa deni na kumalizika ili tuendelee kupata huduma ipasavyo.

Nikiendelea Mhe. Spika, niende na suala la 2(a) na hili linahusiana na Idara ya Nishati. Suala hili liko katika ukurasa wa nne.

Mhe. Spika, Kamati imeagiza Idara ya Nishati katika hatua za uandaaji wa Sera ya Mafuta kuangalia uzoefu wa nchi za wenzenetu ambao waliwahi kupidzia mambo mbali mbali yanayohusiana na uzoefu wa uchimbaji wa mafuta na wizara imesema kuwa ina mpango wa uandaaji wa sera hiyo ya mafuta gesi asilia na Serikali imeunda kikosi maalum kinachoshirikisha sekta muhimu chenye uhusiano wa karibu na sekta hiyo ikiwemo Idara ya Nishati. Kwa Rasimu ya awali imeshatayarishwa na kuwasilishwa serikalini kwa hatua zinazofuata.

Mhe. Spika, mimi hii naunganisha pamoja na (b) ili nikitaka kujua kwa sababu Baraza lako tukufu lilifanya juhudzi kubwa sana kweli kweli kwa kufuatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano kongwe iliyoko kuiondoa mafuta na gesi asilia huwa ni mambo ya Muungano na yasiwe mambo ya Muungano na hakuna waziri hata mmoja kwa

upande wa Chama Tawala na upande wa Chama cha Wananchi CUF tunachongojea kuingia madarakani aliyepinga suala hili, sote kwa pamoja tulikubaliana kwa kupiga kura kuwa mafuta na gesi asilia yasiwe mambo ya Muungano.

Lakini kimazingira inavyoonesha na kwa sababu tunaambia kuwa Serikali ilipeleka watu kule Bara kuzungumza na Waheshimiwa wanahusikana na suala hili kulitoa katika mambo ya Muungano halijapata jibu sahihi. Mimi naipongeza wizara kwa kupeleka hata wanafunzi 30 kwa mkopo kuendelea na kupata mafunzo ya uchimbaji wa mafuta na gesi asilia na ninaamini wanasona katika nyanja mbali mbali ya mambo hayo.

Lakini hasa hebu tujue na hasa kutokana na kauli ya Mheshimiwa mmoja ambaye si vizuri kutaja jina lake hapa, alisema hata mafuta yangeliwa si ya Muungano Wazanzibari hawana mamlaka ya kuyachimba kama yao. Nikitakiwa ushahidi nitautoa halafu wenye watafuatilia.

Sasa nataka nijue hasa haya mafuta ni yetu au tunakwenda kusomesha watu wetu, kwa sababu Katiba inayotaka kupigiwa kura inasema Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi moja yenye mamlaka kamilii hatumo tena, mafuta haya tunashirikiana kuyachimba kama ki-Muungano. Nataka nipate maelekezo hasa vipi mafuta haya ni yetu na kama ni yetu tuzidi kujiardaa zaidi, kama hakuna jibu sahihi, tuambiane ili tujue na tutafute rai ili mambo haya yawezekane.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango katika wizara hii hii kuna kifungu namba (a), ukurasa wa 8 ambacho kinahusiana na ukarabati wa nyumba ya Kengeja. Kamati ilishauri zipatikane hizi milioni 200 kutoka Wizara ya Fedha ili hii nyumba ifanyiwe ukarabati mkubwa na nyumba imo katika hali mbaya sana inahatarisha maisha ya wakaazi wa mule na hamna pa kwenda. Lakini mpaka hivi sasa kwa mujibu wa utekelezaji ni kuwa fedha hiyo haijapatikana na inasuburi wa bajeti ijayo.

Ushauri wangu Mhe. Spika, kwa hili kwa sababu tunajali sana maisha ya binaadamu na Kamati imeliona hili na imetoa kama agizo, naomba wizara husika inayohusiana na utoaji huu wa fedha ijithadi kwa ku-save Matunda ya Mapinduzi na vile vile maisha ya wananchi.

Baada ya hapo Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa kwa ufupi sana naomba niende katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Lakini kabla sijaenda Mhe. Spika, kuna wenzangu walichangia jana hapa na mimi nikachanganyikiwa naomba nipate ufanuzi ni kuwa kuna mmoja alitoa kitandawili hapa "kuna mji wowote duniani amba hauna *parking* yake ya magari". Mmoja akajibu kwa sauti na alijibu sahihi akasema Zanzibar na ni kweli mtawanyo wa magari umeenea katika mji wote hapana mahali maalum kwa ajili ya huduma hiyo.

Sasa mimi nilifikiria kuwa kwa sababu hii Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Baraza la Mji linalohusiana na ukusanyaji wa fedha utiaji gari vyuma na kadhalika, sasa sijui kwa nini likaulizwa suala hili au kama sikufahamu vizuri mawaziri wawili wanajijua wanaohusika na swali hilo, kwa hivyo, nilitaka nipate maelekezo kwa sababu nilifikiria mimi binafsi Wizara hii ya Miundombinu hauhusiana na *parking* katika mji wa Zanzibar.

(a)Nashukuru tumeona picha hapa na hii picha ni ya meli ya kizigo na abiria hiyo mpya inayotarajiwa na meli hii imeitwa *MV*. Mapinduzi *II*. Mimi sipingani na neno Mapinduzi lakini naona kama tumeiga kuna *AZAM I*, *AZAM II* na kadhalika. Lakini sisi tulikuwa na Meli *MV*. Mapinduzi sio *MV*. Mapinduzi *I*, kwa nini hii ikitwa *MV*. Mapinduzi *II* na hili naomba jawabu.

(b)Hii meli naomba radhi nikosea ni picha tu hii inaonesha kama ina muundo wa Pantoni hivi sijui ni muundo wake au ni picha imepigwa kimakosa, naomba maelezo.

Baada ya hapo Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuendelea kuchangia katika Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano kama ifuatavyo na nitaanza na agizo la Kamati namba 3 lili ukurasa wa 3.

Mhe. Spika, Kamati imeitaka maelezo ya kina kwa kukosekana kwa fedha za kuendesha kazi ya uwekaji wa taa za kuongozea ndege na hapa kakusudia katika kiwanja cha ndege kilichoko Pemba.

Jibu kuwa Serikali imeagiza Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuweka taa katika njia za kurukia na kusimamia ndege katika Kiwanja cha ndege cha Pemba na mambo mengine yaneendelea.

(a)Mhe. Spika, mimi najua tokea nilipoanza kuja katika kipindi kile cha 2000/2005 suala hili lilikuweko na lilipigwa makelele sana kutokana na umuhimu wake na sote tunajua umuhimu wa kiwanja cha ndege kuwa na taa.

(b)Ilifiki mpaka tukaambiya kuwa kile kiwanja kitafanyiwa matengenezo makubwa sana na Mfuko wa Afrika Mashariki. Tulipata taarifa hii katika Baraza lako tukufu, tumekaa kimnya. Kwa vile inaumiza na kulikiwa na Mheshimiwa mmoja akasema kama Serikali haina fedha basi iwekwe japo mishumaa na yeze Mheshimiwa Mwenyezi Mungu akamjaalia kuwa waziri na akashindwa mpaka sasa yupo waziri aliekuwepo.

Mimi wa sababu Serikali inajua umuhimu wa kuwa na taa katika kiwanja chochote cha ndege, inaweza ikatokea *emergence* usiku ambayo ni ya hatari sana ikabidi ndege lazima zituwe na isiwezekane ikatokea jambo kubwa sana. Nataka nijue ni kwa sababu gani hasa kwa umuhimu ulionao wa taa za ndege mpaka leo ikabidi Serikali inaweza mipango na wala hakuna jibu la uhakika. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kama keshanukiza vizuri atueleze kiuhalisia ni lini kiwanja kile kitaanza kutumika katika hali ya viwanja vya ndege vinavyohitaji kutumika, isiwe ni kwa mchana tu.

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Salim Abdallah Hamad: Halafu kuna agizo namba 4 ambalo Kamati imetaka Serikali kuweka kipaumbele kwa kuiwezesha mamlaka ya usafiri wa baharini *ZMA* hali itakayopelekeza kuiwezesha kufanya kazi vizuri na kupunguza majanga yanayojitekeza mara kwa mara. Hii kwa sababu ya wakati naomba wizara isimamie maelekezo yake kama yanavyojieleza.

Kwa hivyo, niruke mpaka agizo namba 9, yaani hili ni suala la kupatiwa Viwanja vya Ndege fedha zinazokusanywa kutokana na huduma inazozitoa mamlaka kwa abiria yaani *Airport services charge*.

Mhe. Spika, tunaelewa kuwa pale katika Kiwanja cha ndege kunakusanywa fedha nyingi sana, lakini sijui, maelezo tunayopewa ni kuwa fedha ile takribani yote inakwenda Wizara ya Fedha na bahati mbaya pale hakuna fedha za kuendeshea shughuli nzima za ule Uwanja wa Ndege amba o ule ni wa kimataifa na kuna mambo mengi yanahitaji kutekelezwa na kutotekelizwa kwake ni kuteremsha ile hadhi ya kimataifa.

Hivyo, mimi naomba nijue, ni jambo lipi hasa wakati halifanyiki katika baadhi ya Viwanja vya ndege viliomo hapa Tanzania ya kukusanya kodi yote ikapelekwa serikalini. Ni jambo gani lililofanywa na Serikali ikachukuwa fedha zote wakati inajua hasa kuwa pale panahitaji fedha kwa sababu ya huduma kadhaa na kile kiwanja kiweze kuendelea kutokana na na hadhi yake na hili ombi lililotolewa na Kamati litatekelezwa vipi.

Halafu kwa sababu wa wakati niende katika agizo namba 11 lililoko ukurasa wa 6 na agizo hili namba 11 Mhe. Spika, ni kuwa limeagizwa kwa kujengwa Kituo cha Polisi katika Kiwanja cha ndege cha Pemba, lakini jibu ni kuwa Polisi wanapatiwa chumba ambacho watafanyakazi zinazostahiki na kituo hicho hakuna mpango wa kujengwa tena.

Mhe. Spika, Kamati ikisema jambo imefanya utafiti na imeenda mbali. Kwa hivyo, mimi sikubaliane kuwa kupatikana kwa chumba kidogo pale kuwa ndio suluhisho, nasisitiza msisitizo wa Kamati kuwa Polisi watejengewde kituo chao kwa maslahi ya kufanyakazi zao kwa ufanisi na kwa sababu ya wakati kifungu namba 15, ukurasa wa 7 kuna utekelezaji wa minara.

Mhe. Spika, kwa ufupi nataka nijue kwa sababu kama kumbukumbu zagu ziko sahihi mnara ya Kigomasha ujengwa mwaka 1900, toka nikisoma *Primary* nikaona hiyo pengine inawezekana nimesahau na nafikiri ilikuwa *expire date* yake ni mwaka 1960m nafikiri nilisoma miaka hiyo kabla ya Mapinduzi. Sasa sisi tunaendelea kuufanya ukarabati mnara huu amba ni wa zamani sana.

(a)Je, kutokana na uzee ulivyo mbali na mnara kuonekana lakini kihuduma, unatoa huduma sahihi inayotakikana kutokana na wakati kwenda mbele.

(b)Bado utaendelea kuwa na usalama wowote kwa wanaotumia mnara ule, naomba kupewa maelezo.

(c)Wenzetu wameomba kuangalia japo kujengwa Gati ndogo kule Nungwi na mpango huo haupo lakini Mhe. Spika, Zanzabar imekuwa kulikuwa na watu laki tatu, sasa tuko milioni mia moja laki tatu na, mahitaji yamekuwa safari za Unguja na Pemba zimeongezeka Pemba na Unguja kwa Nungwi ndio karibu zaidi. Kuna sababu gani za msingi hasa na wakati Gati ikijengwa biashara itakuwa na biashara na wizara itajiedesha vizuri, kutotilia maanani umuhimu wa ombo la Kamati na kuona kuwa kwa Zanzibar kuna alau Bandari mbilikubwa; moja hii hapa tulionyayo na nyengine iwe ya Nungwi, itakuwaje Pemba kuwe na Bandari tatu, lakini Zanzibar kuwe na moja tu kwa hilo naomba nipewe jibu.

Mwisho, naomba nipate maelezo sahihi kuhusu ujenzi wa Gati ya Mpigaduri, siku zote ilikuwa tunapata taarifa hizi na zile wakati wafadhili walikuwa wanakuwa na kuondoka na sasa hivi naona kuna azimio. Mimi ninataka nipewe taarifa sahihi njue.

Mhe. Spika, ninashukuru, ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana. Ni zamu yake sasa Mhe. Hamad Masoud Hamad.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa mara ya pili siku ya leo kunipa fursa ya kuchangia taarifa hizi mbili za Kamati ya Mawasiliano ya Ujenzi na zile taarifa ambazo ni utekelezaji za maagizo ya Kamati zilizotolewa na Mawaziri husika.

Mhe. Spika, mimi nina mambo matatu madogo na ninaamini sitochukua muda mrefu. Nimemuona kaingia hapa Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Hamza Hassan Juma na nafikiri kwa sababu asubuhi uliwaita walikuwa hawapo, pengine wanaweza wakapata nafasi na wao, ninasema pengine mamlaka anayo yeye. Mhe.Hamza, umefurahi kweli kweli, eeh! (*Kicheko*)

Mhe. Spika, mimi nimo katika malipo ya fedha taslimu katika kulipia huduma za maeneo yote yaliopo katika Wizara mbili; Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Spika, wakati mmoja nilifanya *pilot project*. Kuna shirika wanaopata huduma walikuwa wanalipia fedha taslimu kwenye kidirisha. Kama una shilingi elfu kumi, laki moja, milioni tano, zote unazokwenda vile kama benki, zinahesabiwa pale. Kwanza ukiwa na fedha nydingi unachukua muda mrefu watu kuhesabu na wakati huo, shirika hilo lilikuwa halina *counting machine*. Kwa hivyo, ilikuwa ni kuhesabu kwa mate na kidole, unaweza ukafika elfu hamsini na tano, lakini akija mtu akikupa *salamu aleykum* ukiitia unaanza upya na ndiyo tatizo la kuhesabu pesa kwa kidole.

Mhe. Spika, makusanyo katika *system* kama hii ilikuwa ni kama milioni nane kwa mwezi. Lakini utaratibu ulipobadilishwa kwamba ye yote ambaye atalipia huduma ya zaidi ya shilingi elfu15, aende akalipe benki na pale aje na *pay slip*. Kwa hivyo, mtoa huduma akishaona ile risiti kwamba umelipa kwenye akaunti yao, yeye atakupa huduma. Mhe. Spika, unaweza ukashangaa lakini makusanyo, huduma ni hizo hizo siyo kwamba kuna huduma zilibadilika, *yali-shoot* kutoka milioni nane kwa mwezi hadi milioni 27.

Kwa hivyo, unaweza kuona athari ya watu kukusanya pesa taslimu na athari ya kukusanya pesa *through bank* ulivyokuwa mkubwa. Hivyo, mimi nashauri sana kwa Wizara zote hizi mbili na Wizara nyengine, malipo ya fedha taslimu kwenye kidirisha basi wayaangalie vizuri na iwe ni fedha ndogo sana iruhusiwa kulipa pale *cash*. Ninasema hii ni juhudhi ya kuipatia fedha Serikali yetu ili fedha hizo ziweze kutumika.

Vyenginevyo, Mhe. Spika, fedha taslimu zina bilisi, zina shetani. Huwezi ukawa na milioni 15 kwenye bweta na siku ile ile huzipeleki benki, zinaweza zikaabiwa pale au hata wewe ukawa *attempted* hasa ukasema aah! mshahara keshokutwa ngoja nichukue hizi kidogo nitakuja kuzilipa. Kwa hili ilikuwa ni *observation* ya kwanza ambayo nasema inakwenda kwa Wizara zote mbili.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu bandari ya Wete. Kuna habari zimezigaa kwamba Bakhareesa mzalendo anakusudia kuijenga bandari ya Wete. Juzi lilzungumzwa lakini bado nilikusudia hasa kulipata sikupata. Kwa

hivyo, pengine hapa nitalipata leo. Labda Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie hili jambo kweli na kama lipo kweli, lipo kweli vipi na limefika hatua gani.

Mhe. Spika, mimi nampongeza sana Bakheressa kwa juhudzi zake za kuisaidia Zanzibar kama Mzanzibari na mfano mmoja mionganoni mwa mifano ni pale bandarini sasa hivi. Mtu aliyejukua Zanzibar miaka mitatu iliyopita na akawa amekuja tena sasa hivi, jana au juzi anaweza akashangaa. Hangeweza kuamini pamefanana kabisa na *Hamburg*, huduma safi, *very efficient*, wafanyakazi wana nidhamu na *Alhamdulillah* kila anayepita pale anasema kweli na kila siku Bwana Bakheressa anaongeza. (*Makofî*)

Kwa hivyo, mimi naunga mkono sana hatua hii ya kutaka kujengwa bandari sehemu ya Wete, lakini kwa faida ya Baraza hili la Wawakilishi na wananchi, huu uvumi mwingi kuwa kunataka kujengwa, sijui hakujengwi na mashine zimeshafika, nafikiri Waziri akaondoa hichi kiwingi ili tukapatataa tarifa vizuri.

Mhe. Spika, jambo la tatu, ni kuhusu *e-Government*. Ninaliweka hapa kwa sababu hili lina wazazi wawili; kuna Wizara ya Fedha na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Sasa kama Wizara ya Fedha wapo, kenda kunywa chai naambiwa hapa, lakini Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano yupo anaweza akatujibu yale yanayohusika.

Mhe. Spika, *e-Government* kwa Zanzibar ina historia kidogo. Imeanza na mkonga wa kitaifa na awamu ya kwanza ya mradi wa *e-Government* kuweka huo mkonga wenye ni mkopo kwa Serikali ya Zanzibar hata kama ilipitia Serikali ya Muungano, lakini nasema tunaotakiwa kulipa ni sisi Zanzibar ya dola kama milioni 20 hivi.

Mradi huu awamu ya kwanza inaonekana umekamilika, lakini Mhe. Spika, sisi mimi, wala siyo Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati hii, kwamba ameona hasa hizi dola milioni 20 hadi sasa, mbona yale matumaini na matarajio ambayo tuliambiwa yatapatikana hayaonekani. (*Makofî*)

Mhe. Spika, inaonekana kama sasa hivi mradi huu, sijui umetelekezwa kwa kweli hakuna shughuli nyengine yoyote inayooonekana. Juzi Mhe. Hija Hassan Hija, alisema hapa, hii *station* ambayo ni *main station* itakayo-control mambo haya ya *e-Government* iliopo Mazizini hapa mkabala na Ofisi ya Vitambulisho, ameeleza Mhe. Hija, hapa kwamba Ofisi ile ilijengwa kwa gharama kubwa na tuliambiwa kulikuwa na *equipments* ya uhakika; kompyuta na vitu chungu nzima.

Sasa amesema hapa, kweli tulikwenda kutembelea mradi ule sisi tukaona mambo mazuri tu, kuna *AC* pale ukiingia wewe unaweza uka-*freeze*, makompyuta haya ya kisasa. Lakini taarifa tulizopitaa baada ya kuondoka kwamba jamani, eeh! yote hii ilikuwa ni kama *flange*, hizi kompyuta siyo za ofisi hii zinaazimwa. Mhe. Spika, ni mtihani mkubwa. (*Makofî*)

Sasa ninakuja nilipokusudia kutaka kusema. Mhe. Spika, kuna balaa jengine linakuja. Kuna *project* inaitwa *e-Health* lakini jina hasa la mradi ni *Tele-Health Solution for Zanzibar*. Mimi nimeoneshwa mpaka ma-documents yote na nimeoneshwa kwa sababu gani. Hawa wanaoshughulikia hili ni watu wa kati na kati hao, siyo *creators*, yaani siyo waombaji, wanasema hili ni balaa jengine. Mradi huu wa *Tele-Health Solution for Zanzibar*, utaigharimu Zanzibar dola milioni 30. Mhe. Spika, na watu wapo mbioni. (*Makofî*)

Sasa mimi muono wangu na naamini wengi wa Wajumbe hapa ni kwamba na huu nao ni mkopo na ndivyo ulivyo kabisa, hakuna atakayekupa pesa hizo bure. Ni mkopo utakaotolewa na hao hao waliota dola milioni 20. Sasa hizi milioni 20 tu hadi sasa hatujaona hasa manufaa na matarajio tuliyopewa. Kila ofisi unayouliza hapa mumeshaunga nyinyi mkonga, wanasema aah! umepita tu hapa. Ni *very few offices* ambazo zimeunga na ndiyo umekwisha na wameshakaa kitako, pesa haipo tena, mradi hauendelei. Kwa hivyo, hakuna manufaa yoyote hadi sasa yaliyopatikana, ni *cable* tu ipo chini ya ardhi kama maiti. (*Makofî*)

Sasa leo dudu jengine linaletwa *thirty three million dollars*. Haya ma-documents Mhe. Spika, ukiyaona unapenda uyakumbatia kwa uzuri. Mimi nasema chonde chonde, huu ni mwenendo jamani, tena ni muendelezo wa kuwatwika Zanzibar deni, lote totalipa siye.

Mhe. Spika, ukiachilia mbali kwamba *e-Health* sasa hivi ni zaidi kimo chetu kwa hapa Zanzibar. Mhe. Spika, ninazzungumzia *e-Health*, wakati unakwenda hospitali choo hakisafishwi, dawa unazoandikiwa asilimia 60 hazipo. Daktari ile gari ya kutoka nyumbani kwake mpaka hospitali hana, *ambulance* kama kuna Chake Chake na mahali kwengine ipo lakini unaambiwa haina mafuta. Yaani mgonjwa anataka *ambulance* utoe mafuta na ndiyo maana siku hizi Pemba majimbo mengi sana, kuna majimbo kama manane, moja likiwa Jimbo la Ole, la

pili ni la Mkanyageni, la tatu la Ziwanu na Mhe. Omar Ali Shehe juzi ndiyo kafanya kufuru, kaleta *ambulance* kwa Tanzania nzima ni mbili tu; moja ipo Chake Chake, moja ipo *Regeants Hospital* Dar es Salaam. (*Makofî*)

Mhe. Spika, sasa nasema hata mafuta ya *ambulance* kwa gari ya Serikali hayapo. Leo unakuja kujitwika mashaka mengine kama haya ya *e-Health*. Hii Mhe. Spika, tutatake tusitake ipo juu ya kimo chetu na huu mimi nasema ni mpango wa walaji tu. Kuna siku tukijaaliwa tunakusanya taarifa tu zikamilie, tutakuja kutoa *break down* ya *twenty million dollars* za awamu ya kwanza. Serikali hasa zimekwenda ngapi.

Sasa hii nyengine ya *thirty three million dollars* ndiyo inakuja hiyo na watu walivyo na ujanja inaweza ikapita hiyo. Hii inaweza ikapita, watu wakachukua mkopo kwa sababu mambo mengi ya hapa Mhe. Spika, yanafanywa chini kwa chini, unakuja kushitukizia wewe *missiles* zimeshawekwa, ma-experts washafika watu wanakodi majumba, kuna nini, aah! kuna mradi huu.

Hii ndivyo *system* inavyokwenda hapa tusifichane. Mimi nafikiri huko mbele Kanuni za Baraza la Wawakilishi au hata ile hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma, tuingize mambo haya. Moja ya mambo yetu jamani hii mikataba kabla hajaletwa hapa au hajatiwa saini, basi angalau na sisi tuione. Kweli hamna wanasheria wengi, wamo wanasheria wapo kidogo. Lakini kuna watu wana macho wanaona, kuna watu humu wana fani mbali mbali. Unajua kabisa kwamba mmh! hii balaa na sisi ndiyo tunaowakilisha Wazanzibari wote majimbo 50 hapa.

Kwa hivyo, tukidhirika sisi na wale wenzetu watakuwa wameridhika. Lakini mambo haya bwana ya kufungiwa ngulai. Kwa hivyo, mimi nashauri sana kabisa, kabla ya Serikali haijafika mbali na hili, suala hili lipo juu sana ya wenzetu kiuchumi na kiteknolojia. Kwa nini tunatafuta kimo kwa kinu. Mimi ndiyo tafsiri yangu hiyo.

Tunataka tufike hapo, wewe unyooshe kwa mikono lakini wewe unatafuta ngazi, ukitolewa ngazi unaanguka imekwisha habari. Mhe. Spika, kwa hivyo, mimi mchango wangu katika hili, chonde chonde mradi huu wa *Tele-Health Solution for Zanzibar* aah! kwanza hoo! (*Makofî*)

Uchaguzi ni mwezi wa Oktoba. Mara nyingi kipindi hichi ni cha lala salama. Kila mtu ana hakika kwamba matokeo yake ya uchaguzi yatakuwaje, nitakuwepo au sitokuwepo. Kwa hivyo, hapa ndiyo watu wanaofomea. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano analipenda neno hili "kufofomea", yaani unakula hapa hujameza na mkono huu una andazi na mkono huu una kuku, hapa umeweka chupa, almuradi kila kitu unataka ule. Kwa hivyo, hichi ni kipindi cha lala salama. Nimetowa indhari hii wa Serikali wanaskia, kipindi hichi mambo haya ya kuwataka kuwatwika Wazanzibari mizigo ambayo hawaiwezi angalau yasimame tuangalie huko mbele yatakuwaje.

Mhe. Spika: Una dakika 5.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, mradi wa *Tele-Health Solution for Zanzibar* ambao ni *e-health* is very very far beyond our reach. Hatuna uchumi huo, deni hili ni kubwa lile la milioni 20 bado hatujajuwa manufaa yake, basi angalau tusirukie hapa. Mimi napenda sana tuwe na Serikali, kuwe na *e-Government* lakini jamani pole pole. Hili la kwanza angalau tulione limefika wapi ndiyo tulichupie hilo jengine.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa muda. (*Makofî*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Hamad Masoud Hamad. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Farida Amour Mohammed, ameomba dakika 5. Mhe. Ismail Jussa Ladhu, nilikwita ukawa hupo, sasa baada ya Mhe. Farida na wewe upate dakika chache ili kuweza kuchangia kabla sijamkaribisha Mhe. Waziri Mohamed Aboud.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante sana Mhe. Spika, ninakushukuru kwa klinikubalia ombi langu la kunigaiwa dakika 5 za kutoa mchango wangu mdogo sana katika Wizara hii.

Mhe. Spika, kama ulivyonigaia dakika tano basi nataka nitumie dakika tano. Nataka nije kwenye Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, nije katika agizo la Kamati namba15.

Mhe. Spika, agizo hili namba 15 maelezo yake yameitaka Serikali kuzikarabati bandari ambazo hazipo katika kiwango kizuri, hali inayopelekea kutumiwa kinyume na utaratibu na kuikosesha Serikali mapato kutokana na kutokuwa na ofisi zinazosimamia harakati za kila siku za bandari hizo. Kwa mfano, Bandari ya Mkokotoni.

Lakini katika majibu huku ya Mhe. Waziri ya utekelezaji kasema shirika limepanga mradi wa ujenzi wa gati za Mkokotoni na Tumbatu katika bajeti yake ya mwaka 2014/2015, pamoja na gati ya Wete. Lakini pia kaendelea

kama utaratibu wa mradi huo unaendelea ambapo kazi ya kufanya uchunguzi wa kimazingira katika maeneo ya ujenzi yaani Mkokotoni na Tumbatu umekamilika. Sambamba na kazi hiyo shirika limeanza kukusanya vifaa vya ujenzi Tumbatu na tayari shughuli ya ujenzi itaanza.

Mhe. Spika, naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri, wizara pamoja na watendaji kwa jumla, kwa hatua hii ya bandari hizi mbili ya Tumbatu na Mkokotoni. Lakini juu ya kuwa imetajwa hapa Bandari ya Wete, lakini sikuona utekelezaji wake ukoje.

Mhe. Spika, nimekuomba dakika tano kwa uchungu kwa sababu ya jambo hili, kila bajeti mimi nalipigia kelele lakini bado hatujaona utaratibu wake kuchukuliwa hatua.

Mhe. Spika, nianze na mji wa Wete, Wete ni mionganoni mwa wilaya iliyokuwa ina wakaazi wengi, pia sitosema kwa Wilaya ya Wete, kwa Mkoa mzima wa Kaskazini una wakaazi na wafanyabiashara wengi na kama Serikali italizingatia hilo katika ujenzi wa bandari, basi ina hakika Serikali itakuwa na kipato kikubwa katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, bandari hii ya Wete tokea mwaka juzi ilipozama *MV. Spice* mpaka leo hii hakuna usafiri wa uhakika, hakuna hasa usafiri unaofikia pale Wete, sio wa uhakika, hata huo wa kufikiria hakuna. Sasa Mhe. Spika, hili ni tatizo. Katika ajali ile waathirika wakubwa wa *MV. Spice* ni watu wa Mkoa mzima wa Kaskazini Pemba, ndio watu wengi walioathirika na ajali ile.

Lakini kwa bahati mbaya sana hadi hii leo hatujaona kufanyiwa angalau chochote kile cha kuonesha tu kwamba ile Bandari ya Wete inajaliwa na itafanyiwa ukarabati angalau nayo ionekane vyombo vinakuja pale kwa kuondosha usumbufu kwa wananchi wa Mkoa wa Kaskazini na pia kuwapa angalau nafuu wale wafanyabiashara wa Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Mhe. Spika, katika utafiti uliofanyika Wilaya ya Wete au ule mji wa Wete una wakaazi wengi sana kutokana na maelezo ya utafiti wa sensa iliyopita ya mwaka 2012. Lakini pia idadi ile ya watu hajachukuliwa uzito wa aina yoyote.

Mhe. Spika, kukosa bandari pale Wete kunadumaza wafanyabiashara na pia kiuchumi, kwa sababu bandari ile ingeleta faida kubwa kwa uchumi, Kimkoa, Kiserikali kwa jumla na wafanyabiashara wenyewe pia wangepata faida. Lakini hilo halioneekani.

Mhe. Spika, katika kipindi cha nyuma nilichangia hapa katika bajeti, ilitokezea tukaambiwa kama zitawenza kufunga gati meli pale zile za Bakharesa, kama Kilimanjaro I, II na III, inatakiwa ile bandari isogezwe mbele mita 20. Mhe. Spika, hivi kweli niulize Serikali imeshindwa nini angalau kukubali kuongeza ile mita 20 tu kule mbele ili ile Bandari ya Wete nayo ikafufuka, bandari imekufa tena imekufa katika kifo kibaya, hadi hii leo hakuna hatua yoyote iliyoachukuliwa katika eneo lile.

Mhe. Spika, mfanyabiashara anayetoka Msuka, Micheweni atoke na biashara yake mpaka Mkoani, akifika Mkoani asafirishe kupeleka Unguja, ambapo mazingira yetu sisi ni ya kibiashara na mji wetu ni wa kisiwa, Pemba Unguja, Pemba Unguja ndio biashara zetu. Sasa kweli mtu huyu biashara hii hata akifika nayo Unguja, atapata faida au ni faida kwa wenye magari.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naiomba hii Serikali kwa kupitia kwa Mhe. Waziri ulichukulie uzito suala hili na pia unijibu haswa, unipe ratiba maalum. Hii gati ya Wete utekelezaji wake utakuwa lini au mwaka gani, ili angalau na wale wananchi wa Mkoa ule wa Kaskazini wawe na imani na Serikali yao.

Mhe. Spika, sina maelezo mengi kwa leo, lakini eneo langu kubwa katika wizara hii moja lilikuwa ni hilo.

Mhe. Spika, jengine nataka niende kidogo katika ujenzi wa barabara. Mhe. Spika, katika ile barabara ya Wete Gando, kuna kijiji kimoja pale kati, kijiji kile kimetenganishwa na ile barabara katika ujenzi. Barabara kongwe ya zamani ilikuwa pale pale inapita sawa sawa, lakini baada ya ujenzi wa barabara mpya, basi kile kijiji chao kimetengwa kidogo na ile barabara. Sasa pale pamekuwa na usumbufu mkubwa, kwa sababu kuna mtaro na mtaro ule unaleta dhiki kubwa hasa kwa wanawake, huwezi kuchupa mpaka kwanza ushuke uingie kwenye mtaro, kisha ndio upandishe juu.

Kwa hivyo, naiomba wizara iliangularie hili kwa kuwaonea huruma wananchi wale wa eneo lile hasa wanawake katika kulifanyia ukarabati eneo lile.

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, namshukuru Mola wangu kwa kutuamsha kuwa hai na wazima tukaweza kuendelea na shughuli zetu. Nakushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii. Niombe radhi kwamba kweli uliniita, lakini nilikuwa na shughuli nyengine kidogo, uliniita jina la mwanzo nilikuwa bado sijaingia Barazani. Nashukuru kwamba bado umenifikiria kunipa nafasi.

Mhe. Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, kwa hivyo, kwa sababu hiyo sitojikita sana katika mambo mengi ambayo tayari tumeshazungumza na wizara zinazohusika. Niseme tu kwamba kwa jumla nataka nipongeze, kwamba pamoja na misuguano mingi iliyokuwa inajitokeza katika taasisi mbali mbali, lakini ufanisi unapatikana katika baadhi ya maeneo, tunaona kuna *improvement* kutoka pale tulipokuwa.

Kwa hivyo, hilo nashukuru, matatizo hayeshi tutaendelea kuyasema kwa sababu ndio wajibu wetu, tumechaguliwa na tunalipwa tufanye kazi hiyo kwa ajili ya kuwasema wananchi wa Zanzibar. Lakini kwa jumla nasema yako maeneo ambayo tunayapongeza. Kwa sababu ya muda sitaki kutaja taasisi moja moja, lakini kwa jumla nazipongeza taasisi zote ambazo zinajitambua katika vikao vyetu tulipongeza, kwa kazi ambayo wamekuwa wakifanya na mabadiliko ambayo tumeyaona.

Mhe. Spika, mimi kuna maeneo machache tu ambayo nilikuwa nataka kuyawekea msisitizo na kwa sababu pengine baadhi yetu tunakawaida hizi ripoti hatuzisomi kwa kina tukishapewa hapa, hasa wale waliokuwa wamepewa dhamana Serikali, nilikuwa nadhani kuna baadhi ya masuala yanahitaji kupewa msukumo mkubwa zaidi ili Serikali ijichunge na ijirekebishe na mambo haya ambayo Kamati imeyataja hapa.

Moja Mhe. Spika, ambalo ningependa nilizungumze naanza na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, ni suala linalohusu mamlaka ambazo zinapaswa kuhudumiwa na taasisi za Muungano.

Mhe. Spika, Zanzibar ilipokubali kuungana na Tanganyika, haiku-*surrender sovereignty* yake, ilichofanya ni *ku-share sovereignty* yake Tanganyika. Maana yake taasisi ambazo zimeundwa kuhudumia Muungano zinapaswa zihudumie Tanganyika na Zanzibar kwa misingi ya usawa na heshima ile ile. Ripoti yetu imebainisha matatizo ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania, jinsi inavyokwamisha ndege za Kimataifa zinazotaka kutua Zanzibar. Mojawapo kiwa ni *Qatar Airways*, lakini nashukuru baada ya kulisema hili na limefika katika majukwaa ya kisiasa Makamu wa Kwanza wa Rais alilizungumza hili na baada ya sisi kulisema kwamba tutalifikisha mbali, nashukuru kuwa limekwamuka juzi kwamba *Qatar Airways* imetangaza rasmi kwamba kuanzia Julai itakuwa inaleta ndege zake Zanzibar.

Lakini yako mashirika mengine kama *TAK Share lines*, tuliambiwa kuna Shirika la Abudhabi liliomba kitu kama hichi, bado *TCA* inaonekana inahujumu kwa makusudi uchumi wa Zanzibar kwa kuyakatalia mashirika haya.

Lakini hapo hapo niunganishe Mhe. Spika, vile vile tumepeata malalamiko ya Mamlaka ya Usafiri Baharini (*ZMA*), kwamba Zanzibar ndio pekee katika Jamhuri ya Muungano ambayo ina usajili wa meli wa kimataifa. Lakini kuna sheria inayoitwa mkataba wa kimataifa, *Maritime Label Convention*, ambao unapaswa usainiwe na kuridhiwa na Tanzania, ili tuweze kuwafaidisha vijana wetu kupata ajira katika masuala ya meli zile za kimataifa zilizosajiliwa Zanzibar. Vijana wa Zanzibar wanakosa kufaidika na fursa hizi kwa sababu tu Tanganyika hawataki kuridhia hili kwa kuititia jina la Jamhuri ya Muungano. Kwa hivyo, nasema na hili Mhe. Spika, litizamwe. Yako mengine sitayagusia kwa sasa.

Jengine Mhe. Spika, ni lile ambalo nawaomba Waheshimiwa Wajumbe sana, waangalia ukurasa wa 57 na 58 wa ripoti hizi za Kamati, ambapo kuna ripoti yetu kuhusiana na suala la uamuvi wa kusitisha mkataba wa Kampuni ya *Philtex*.

Mhe. Spika, Kampuni ya *Philtex* imesimamishwa baada ya malalamiko mengi, lakini baadae kuna balaa jengine linaitwa *Al-Khaleej Industry* limeingizwa humu ndani. Mhe. Spika, tulidhani kwamba viongozi wetu watajifunza baada ya matatizo ya *Philtex*, lakini bado inaonekana mamlaka inayohusika haikupewa fursa ya kufanya maamuvi, badala yake bila ya kutafuna maneno baada ya kuwahoji, tuaambiwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndiyo iliyopeleka agizo kwamba wamchukuwe *Al-Khaleej Industry* kufanyakazi iliyokuwa ikifanywa na Kampuni *Philtex*.

Tukawaauliza kwamba je, nyinyi wenyewe mmeridhika, wakasema sisi tumepewa maagizo na wakubwa. Lakini cha ajabu zaidi yale yote ambayo waliahidiwa kwamba yangetekelezwa na *Al-Khaleej Industry* katika kusimamia ule uwakala wa usajili wa meli pale Dubai kuititia Ofisi ya Sharja, yametekelezwa labda kwa asilimia 30 au 40. Kwa hivyo, kumeanza kuonekana matatizo licha ya yale ambayo yalikuwepo katika *Philtex* hata hatujafika popote. Kwa hivyo, niwaambie wakubwa, waache kuziingilia mamlaka hizi kuingiza mambo yao.

Mhe. Spika, kwa hivyo, nilikuwa nasema suala hili niliwaomba wajumbe wasome sana katika ukurasa wa 57, 58 tulielewe hili kwamba pana tatizo jengine linakuja. Naomba kwa sababu ya muda ulionipa mchache Mhe. Spika, niondoke Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, niende katika Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Spika, hapa kuna suala jengine vile vile naomba Serikali ije na majibu ili kuwaondoshea mzigo wananchi wa Zanzibar wenye hali ngumu ya maisha na sisi tunawaongezza ugumu. Katika ukurasa wa 52 na 53 Mhe. Spika, wa ripoti ya kamati tumezungumzia suala la deni ya *ZECO* wanalodaiwa na *TANESCO*. Kwa sababu ya muda sitoisoma sehemu yote. Lakini katika ukurasa wa 53 inaonekana kwamba bei ya umeme Zanzibar na inakuwa pia mzigo kwa *ZECO*, kwa sababu kuna asilimia 31 ambayo imeshakubaliwa kwamba ni punguzo la bei kwa umeme wetu wa Zanzibar. Lakini bado *TANESCO* inalitoza pale pale.

Mhe. Spika, kuna tozo ya kugharimia umeme wa vijiji Tanganyika, wanatozwa Wazanzibari asilimia 3, kuna tozo ya *EWURA* asilimia 1 inatozwa Wazanzibari, wakati *EWURA* aihudumii Zanzibar. Lakini vile vile *ZECO* wametuambia kuna bei kubwa sana ya umeme wanaouziwa wa *KVA* amba ni tofauti na kima kinachotumika kuwauzia Tanganyika.

Sasa Mhe. Spika, utakuta haya maeneo manne ukiyachanganya yanaifanya bei ya umeme Zanzibar kuwa kubwa na kuwa mzigo kwa *ZECO* na ndio maana deni la *TANESCO* maisha halimaliziki vile vile. Lakini zaidi Mhe. Spika, *ZECO* wanatuambia kwamba wao wana mradi wa kusambaza umeme vijiji hapa, wanashindwa kuhudumia kwa sababu ya ukosefu wa fedha, fedha ya Wazanzibari wanaingiziwa kodi ya nyongeza kwenda kuhudumia umeme wa vijiji Tanganyika, wakati na sisi tuna mahitaji yale yale. Kwa hivyo, na hili nasema serikali ikija itupe maelezo ya kina katika hili, tumeifikia wapi. Tumechoka kama Kamati na wajumbe na wananchi wa Zanzibar, kila siku kupewa ahadi ambayo hakuna linalokuwa katika hili. Hilo moja ambalo nilikuwa nawaomba pia wajumbe walitizame sana katika ukurasa wa 52 na 53 wa ripoti yetu.

Jengine Mhe. Spika, ambalo nimetaka nilitolee maelezo kwa sababu linanihusu pia kwa jimbo langu, hili ni dogo tu la kuelimishana. Nimesikia katika kikao hiki na vikao vilivyopita, panazungumzwa sana suala la Mji Mkongwe Mhe. Spika, na wajumbe baadhi yao pengine kwa kutokuelewa, wanasema kwamba tunakwamishwa na *UNESCO* hatusongi mbele.

Mhe. Spika, nasema kwamba eneo la Mji Mkongwe ndani ya Zanzibar ni eneo la, wanasema wenyewe *one square mile*. Sasa hivi kama tunataka kuendeleza nchi hii, hii ardhi yote iliyobakia haiendelezeki mpaka iwe Mji Mkongwe. Mji Mkongwe ni urithi wa kimataifa na dunia nzima watu wanaujua thamani yake, wanatunza historia zao.

Mhe. Spika, ukienda *The Hague* pale katika Mji Mkongwe ni kama ilivyokuweko hapa kwetu. Niliwahi kutembelea siku moja nikakuta nyumba imevunjwa yote nyuma lakini mbele ule ukuta umesimamishwa vile vile, kwamba sheria zao ile mandhari ya nje ibakie vile vile kama ilivyokuwa.

Lakini hata ukienda Uingereza Mhe. Spika, kuna Kanisa kongwe pale *Westminster* ambalo mpaka Malkia analitumia, wanataka kufanya marekebisho hawaruhuswi kwa sababu wameliingiza katika urithi wa kimataifa. Kwa hivyo, ni mambo ya kawaida hayo. Sasa kama unasema mji haukuwi na mara nyengine nasikitika mpaka Rais tunampotosha kwamba na yeze siku moja alizungumza kuwa tunazuiwa.

Mhe. Spika, mimi nasema kama tunataka maendeleo ardhi yote hii ya Zanzibar, maeneo mengine yote mbona hatuzuiwi, kama tunataka kuendeleza kweli tuna nia ya dhati, tuna mipango mbona hatuoni huko kwengine iwe kisa Mji Mkongwe tu.

Mhe. Spika, Mji Mkongwe wa Zanzibar ni urithi kwetu na vizazi vijavyo, uachiwe utunzwe na nampongeza sana ndugu yangu Issa ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka, najua anapambanana vikwazo vingi na changamoto nyingi. Lakini nadhani kama sio jitihada zake tusingebakia na hali ile ya Mji Mkongwe.

Kwa hivyo, nasema Mhe. Spika, kwamba nawaomba sana wajumbe wenzangu katika hili tuwe makini sana, tupanuwe kidogo uwezo wetu wa kufikiri na kufahamu mambo tunapochangia mambo, tusijikite tukadhani kwamba ati nchi yetu haikuwi kwa sababu Mji Mkongwe umezuiwa, huku kwengine katuzuwia nani, mbona hatuendezei Mhe. Spika. Hilo la pili.

La mwisho, Mhe. Spika, kwa sababu ya muda ulionigaia ni mdogo. Mhe. Spika, na hili vile vile niseme kidogo kuhusu Baraza hili, kwamba mara nyengine mnapotubana kwamba ripoti ya Kamati isizidi kurasa 20, kidogo kuna baadhi ya mambo yanakua yanaachwa hayaingizwi Mhe. Spika, na hasa kwa hali ya utendaji wetu ulivyo kuna mambo mengi muhimu.

Moja ambalo nataka kulizungumzia hapa ni suala la ardhi, lilizungumzwa sana katika ripoti yetu ya Kamati Mhe. Spika, wajumbe wengi walilizungumza.

Mhe. Spika, Katiba yetu kifungu cha 69(4)(a) imezungumzia miiko ya viongozi, inasema naomba ninukuu;

Kifungu cha Katiba namba 69(4)(a);

"Ni mwiko kwa kiongozi kutumia madaraka aliyopewa kwa ajili ya manufaa yake binafsi au kwa upendeleo au kwa namna yoyote ambayo ni kinyume na lengo lililokusudiwa madaraka hayo". Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Spika, nimekisoma kifungu hiki kwa sababu Kamati imefuatilia, Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, mara nyingi tumemuambia bado kuna malalamiko mengi sana ya wakubwa wazito serikalini wengine amba wanatumia nafasi zao kujikusanya ardhi wakati wananchi wa Zanzibar wenyewe wanapata tabu, hata ardhi ya kujengea mtu hana.

Kuna suala Mhe. Spika, bahati mbaya halikuingizwa katika ripoti ya Kamati, Mhe. Waziri anajua nililiacha katika kazi za Kamati zilizopita lifuatiliwe na wizara yao. Kuna mke wa mkubwa mmoja, kaweka shindikizo kwamba kuna eneo kubwa la ardhi eneo la Mangapwani apimiwe yeye na haya Mhe. Spika, yako kila pahala.

Mhe. Spika, tunafuatilia suala na katika bajeti tutakuja kukamatana hapa. Katika Jimbo langu la Mji Mkongwe kwenye kona ya barabara inayoitwa Dk. Salmin Amour *road*, ukitoka *roundabout* Michenzani kama unakuja zako Bwawani, kwenye kona ya kuelekea Malindi, kona ambayo kitaratibu hairuhusiwi kujengwa, kwa sababu ya usalama barabarani. Mhe. Spika, pamekwenda kuwekwa makontena pakajengwa kwa sababu kuna mkubwa katika ofisi hizo hizo kila siku zinazotajwa katika mambo kama hayo. Tositumie nafasi yetu vibaya kama Katiba yetu inavyotaka.

Mhe. Spika, niseme na katika hili nitamalizia nikae, kwamba suala la ardhi ni suala *very sensitive* duniani nchi nyingi sana jamii zilizoingia katika machafuko kwa sababu ya suala la ardhi, hapa Zanzibar tumefundishwa sana kwamba mojawapo ya sababu kubwa ya Mapinduzi ilikuwa ni suala la umiliki wa ardhi ulivyo. Mhe. Spika, tarehe 8 Machi, 1964, Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume alitangaza hapa, nanukuu katika gazeti la kweupe hili, linasema kwamba;

"Ardhi yote ni mali ya Serikali ya Jamhuri, ardhi yote iliyo khalia ni rasilimali ya Serikali ni marufuku kwa mtu ye yoyote kuingilia ardhi kama hiyo kwa kupanda kitu chochote kile bila ya amri na matengenezo na Serikali".

Lakini ikatolewa maelezo, kwa nini Serikali ikachukua hatua hii, naomba ninukuu;

"Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar imechukua hatua hii kwa sababu ya kuwasaidia maskini wote, tumechukua hatua hii kwa manufaa ya umma, watu wengi sana wa nchi hii hawana ardhi na ardhi yote imechukuliwa na watu kidogo tu, mabwanyenye wakubwa wakubwa. Kwa hivyo hatua hii ya kwanza ya kuichukua ardhi yote, itafuatwa na ardhi nyenginezo, ambazo zitamsaidia kila mnyonge na masikini yoyote yule aweze kuishi maisha bora." Mwisho wa kunukuu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Ali Mzee kwa kuliingiza hili katika ripoti ya Kamati Teule ya Ardhi wakati ule kwamba alilitambua. Sasa tunaposema tunayalinda Mapinduzi, tunaposema tunamuenzi Mzee Karume, mbona katika haya tunamkiuka Mzee Karume, kwamba viongozi wanatumia nafasi yao kinyume na ilivyopitishwa Katiba ya Zanzibar kuagiza tu, chukua eneo hili, chukua eneo hili.

Mhe. Spika, sasa namuomba Mhe. Waziri wa Ardhi, hili mwaka juzi na mwaka jana tukamkumbusha aliwahi kutwambia kwamba sheria zetu zinataka kwamba umiliki wa ardhi usizidi heka tatu, na kwa viongozi akatutajia kiwango fulani cha eka. Ingawa na mimi sijui kwa nini kuwe kuna tofauti kati ya mwananchi na kiongozi katika nchi ambayo inaamini watu wote ni sawa.

Mhe. Spika, hivyo kuwa kiongozi wewe una mamlaka ya kujichukulia ardhi unavyotaka wewe. Akatwambia atakuja kuwataja. Nimuombe Mhe. Waziri wa Ardhi katika hili ajiandae. Katika bajeti tukijaaliwa hapa, maana hapa leo hakuna vifungu, lakini katika bajeti hili tutalismamia kikamilifu. Huu mtindo wa wakubwa kutumia na fasi za kujilimbikizia maardhi, halafu huku wakahubiri wasiyoyatenda, hatuwezi kuendelea kukubali Mhe. Spika, katika haki za wananchi. Tutasimamia haki za wananchi wa Zanzibar, ndio jukumu tuliloletewa hapa.

Mhe. Spika, nakushukuru sana na nimtakie kila la heri Mhe. Waziri wa Ardhi na Mhe. Waziri wa Mawasiliano katika kazi yao, na kazi ya kuwasimamia tutaiendezea, kwa sababu ndio jukumu letu tuliloletewa hapa na wananchi wa Zanzibar. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nami nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tena uwezo na hatua ya kukutana hapa ili kuzungumzia mambo yanayohusu maslahi ya nchi yetu.

Aidha, nichukue fursa hii kuipongeza sana ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, iliyosheheni maelezo, yenye nia ya kujenga kwa maana ya kuleta mafanikio kwa wananchi wetu.

Aidha, niwapongeze sana mawaziri wote waliotangulia kutoa hoja mbali mbali katika kamati mbali na hasa Kamati hii iliyo mbele yetu kwa maelezo ya kina, kwa nia ya kujibu hoja na pia kupokea yale ambayo Baraza hili Tukufu yaliyopendekezwa.

Niwashukuru zaidi Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao mizuri ambayo naamini sote inatusaidia katika utekelezaji wa kazi zetu za kila siku. Wajitahidi sana katika kuendelea kusimamia hayo ambayo yanatakiwa yatekelezwe kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nina moja dogo sana ambalo nataka nilieleze linalohusu usitishaji wa mkataba wa *Philtex*. Uamuzi huu wa serikali haukuja moja kwa moja kuwa ultokana na serikali. Uamuzi huu ultokana na *Philtex* yenye kukiuka taratibu kwa mujibu wa mkataba, lakini pia kwa kukiuka zile taratibu za kimataifa zinazohusu masuala ya uendeshaji wa shughuli ile. Ndio maana shindikizo kubwa tukapata kwa sababu ya kuvunja taratibu hizo, na hasa kuititia kwa marafiki zetu wa Marekani pamoja na Jumuiya za Kimataifa kwa msingi wa kututaka tusikatishe mahusiano hayo.

Mhe. Spika, serikali baada ya kuchunguza na kuona makosa yale, ndipo ilipofikia uamuzi. Licha ya matatizo ambayo yamejitokeza ya kimataifa kwa kusajili meli za Iran kinyume na utaratibu, pia kuna kasoro nyingi ambazo *Philtex* walizifanya. Kwanza kuharibu jina la Zanzibar katika suala zima la usajili wa meli, lakini pia kukosesha mapato halisi kwa *ZMA* pamoja na kutoa *certificate za registration*, wakati mwengine *certificate* moja kwa meli zaidi ya moja, na nyengine kusema meli hii haifanyi kazi wakati inafanya kazi, na hususan hutoa taarifa wakati mwengine zisizokuwa za kweli, ambazo zilipelekea kwa njia moja au nyengine kuharibu sifa ya Zanzibar katika jambo hili.

Mhe. Spika, wale wanaotutishia kwamba *Philtex* wana uwezo wa kwenda Mahakamani kuishtaki serikali waache kututisha, hawana uwezo huo. Kwa sababu tukizonesha kasoro hasa za *Philtex* inawezekana licha ya kututisha sisi, watalipa fidia ni wao ndio ambao wanapaswa kuilipa fidia serikali. Kwa hivyo hatua zitakazofuata baadaye ambazo kwa kiasi kikubwa tunasaidia na wenzetu hawa tulioiwapa watusaidie katika utaratibu wa kusajili meli.

Tatizo la msingi Mhe. Spika, ni kwamba *ZMA* sasa inataka yenye iwe ndio inafanya masuala ya ku- *register* meli huko Dubai na pahala pengine. Mtihani tulionao upo hapa ndio tatizo liliopo, kwa mujibu wa sheria ya *UAE*, ukitaka kufanya shughuli hiyo ni lazima tupate leseni inayoruhusu kufanya kazi hiyo. Ili upate leseni hiyo unahitaji kutimiza vigezo vinavyotakiwa, hasa hasa ya kuwa na *qualified surveyors* ili uweze kupata hiyo. Sasa tatizo letu kwenye *ZMA* hatujakuwa na hao wataalamu wenye kiwango hicho kinachotakiwa ili tuweze kupata leseni na kazi ya *registration* iweze kuwa.

Ndio maana tulidhani tungetumia wenzetu watusaidie katika kufanya shughuli hiyo, lakini katika msaada wowote utakavyokuwa lazima suala la *registration* lazima lipate uamuzi wa kisera kutoka serikalini.

Tumewambia *ZMA* wao wafanye shughuli za usajili wa meli pale. Na kutokana na zile taratibu za kisheria na kitaalamu hawatoweza moja kwa moja wao kufanya shughuli hii.

Kwa hiyo, inabidi *ZMA* kuititia Wizara husika sasa itushauri namna gani ya kufanya, ili utaratibu wa kusajili meli uwezekane kwa utaratibu huo ambao serikali ilitaka, lakini kwa sasa kinachotokea wale walipewa jukumu kutusaidia wanapotusaicia katika suala lile la kitaalamu la kwenda kufanya *survey*, *waka-survey* meli baadaye wakatoa ripoti yao, tatizo linapokuja sasa kwamba *ZMA* ndio watoe zile *certificates* au wenyewe wanaziita *sign calls* na kusainiwa na *ZMA*.

Hapo nao wana swaliliza Je, ikitokea *ZMA* wakatoa *certificate* kinyume na haya matakwa ambayo unatakiwa uylatekeleze mwenye kubeba mzibo wa dhamana itakuwa ni ile kampuni ambayo inatakiwa ikafanye tathmini mpaka kuhakikisha kwamba meli hiyo iwe na haki ya kupewa *certificate*. Sasa na wao hawa wanataka kwenye *certificate* wawe wanasaini na lazima saini iwe moja. Kwa sababu wanasema ikiwa kuna mtu mwengine ana uwezo wa kusaini, litakapokuja kutokea tatizo wao watakuwa dhamana wa serikali ya *UAE* na wake wenye meli hapo mtihani ndio unapoanza.

Kwa hivyo, *technical* lipo tatizo, na linapaswa kutafutiwa ufumbuzi. Huenda suala si kuongezewa fedha *ZMA* kwa ajili ya kufidiwa kuendesha shughuli zao, suala ni *ZMA* kuja na mpango utakaotuelekeza namna gani ya kuondoa tatizo ili waweze kufanya *registration*. Kampuni ambayo inafanya kazi kwa niaba ya Al-Khaleej kama alivyosema ndugu yangu Ismail Jussa ni *ALCO SHIPPING COMPANY* ambayo ye ye ndiye mwenye mkataba na Al-Khaleej na ye ye analipwa na Al-Khaleej kufanya hizi kazi.

Mhe. Spika, Kampuni hii ndiyo yenyе Chelezo, yenyе wataalamu, yenyе kujua namna ya kufanya shughuli zote. Sasa kutekeleza hapa ni lazima tupate muelekeo kutokana na *ZMA* ni namna gani tutaondoa tatizo ili sasa *registration* zifanyike na mapato yapatikane kwa wingi sana. Wao wanacho sema watu wa *ALCO* kwamba bado *Philtex* wanawenza kwa chini chini wakatoa *certificate* hizo, kwa sababu haja-*submit* kila kitu kwa serikali. Sasa wanachotaka wao wana uwezo kamili wa kutusaidia kupambana na *Philtex* katika kila kosa ambalo litawenza kujitokeza.

Mhe. Spika, sasa hivi mtihani wetu mkubwa kwanza tuachane na kuogopa kutishwa kwa mbinu za *Philtex* kutaka kuzunguka kwa mlango ya nyuma. Maana kuna mbinu hapa *Philtex* kwa kutumia watu wengine wanaowataka wao waendelee kufanya hii kazi. Wanajisifu kwamba wameahidiwa kuwa watarudishiwa uwakala.

Mhe. Spika, sisi tunasema wazi kuwa *Philtex* hawezi kurudishiwa uwakala na yeyote yule anayehusiana na *Philtex* hatopewa uwakala. *ZMA* wana mamlaka kamili ya kuamua mtu yeyote wanayemtaka mwenye kutimiza vigezo kumpa uwakala, ili shughuli ifanyike. Kusiwe na visingizio kwa Ofisi ya Makamu wa Pili ama pengine kwa sababu wao wana mamlaka kamili kufuta mkataba wa Kampuni yoyote hata hiyo ya Al-Khaleej wanao uwezo huo wakaufuta wakati wowote na kuingia mkataba na kampuni wanayoitaka.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tunakusudia kazi hii tuimalize si muda mkubwa kutoka hivi sasa. Kwa hiyo wale Waheshimiwa waliokuwepo nje niwaombe warudi, na vile vile wale waliokwenda nje kwa dharura wakumbuke kurudi muda mchache baada ya dharura zao, endelea.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais haina mamlaka kuwalazimisha *ZMA* waingie mkataba na Kampuni yake. Pale *ZMA* watakapoona kwamba hapa tunataka tushirikiane na nani ili suala hili likamilike, ndio liweze kukamilika. Kinachotokea sasa hivi kwa sababu hawa *ALCO* kampuni wanawajua *Philtex* utandu na ukoko, na makosa yao, na wako tayari kuyaeleza, ndio woga wa *Philtex* juu ya kampuni hii.

Mhe. Spika, cha msingi cha kufanya ni kwamba *ZMA* wayapitie kwa kina mambo haya, washauri na hakuna sababu ya serikali kutenga fedha maalum ya kuwasaidia *ZMA*, kwa sababu *registration* yenyewe inaweza kuingiza pato kubwa sana. Ni suala la kiufundi na la kisheria, linalopaswa kufanyika ili utaratibu uendelee kwa kubadili sera yetu ya maamuzi kuhusiana kwamba *ZMA* yenyewe ndiyo ifanyike *registration*.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, ingawaje sina mchango mkubwa isipokuwa tu nikushukuru na pia niwashukuru Wajumbe wote ambao

wamechangia kupitia wizara yangu. Niseme kwamba wale wote waliochangia nawashukuru kwamba wamechangia kwa lengo zuri kwa kutupa miongozo, kutuelekeza pamoja na kutukosoa.

Katika hayo waliochangia nakubaliana nayo mengi, niseme kwamba yapo ambayo yamefanyika kama yalivyzungumzwa, na yapo baadhi yao yanahitaji kutolewa ufanuzi. Nafikiri zaidi atayatolea ufanuzi Mhe. Waziri atakapokuja yeze ataelezea kwa ukamilifu zaidi.

Mhe. Spika, baada ya hayo niseme nashukuru na niseme kwamba tumesikia, tumejifunza na tutaendelea kujifunza zaidi. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nashukuru kwanza na mimi kunijaalia kuwa mzima wa afya kufika tena katika Baraza hili Tukufu. Pia nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi nisimame tena sio kwa kujibu hoja, bali kwa kutoa ufanuzi wa hapa na pale katika kazi yetu hii muhimu tunayoifanya kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wetu.

Mhe. Spika, nashukuru kwamba ripoti hii ya Kamati ya Miundombinu na Mawasiliano, imejadiliwa mpaka sasa hivi na watu kumi na moja. Imewasilishwa na Mhe. Marina Joel Thomas kwa niaba ya Mwenyekiti na ikajadiliwa na Wajumbe wafuatao:

- 1.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
- 2.Mhe. Hamza Hassan Juma
- 3.Mhe. Abdi Mosi Kombo
- 4.Mhe. Hija Hassan Hija
- 5.Mhe. Salum Abdalla Hamad
- 6.Mhe. Hamad Masoud Hamad
- 7.Mhe. Farida Amour
- 8.Mhe. Ismail Jussa Ladhu
- 9.Mhe. Mohamed Aboud Mohamed; na
- 10.Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Spika, wote hawa wamezungumza mambo ya maana sana, ambayo nina hakika tukiyafanya kazi yatatusaidia sana katika kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi wetu. Nianze na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Kwa upande wangu mimi upande wa ardhi amezungumzia juu ya suala la nyumba moja ambayo iko Makongeni, na akasema kwamba nyumba hii ameuziwa mtu mmoja Bi Miza, na barua anayo pale ameioneshaa.

Ni kweli nyumba hii ilikuwa katika hali mbaya upande mmoja, lakini upande mmoja ulikuwa ukikaliwa na aliyejikuwa askari wa KMKM, na Bi Miza aliomba kuuziwa nyumba hii na alikubaliwa kuuziwa. Kilichotokea ni kwamba bado tu hajakabidhiwa, lakini huyo askari wa KMKM amerudi tena kwa sababu alihama kipindi fulani, amerudi tena na kuamua kwamba aendelee kukaa yeze. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Mshimba kwa suala hili anipe nafasi nilifuatilie zaidi ili baadae nichukue uamuzi wa kulitekeleza.

Amezungumzia vile vile juu ya upungufu wa mita kwa upande wa ZECO. Mhe. Spika, ni kweli kwa sababu watu wengi siku hizi wamepata muamko wa kutosha juu ya kuunga umeme katika majumba yao. Ni kweli maombi mengi sana ya watu kuunga umeme yapo, na mita kila zikiletwa hazichukui muda mrefu zinamalizika. Kwa hivyo ni kweli lipo tatizo hilo, lakini nyengine wameshaagiza, kwa hivyo, kazi ya kusambaza umeme itakuwa inaendelea siku hadi siku.

Amezungumzia juu ya suala la mgogoro wa ardhi kwa hati iliyotolewa mwaka 1998 ambayo sehemu hiyo sasa hivi amepewa mtu mwengine. Mhe. Spika, kujibu tu haileti maana kufanya kazi, ndio maana kwa hivyo madam ameniletea suala hili hapa na mimi sikuwa nalo, nadhani ni vizuri vile vile anipe nafasi nikalifanyie kazi na uamuzi niutoe.

Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa upande wangu ninamshukuru sana, ametilia mkazo suala la hifadhi ya Mji Mkongwe. Na Mhe. Jussa amezidi kutoa taaluma juu ya suala hilo la kwamba lazima tukubali kwamba tuhifadhi Mji Mkongwe na tuisitake wote kwamba uharibiwe.

Mhe. Jussa amesema vizuri kwamba ardhi bado iko sehemu nyengine, ni vizuri waombe sehemu nyengine kujenga majumba ya maghorofa wanayoyataka ikiwa ghorofa 15, 20, 40 kadri ya mtu ya uwezo wake, asipate tabu kwamba lazima nyumba hiyo aisimamishe Mji Mkongwe.

Jana Mhe. Mohamed Aboud amejibu vizuri sana juu ya suala la kuhifadhi Mji Mkongwe, na sheria ya *UNESCO* ni sheria yetu ambayo inafanyiwa kazi na *UNESCO*. Kama tutaifanyia marekebisho ili Mji Mkongwe uendelee kuwepo na baadhi ya mambo tunayotaka tuyafanye vile vile kwa faida ya wananchi wa nchi hii.

Mhe. Abdi Mosi ameulizia ni nani hasa mwenye jukumu la kusimamia ujenzi katika nchi hii. Bila ya shaka ni Wizara ya Ardhi ndiyo inayogawa ardhi, na ndio inayotoa viwanja, ila kuna usugu wa aina yake, na kwamba amewataja watu amba kwa mujibu wa sheria hawana uwezo wa kugawa viwanja, lakini wanaauza viwanja, hili ni kosa na linapofanyika ni vizuri viongozi wasaidie kutoa taarifa kuliko kukaa nalo tu hivi hivi, kwa kuja kulizungumza hapa halisaidii, ni vizuri wasaidie kutoa taarifa.

Lakini ni kweli vile vile na wananchi wao wanataka kunyakua haya madaraka kinyume na sheria. Wizara yangu ina jukumu la kuwaelimisha wananchi juu ya suala hili, na ndio maana nimefanya mikutano na mashehe hawa Wakuu wa Wilaya na Madiwani, kuwaelimisha juu ya suala hili kwamba wao hawana madaraka ya kugawa viwanja. Ardhi yote ni mali ya Serikali kama ilivyotangazwa tarehe 8 Machi, 1964. Kwa hivyo, Wizara hii ndio yenye jukumu la kusimamia masuala hayo. Isipokuwa ninasikitika tu kwamba hata tunapokuwa tunataka kufanya kazi hiyo ya kutengeneza ardhi kwa mpango mzuri, vile vile kuna baadhi ya wananchi wanatukatalia na inakuwa ghasia nyingi kidogo, mfano mzuri ni huko Matemwe.

Matemwe tulitengeneza *layout* nzuri kabisa ya kutaka kupima viwanja, na ninasikitika kusema hata baadhi ya Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi waliwahi kupewa ankara za viwanja hivyo ambavyo kabla havijapimwa. Bahati mbaya Matemwe wakakataa kabisa kusipimwe, na kukawa kuna ugomvi mkubwa kabisa kule Matemwe kwamba kusipimwe na ardhi ile ipo mpaka leo.

Na tunajua kwamba itafika mahala tutakubaliana kwenda kuianga, kwa sababu tukiipanga ile ardhi watakaojenga ni watu wa Matemwe pamoja na wale watakaotaka, maana yake hii nchi yote ni yetu, kila mahala unaweza ukapata kiwanja hapa, ukapata na hapa ukabadilisha mazingira. Kwa hivyo, tutafanya suala hilo.

Nakubali kwamba nchi za wenzetu zimepangwa na njia zinaonekana vizuri, ni kweli sisi tunakuwa wakaidi, maana yake hata ukienda katika maeneo ambayo yalipimwa vizuri na kupangwa vizuri, kuna mfano Kwahani kulpimwa vizuri, lakini jinsi binadamu alivyokuwa hatosheki na eneo analopewa basi siku ya tatu utakuta kashusha kipenu, kashusha sijui kilango gani, kajenga sijui kitu gani, ilimradi ile njia ilikuwa inapita gari sasa hivi haiwezi kupita gari tena kutokana na uharibifu tunaofanya sisi katika maeneo ambayo yamepimwa.

Na hata ukienda katika maeneo kama Mombasa ambako kumepimwa vizuri kabisa, vile vile utakuta watu wanatanua, mara anavuta kiambaza kile hakimtoshi, anavuta kidogo anatanua vyumba kwa kuongeza eneo lile. Hili ni tatizo ambalo tunalo na Wizara yangu inalifanyia kazi. Lakini tunawaambia tu kwamba kwa upande huu sisi tumeshatarisha *master plan* sasa hivi nzuri tu, na tutaileta kwa Waheshimiwa Wajumbe hawa na wataionna na wao ndio watatakiwa kuifanya kazi ili tuone kwamba *master plan* ile inatekelezwa.

Kuna suala la Mahkama ya Ardhi ambayo Mheshimiwa ameuliza hapa kwamba inakuwaje Mahkama ya Ardhi inatoa hukumu halafu baadae inarudi nyuma inabadilisha ile hukumu. Mimi si mwanasheria, lakini wanasheria wenyewe wanajua, kwamba kwa mujibu wa sheria Mahkama inaweza kutoa hukumu na ikabadilisha ikiwa kesi hiyo imesikilizwa na kutolewa hukumu kwa upande mmoja.

Ikiwa upande wa pili ikileta ombi la kutenguliwa hukumu hiyo ili kesi isikilizwe upya pande zote mbili; ya *interparty*, hivyo katika mazingira hayo Mahkama inaweza kubatilisha hukumu ile, haya ni maelezo ya kisheria na wanasheria wanayatumia maelezo haya katika masuala ya kisheria. Huu ni utaratibu wa kisheria na kutoa hati kwa pande zote, hilo ni moja.

Na wakati mwengine Mahkama wenyewe inaweza ikasikiliza kesi lakini igandua mahala imekosea, ikigundua imekosea inao uwezo wa kuirudisha tena kesi ile na kuisikiliza upya, huo pia ni utaratibu wa kisheria amba umeruhusiwa na wanasheria. Wanasheria wana lugha zao na wana mambo yao wenyewe wanafanya kwa masuala haya.

Vile vile, kuna suala la kukata rufaa ikiwa upande wa pili hakuridhika anaweza kukata rufaa kwa kesi ile na kesi ile ikasikilizwa tena vile vile kwa kesi inaweza ikarejewa tena. Kwa hivyo, haya ni masuala ya kisheria ambayo tuyastahmilie, lakini tuijanda vizuri katika masuala ya sheria.

Mhe. Hija, amesema Serikali itafute uamuzi wa kuiwezesha *ZAWA* kutoa huduma, yaani wapatiwe ruzuku kutoka Serikalini. Mhe. Spika, suala hili Serikali imeshalizungumza vizuri sana, na imeshafanya maamuzi katika baadhi ya mambo. Kwanza deni lote ambalo *ZAWA* wanadaiwa limeshatolewa uamuzi kwamba sasa hivi lilipwe na Wizara ya Fedha, kwa hivyo hilo suala limechukuliwa hatua. Na vile vile mita za *TUKUZA* katika visima vya maji, uamuzi umeshatolewa kwamba zote zimeondoshwa na zimeshaondoshwa tayari hivi sasa.

Kwa hivyo, hakuna tena tatizo la mita ya *TUKUZA* katika visima vya maji. Na hii ilitokana na Waheshimiwa Wajumbe wa kamati walizungumza suala hili walipokuja kuona wizara yangu, nikaona ni vizuri tulifanyie kazi, tukalifanyia kazi, kwa bahati Serikali ikalikubali, kwa hivyo mita zote za *TUKUZA* zimeshaondoshwa haziko tena kwenye maeneo yale.

Mhe. Salim Abdalla Hamad, amezungumza juu ya suala la *ZECO* kuongeza vituo vya kuuzia umeme Pemba, na kwa bahati muda wenyewe ni mfupi sikuweza kupata orodha hasa kutoka maofisa wangu juu ya vituo ambavyo walivyoviongeza kule Pemba, lakini hata hivyo nafikiri tumefanya uamuzi wa makusudi kabisa wa kujiunga na masuala ya kununua umeme kwa kutumia simu, watu wanafaidika sana. Na siku hizi katika vituo vya umeme hasa hapa Unguja hukuti foleni kubwa sana, kwa sababu mtu ananunua umeme kupitia katika simu yake mwenyewe ya mkononi aliyonayo. Kwa hivyo, ni utaratibu ambao tumeuanzisha.

Suala la Wizara ya Fedha ilipe deni la *ZAWA* hilo nimeshalizungumza, kuna suala moja limezungumzwa na Mhe. Salim Abdalla Hamad hili suala la mafuta. Mhe. Spika, masuala haya hasa ni masuala ya kisheria, nimepata maelezo kidogo kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na ndio nataka niyasome hapa kidogo kwa sababu kifungu cha 26 kimezungumzia maliasili zote za Taifa ikiwa ni pamoja na madini, gesi, na mafuta ni mali ya umma, na Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hapa limetumika neno au. Ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaweka utaratibu wa kuhakikisha zinatumika kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Ni kwamba suala la mafuta kwa kifungu hiki limeondoka kabisa katika mambo ya muungano, na ndio maana katika mambo yaliyotajwa katika nyongeza ya kwanza mwisho wa hii Rasimu ya Katiba itakapopitishwa lakini sio sasa hivi, sasa hivi tuna Katiba ile ile ya zamani ambayo bado ingali ya Muungano, lakini nyongeza ya kwanza imetaja mambo 16; suala la mafuta na gesi halimo, kwa sababu limeondoka kabisa katika masuala ya muungano. (*Makofi*)

Ufanuzi nilioupata ni kwamba, kwa sababu umetolewa uwezo wa pande mbili kusimamia utaratibu wa kushughulikia masuala haya kwa faida ya kila upande. Ina maana kwamba sasa hivi sisi tutachimba mafuta Zanzibar kwa faida ya Wazanzibari, na sio kuingia katika masuala ya muungano, na kule wanaendelea kuchimba mafuta kwa faida ya iliyokuwa Tanganyika na sio kwamba ni suala la muungano.

Huu ndio utaratibu ambao nimeelekezwa ambao unatumika hivi sasa. Kwa hivyo, sasa hivi hakuna tena tatizo la kwamba mafuta ni mali ya Jamhuri Muungano, mafuta ya Zanzibar ni ya Zanzibar na mafuta ya Tanganyika ni ya Tanganyika, huo ndio ukweli katika Katiba hii mpya ambayo ikipita Katiba hii hivyo ndivyo itakavyokuwa.

Na nitawakumbusha tu kwamba suala hili tulipitisha hapa katika Baraza la Wawakilishi, kuyaondoa mafuta katika orodha ya mambo ya muungano, likawa halikutekelezwa tukaenda kwenye mchakato wa Katiba na mchakato wa Katiba ukalikubali kwamba liondoke na limeondoka hivi sasa hivi, kwa hivyo, kila nchi itashughulikia kwa upande wake. (*Makofi*)

Suala la nyumba ya Kengeja, Mhe. Spika, Serikali inataka kuyaenzi fikra na mawazo aliyetuanzisha mzee wetu Mhe. Abeid Amani Karume Rais wa Kwanza wa Zanzibar na ninasema tukirudi katika fikra yake basi tutajenga kwa urahisi sana na itakuwa ni Zanzibar nzuri sana.

Nasema Mhe. Karume alifanya mambo haya, nilisema juzi hapa nazungumza habari ya Kamisheni ya Ardhi katika Mipango Miji ni kwamba, Mzee Karume alianzisha mpango wa mji mzuri sana badala ya kwenda hivi kutanuka kaanzisha mpango wa kwenda juu na kaanzisha maeneo mbali mbali ili tusiwe na mji mmoja tu Unguja na Pemba, ndio maana akajenga mjini, akajenga Kusini, akajenga Kaskazini, mote kaanzisha majenzi humo. Na Pemba vile vile akajenga Kusini, akajenga na Kaskazini na kwa bahati Pemba kajenga Kusini kajenga

sehemu 3; Kajenga Mkoani, kajenga nyumba hii ya Kengeja, kajenga na Chake Chake. Na Kaskazini kajenga Wete, kajenga na Micheweni.

Huu ni mpango peke yake wa nyumba tukiufuata huu kwa kweli ardhi tutakuwa nayo ya kutosha sana, na ndio maana tumeanzisha *master plan* ambayo itaamua wapi pajengwe nyumba za ghorofa tano, wapi pajengwe nyumba za chini, wapi pajengwe nyumba za ghorofa tatu na wapi mtu apewe kwa kujenga nyumba za ghorofa 40 mpaka 50 kama uwezo anao. Tunayo *master plan*, na tutaitela na itapatikana.

Kwa hivyo, tumekuwa tukihangaika sana kutafuta hizi milioni mia mbili (200,000,000) na nategemea kwamba Wizara ya Fedha sasa hivi tayari kutupa hizi milioni mia mbili (200,000,000) ili tulitengeneze jumba lile, tunataka tumuenzi Mzee Karume lazima tutengeneze. Nia ya Serikali kwamba jumba lile tulitengeneze, na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akipenda tutalitengeneza.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ametilia mkazo sana juu ya suala la Mji Mkongwe, mimi ninamshukuru sana na naomba Waheshimiwa wachukue ufahamu huo, na amezungumza juu ya suala la ardhi kwamba ni madaraka yetu na amezungumza juu ya ardhi ya eka 5 kwa viongozi na eka 3 kwa mwananchi.

Ila nataka kumfahamisha ile haikuwa ni sheria, ilikuwa ni utaratibu, lakini utaratibu huu mimi naona sasa hivi tumeshauondoa, hata kiongozi yeoyote tukienda kumpa eka sasa hivi tunampa eka tatu, hatumpi tena tano au tisa kama zilivyokuwa zikitumika wakati ule, lakini lililokwisha kufanyika ndio lishafanyika tutakuwa sisi hatuna la kufanya. Kwa sababu waliokwisha fanyiwa wameshaondoka, wengi duniani hawapo tena hivi sasa, hivi katika masuala hayo. Lakini wengi wanaokuja sasa hivi tunawapa hizo hizo eka 3 tu hatuwapi zaidi ya hiyo inapokuwepo, maana eka zenyewe nazo hazipo nyingi kabisa, zimeshajengwa, na ziliopo ni chache sana na zina watu zote, labda itokee eka tuigundue mahala iko tupu imefichwa huko na Sheha au nani, hiyo tunaigawa tunampa mtu mwengine.

Mhe. Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, na ninashukuru kwamba kwa kweli kumbe mimi nimugundua ukifuata maelekezo ya Wajumbe wa kamati hawa wakikupa basi uongozi wa wizara yako unakuwa rahisi sana, na kwa kweli yananisaidia sana maelekezo yao, na ndio maana mambo mengi yanapungua katika maoni na maagizo ya kamati hizi wakati tunapoyafanya kazi vizuri sana, ninawashukuru sana.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofit*)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, na mimi kwa mara nyengine tena nikushukuru na kuwashukuru Wajumbe wote waliochangia masuala ya kamati. Ninawashukuru vile vile kwamba wamekuwa wawazi kutushauri, kutuelekeza na baadhi ya mambo machache kutupongeza kwa mule ambapo tunajitahidi kufanya vizuri.

Mhe. Spika, yaliyozungumzwa ni mengi, na kama alivyosema Mhe. Waziri mwenzangu sitaweza kujibu hoja zote isipokuwa kuna mambo mengine makubwa ya msingi ambayo mengine yanahitaji maelezo pengine ni ushauri na mengine tutakwenda kuyafanya kazi.

Sasa katika haja hiyo nisingependa kumtaja kila mtu kwa yale yote aliyochangia kwa sababu mengi yao Mhe. Spika, yamejirudia. Kwa hivyo, nitakapojobu hoja nitakuwa ninajibu hoja za wote wale. Kama vile alivyosema mwenzangu waliochangia hoja hii ni watu 11 ambao na mimi kwa heshima ya kuwatambua ni vizuri nikawataja.

1. Mhe. Marina Joel Thomas
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Hamza Hassan Juma
4. Mhe. Abdi Mosi Kombo
5. Mhe. Hija Hassan Hija Sijui Hija na Hamza ni ndugu
6. Mhe. Salim Abdalla Hamad
7. Mhe. Hamad Masoud Hamad
8. Mhe. Farida Amour Mohammed
9. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
10. Mhe. Mohamed Aboud Mohamed; na
11. Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi ambaye alikuwa anajaribu kusaidia mchango kwa Wizara yake.

Mhe. Spika, ulimwita Naibu wangu bahati mbaya hayupo, lakini asubuhi alinambia kwamba ana dharura na dharura nyengine huwezi ukazikataza, kwa hivyo ninamuombea radhi kwa hilo.

Mhe. Spika, kuna mambo makubwa kama manne matano ambayo nitayaeleza badala ya kueleza suala moja moja.

La kwanza ambalo mimi ningependa nilianze ingawa sikuliweka namba moja, ni suala la vituo vya daladala na kituo cha Darajani.

Mhe. Hamza amesema kwamba hajaona duniani nchi iliyokuwa haina kituo cha magari. Uamuzi ulishafanyika na ulifanyika na Serikali kwamba kituo cha Darajani kiondoke na sababu za kuondoka zilikuwa za msingi

Tulipokuwa tunajadili wizarani kwangu na wenzangu walisema ule Mji Mkongwe wenyewe ushacheuka, sijui Mhe. Spika nadhani anajua. Ushacheuka kwamba ni mdogo kuliko wale watu wanaoingia pale Mjini na barabara zetu mbili au tatu. Sasa hali ilivyokuwa kwa kituo cha Darajani ilikuwa lazima yafanyike mabadiliko.

Sasa mabadiliko yamefanyika lakini mimi yamezaa matatizo, lazima tukubali utekelezaji wake haukwenda kama vile ilivyotegemewa. Na sababu si kwamba tu maamuzi yalikuwa sio, lakini na moja katika sababu kubwa na wanansikia ni kwamba wengi sasa vijana wadogo hawataki kufuata sheria.

Suala la daladala ni MTAMBUKA, suala la kufuata vituo linahusu idara nyangi. Inahusu wizara yetu ya Idara ya Nchi Kavu, inahusu Baraza la Mji, inahusu Polisi, inahusu Mahakama, inahusu kutoa leseni. Sasa ukweli uliopo ni kwamba pale zinapotakiwa taratibu zifuatwe, ukimgundua mtu mwengine unamkuta hata ule umri wa kupewa leseni hajafika anaendesha gari, madaladala wanashindana kila mtu anataka apate abiria, akiambiwa asimame mahala fulani kwa dakika fulani amchukue abiria imekuwa sasa wanatuama. Lile zogo la pale CCM ni kutokana na kwamba pale palikuwa watu wanatakiwa wapite wasisimame, badala yake pamegeuzwa ndio kituo. Ni batati mbaya na kwa kweli si jambo zuri. Mhe. Spika, sasa tufanye nini?

Kwanza, nilipokutana na mwenzangu Waziri wa Tawala za Mikoa ikagundulikana kwamba yeche kumbe si kazi yake, Sheria ya Usafiri wa Nchi Kavu shughuli ile ni shughuli ya Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu.

Tukakutana sote, tukakutana mimi na waziri kikao kimoja, mimi na Mkuu wa Mkoa alikuwepo Mkuu wa Wilaya ya Mjini, alikuwepo Mkuu wa Polisi wa *Traffic*, mtu niliyeshindwa kumpata siku ile alikuwa mtu wa Mahakama ambaye naye alikuwa na sehemu yake ya vurugu, maana akipelekewa kijana kule badala ya kumpiga faini kwa mujibu wa sheria anampiga shilingi kumi na tano elfu (15,000), kijana siku ya pili yuko barabarani anadharau kama ilivyokuwa mwanzo. Kwa hivyo, ikabidi sote kwa pamoja tukutane tuulizane tufanye nini katika kulirekebisha hili.

Mhe. Spika, tukapeana kazi, kazi hiyo tukaikamilisha niliachiwa mimi na wizara yangu. Kabla hatujamaliza kazi hiyo ya kutaka kufanya marekebisho Kamati ya Miundombinu ikaja kututembelea ikakutana na sisi tukajadiliana ikaonekana kwamba suala hili haliwezi kupata ufumbuzi isipokuwa sote tukutane pamoja halafu kufanywe semina. Madereva wawepo; kuna wale wengine wanaitwa mabaguani sijui utingo, Mkuu wa Polisi awepo, mtu wa Mahakama awepo, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wawepo. Na hivi ninavyosema Mwenyekiti wa Kamati hii ananisikia, ilikuwa tarehe 28 semina hiyo ifanyike, lijadiliwe suala hili kwa undani na maoni ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wale wadau, halafu tupeleke serikalini kwa marekebisho ya hali iliyoko sasa.

Mhe. Spika, hali iliyoko sasa hairidhishi wala haitupi faraja sote, na Wajumbe mna haki ya kulilaumu katika hali ya sasa, lakini ufumbuzi ulikuwa tuupate kuhusu suala hilo, na kama kila kitu kitakwenda sawa basi tarehe 28 mtapata nafasi kutoa maoni yenu, tutamwita mtu wa Polisi aeleze matatizo anayoyapata, tutamwita mtu wa Baraza la Mji aeleze matatizo anayoyapata, tutamwita Mkurugenzi wetu wa Usafiri wa Nchi Kavu anavyopata tabu kuhusu leseni, tutawaita watu wa ZRB wanaotoa vile vidudu vile, atakuwepo mtu wa Mahakama, na kila mmoja atatoa waraka au taarifa zake halafu kwa pamoja tujadili tupate maelekezo.

Mhe. Spika, sasa ushauri wa mwanzo ulikuwa vipi? Kwamba hali iliyoko sasa hairuhusu tuibadilishe, na watu hasa wanaopata tabu hivi sasa ukiacha wale hali ya mzogo, watu wanaopata tabu ni wale wanaotoka pwani baada ya kushuka meli au wanaokwenda pwani wanapotaka kusafiri, hao kwa sasa ni moja katika watu wanaopata tabu.

Maana mtu anatoka kwenye meli pwani anataka aje Darajani ndio alivyozoea, lakini si sasa, inabidi aje CCM au aje hapa Baraza la Wawakilishi ni tabu kweli, ni zogo hasa. Tukadurusu zile njia wanazopita hii ya Mwanakwerekwe, hii ya Kiembesamaki hii wapi tulijitahidi kufanya kazi ambayo ilikuwa ikamilike, Mungu ajaalie tukutane totalifikisha kwetu na nyinyi mtatoa maoni.

Mhe. Spika, lakini la pili suala la msingi ni kwamba suala hili ni la muda, hayo marekebisho tutakayofanya, suala la kudumu ni kwamba inategemea na Mhe. Waziri hapa anahuksika Mipango Miji (*master plan*) ya mji wenye. *Master plan* ya mji wenye imeshafikishwa serikalini na uamuzi umeshatoka marekebisho ya mji uwe vipi, na barabara kuu ziweje, na magari yanayotoka kuingia mjini yapite wapi na yakae wapi. Sidhani kwamba nina madaraka hayo ya kueleza hivi sasa, kwa sababu si suala la wizara yangu, lakini huo mpango miji umeshakwisha na suala hili la kudumu nalo litapata ufumbuzi hapo wakati utakapofika kufanyiwa utekelezaji suala hili.

Mhe. Spika, lakini kwa sasa marekebisho yatafanywa, na Mungu akijaalia vurugu hili litaondoka kwa kiasi fulani, isipokuwa tu polisi watapokuwa wanafanya kazi zao itabidi sasa wawe *strict* sana katika kuona kwamba anayekamatwa na anayepelekwa Mahakamani sheria inafuatwa. Nina mmoja mmoja nasikia ukiwa umeongeza watu kwenye daladala mtu mmoja unalipa dola 15, mtu anakwenda kulipishwa elfu tano (5,000). Sasa yule dereva siku anayomkuta yule askari anamwambia silipwi bwana si unaniona bado mambo ye ye anaiga, imetuwa kama ni suala la dhara. Kwa hivyo, hilo Waheshimiwa naomba tustahamiliane, na mimi nalijua linaathiri mji mzima, na kwa kweli halipendezi, hata watu barabara zile njia za pembedi pia watu wanazigeza *parks*. Hakuna utaratibu kunahitaji marekebisho makubwa.

Mhe. Spika, tulikuwa tumeshauri *route* ziwe na rangi ikiwa ni gari ya Kiembesamaki ijulikane kwa rangi sasa si namba tu. Wale madereva wavae sare maalum kila kitu kilikuwa tayari isipokuwa Mungu ajaalie semina hiyo isimame. Naliunganisha hilo, na suala la taa ambalo nalo vile vile alisema Mhe. Hamza taa pale panaitwa Kwa Khamis Machungwa na huku Mpenda huku *junction* hii.

Mhe. Spika, mpaka sasa mradi ule hatujakabidhiwa sisi kama wizara au idara uko chini ya mkataba kwa majoribio, na moja katika suala tulomkosoa huyo anayeweka taa zile ni hilo, suala la taa za kwa Mzee Khamis Machungwa, kwamba inakwambia sasa pita lakini uende CCM badala ya kwenda Darajani. Lote limeonekana na tumemwita na tumemuandikia na bado atafanya marekebisho.

Mhe. Spika, uzuri wa taa zile hazitumii umeme zinatumia mwanga wa jua, ilikuwa kazi afanye na hapa Malindi na huku kiko majoribio nacho hakijaa vizuri cha huku, lakini suala hili bado liko kwenye mkataba. Nadhani niliache hapo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nilitaka nilizungumze kwa ujumla ambalo limezungumzwa na watu wengi, suala la mkataba wa *Philtex*.

Mhe. Mohamed Aboud ye ye ameeleza kwa kiasi fulani, lakini mimi nilikuwa sijui kwamba Mhe. Spika utanistahamilia niliambiwa hasara gani serikali ilikuwa inapata, kwa sababu ya kuvunja mkataba ule.

Mhe. Spika, suala moja ambalo la msingi ni kwamba kulikuwa na matatizo kwamba *Philtex* inaandikisha meli za Iran, na Iran na wakubwa wa dunia walitaka wawekewe vikwazo, inaonekana kwamba sisi kama Serikali ya Zanzibar tumeajiri *Philtex* na *Philtex* inaajiri meli za Iran. Kwa hivyo, tukatakiwa katika Uhusino wa Kimataifa na Kidiplomasia kwamba suala hilo mkataba na *Philtex* uvunjike kwa sababu akiambiwa alikuwa hafuati kuziachia meli hizo ambazo zilikuwa hazipungui 36.

Lakini *Philtex* alikuwa ana makosa mengi tu hapa ninayo hayapungui tisa. Moja, wakala kuijuulisha serikali iwapo wakala atafunga ofisi sehemu nyengine duniani, alikuwa hatwambii.

Wakala atatoa huduma kwa mujibu wa Sheria na Kanuni chini ya Sheria ya *MTA* ya 2006 alikuwa hafanyi.

Wakala kufuata maelekezo ya serikali, alikuwa hafanyi.

Wakala kuijuulisha serikali kwa maandishi anapoteua watu wengine nje ya kampuni yake, alikuwa hafanyi.

Wakala kuishauri serikali juu ya uteuzi wa *Ma-regional Office Commander*, alikuwa hafanyi.

Wakala kutoa taarifa kwa serikali baada ya kukamilika kwa usajili wa awali, alikuwa hafanyi.

Wakala kufuatilia hali za meli walizozisajili na kuiarifu serikali pale inapohitajika, alikuwa hafanyi.

Meli zote zinazosajiliwa zinatakiwa kutimiza viwango vya kiusalamu, alikuwa hatwambii.

Wakala kutoa taarifa ya meli zilizozuiliwa na *Port State Control Officer* yaani ikiingia nchini. Ni mengi makosa aliyokuwa akifanya na sisi tulikuwa na wajibu kumshitaki au kumnyang'anya huo uwakala, lakini ilipotokea na hili la Kimataifa ndio uamuzi ukaja kwamba tumsimamishe *Philtex* asifanye kazi hiyo.

Mhe. Spika, suala la kwa nini kapewa *Al-Khaleej* na watu kuwa na wasi wasi kwamba labda kumtokea mambo yasiyokuwa mazuri. Sasa hiyo kila binadamu na hasa kwenye kula wasi hawishi. Iisipokuwa wamekuja kuniambia. Mwenyekiti wa Kamati kwamba wanakusudia katika moja ya safari zao za kutembelea shughuli zao watakwenda Dubai. (*Makofsi*)

Mhe. Spika, huru waende wakaichunguze waone ukweli ulivyo, halafu wataripoti watatueleza kama vile wanavyopita kwenye maidara yetu kufanya shughuli nyengine. Mimi sina wasi wasi na ikiwa makosa yataokea yatasahihishwa.

Mhe. Mohamed Abood amesema hapa kwamba si lazima *CDMA* kuendelea kubaki na *Al-Khaleej*, na ule mkataba wenyewe haujafunga kwamba sisi tusiwe na wakala mwengine mzuri. Kama atatoka mzuri au tutatoa *tender* tupate mzuri zaidi, basi tutamchukua. Kwa hivyo, hiyo nadhani ni vizuri niishie hapo.

Mhe. Spika, suala la taa za Pemba nalo limesemwa sana. Kwenye taarifa yangu nimesema kwamba ikifika mwezi wa Juni hakutokuwa na tena na mishumaa kama alivyosema Mhe. Salum Abdalla, tunategemea taa za Pemba zitakuwa zimeshatiwa pale. Tumeshamaliza mambo ya *tender* na mkataba umeshatiwa saini na tunategemea kwa mwezi wa Juni suala la taa za Pemba litakuwa nalo halipo tena.

Mhe. Spika, suala la Wete na Bakhressa, ni kweli kwamba tumemkubalia Mhe. Bakhressa ajenge sehemu ya upande wa kama unatoka juu kuingia gatini Wete mkono wa kulia, upande ule ndio ametakiwa yeye kama anajenga ajenge kule. Lakini hajengi kwa kutaka anavyotaka yeye, atajenga kwa makubaliano na Shirika la Bandari. Na kwa kiasi fulani jamani bandari ya Wete imekufa fofofu nimemsikia Bi Farida anavyolalamika hapa, haipo. Na nusu ya watu wa Pemba ilikuwa safari zao wanashuka bandari ya Wete, haipo, wote inabidi waje Mkoani.

Sasa kama itajengwa bandari ile upande ule wa mkono wa kulia na meli zitakuwa zinakwenda hizo za Bakhressa itarahisisha na wenzetu wa Pemba vile vile kupata huduma nzuri. Lakini wenyewe Shirika la Meli wao wametegemea wana upande wa mkono wa kushoto nao waendeleze bandari ile, iwe huku zinakuja za serikali kule zinakwenda za Bakhressa na suala la kwamba atumie yeye moja kwa moja ni suala la mkataba. Mkataba huo ameleta Bakhressa wameutizama shirika wamerejesha, wamepeleka maoni yao kwake na mwisho itafikisha kwa Mwanasheria Mkuu na serikali kwamba basi kama unajenga masharti yetu haya. Lakini si vizuri kumuachia mزالendo akatumia rasilimali zake kuimarisha sehemu ya mahitaji ya wananchi kwa sababu tu kwamba labda atakuwa hivi, atakuwa hivi. Mhe. Spika, mimi natoa wito, kama kuna matajiri wengine basi waje watujenge ya Mkoani na masharti tutawapa laini.

Mhe. Spika, samahani nina mfano mmoja nadhani nishawahili kutoa hapa, nilikwenda Baltimore; Marekani katika ziara za kikazi miaka hiyo nilipokuwa Katibu Mkuu nikaonana na Meya wa pale Baltimore, Marekani. Mji Mkongwe kama hivi wakataka mji ule ubadilike, lakini sisi tulipofika tayari umebadilika isipokuwa ile sehemu kongwe bado wanayo. Tukamuuliza umefanya nini? Anasema katika *best hoteli duniani* ni Hilton na wengine *Hyatt*, akaenda kwa Managing Director wa *Hyatt* Meya wa Mji wa Baltimore akamwambia njoo bwana nitakupa ardhi bure na kila kitu bure ujenje hoteli. Yule jamaa akasema *but there's no business there*, akamwambi *okay*, *Hyatt* akajenga. Hivi sasa nendeni Baltimore uko huko mbinguni, kwa sababu baada ya kuja ile Hyatt Hotel ikawa *potential* ya makampuni kuja.

Sasa mara nyengine unapompa mmoja kuanza shughuli nyengine zinafunguka, na hiyo ndio inaitwa maendeleo. Hatuwezi tukakaa tukangojea tu bandari ya Wete iko fofofu, aah basi asipewe, maana yake aah masharti tu ya ujenzi itategemea tutakavyokubaliana, lakini lazima Wete nako kuwe na sehemu ambayo watu wa Kaskazini Pemba wanapata nafasi kuweza kufika kwa urahisi.

Mhe. Spika, mkataba na *Transworld* umetiwa Dubai lakini kutia mkataba Dubai au London au Japan au Marekani *is not cheat*, si suala la msingi. Suala la mkataba huo kama utafuata masharti au makubaliano yaliyotakiwa na serikali. Waliokwenda kutia mkataba ule ni Maofisa wa juu wa serikali akiwemo Katibu Mkuu Fedha, Katibu Mkuu Miundombinu na Mwanasheria Mkuu na Mkurugenzi wetu Mkuu wa Uwanja wa Ndege.

Sasa mkataba ule ulikuwa na masharti kwamba baada ya miezi sita aanze kufanya *operation*, mkataba umetiwa tarehe 12/10/2014 miezi sita inamalizika mwisho huu. Taarifa niliyopewa na watu wangu ni kwamba anaanza

ku-mobilize analeta vitu. Kama masharti hatotimiza hatuzuiwi sisi kukaa tena kama tutatoa *tender* kumtafuta mwengine, lakini Uwanja wa Ndege pale lazima kuwe na mashindano hapawezi pakawa na kampuni moja inayotoa huduma. Na hatuwezi kuiachia kampuni moja kwa sababu moja kubwa.

Ndugu zangu *Qatar Airways* wanataka kuleta ndege kuanzia Juni, *Emirates* wanataka kuongeza safari, *Oman Air* wanataka kuongeza safari, *Turkey* wanataka kuongeza safari, Ufaransa wanataka kuja, sasa hatuwezi ikawa kila siku huduma zile za *handling* pale zikawa dhaifu, lazima ziimarike na ziwe na ushindani ili tuweze kupata watalii zaidi na kuongeza mapato ya nchi.

Kwa hivyo, na hilo kamati inakwenda Dubai na wakaone hali ilivyo wakiwa kuna matatizo basi tushauriwe serikali tutafanya vyenginevyo. Sasa Mhe. Hija Hassan anasema kwamba na Mhe. Hamza nadhani alisema kuna mawazo kwamba hii ni feki haikusajiliwa hapa.

Hayo nadhani ni masuala ambayo mimi siyajui kama ni feki au hajasajiliwa, hata ikifika hadi watu wetu wa serikali wakatia saini mkataba nadhani walijitahidi hivyo, lakini kama kuna haja ya kufanya uchunguzi basi ufanywe na ikiwa haipo sawa sawa, kama haipo kweli *Transworld* Dubai ni kampuni kubwa sana linauza vifaa vya ndege (*spares*) ndio nilivyoambiwa. Sasa kama na shughuli hiyo wanafanya bila shaka kuna uwezo waliofanya watu kuweza kulijua hilo.

Mhe. Spika, kuna suala namaliza...

Mhe. Spika: Kuna taarifa.

TAARIFA

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, Mhe. Waziri amemjibu Mhe. Hija mimi hajanijibu, mimi niliuliza utaratibu wa *tender*, kwanza *tender* kabla ya kwenda kutiwa huo mkataba utaratibu wa *tender* ulifuatwa? Hii kampuni ilishindwa na ndio maana tukasema tunataka hapa twende tukaona tupate hiso *documents*, tuone *tender* ilivyoitishwa na yule aliyekuwa *awarded* na utaratibu wa *tender* aliyekuwa *awarded* anatangazwa na wale waliokosa wanapewa taarifa. Hayo mambo yote yako *silence*, hicho kitu hakikufanyika Mheshimiwa hata ule mkataba hewa, mikataba feki inayotiwa, inatiwa na watendaji wa serikali sio natia mimi kutoka Kwa Mtipura, watendaji wa serikali. Sisi tunasema utaratibu haukufuatwa na ndio maana mpaka leo hiyo kampuni imeshindwa kufuata hayo masharti, hiyo miezi sita waliyopewa imeshafika hawajafanya kitu, hana wataalamu. Mtu kampuni inauza vifaa vya ndege sisi tunajua Dubai pale tunakwenda siku zote wana mlango wanaauza vifaa vya ndege ...

Mhe. Spika: Mheshimiwa hiyo sio taarifa sasa huo ni mchango mwengine. Mhe. Waziri endelea ili utoe majibu kuhusiana na suala hilo ambalo alikuwa ameliuliza.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Sijakufahamu Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Nasema uendelee kutoa majibu kwa mchango ambao umetolewa ambao hiyo inayozungumzia kwamba utaratibu labda wa *tender* ilikuwa haukufuatwa wewe utaelezee namna ambavyo mumefuata huo utaratibu au kama kuna makoseo utatueleza.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ninavyoamini mimi, mimi nimekuja suala hili lilishakamilika na ninavyofahamu ni suala la uamuzi wa serikali kama utaratibu haukufuatwa au umefuatwa kamati wataweza kufutilia na wakaona ukweli ukoje.

Mhe. Spika, suala la *E-Government* kazungumza Mhe. Hamad Masoud Hamad kwa urefu mimi sina maelezo zaidi kuhusu *E-Government*. Suala *E-Government* limekuwa muda mwingi linashughulikiwa na Wizara ya Fedha na hivi sasa ninavyolifahamu liko kwenye Afisi ya Rais kwa Mhe. Haroun Ali Suleiman ndiye anayeshughulikia suala hili.

Lakini hili suala analilosema Mhe. Hamad Masoud *E- Health* kwetu Wizara ya Mawasiliano halipo. Kama liko huko serikalini inawezekana labda kwa wizara nyengine ya Afya lakini kwetu halipo hiyo (a).

- (b) Ni kweli kwamba Mkonga umeanza zamani, jana Mhe. Waziri wa Fedha alijitahidi kueleza nilikuwa kwenye gari njiani kwenye shughuli nyengine akasema jambo hili ni jipy.

Mimi ninavyofahamu kwamba wizara nydingi tayari zimekuwa zinatumia Mkonga huo, kuna wizara baadhi, chache tu, kwa taarifa zilizoletwa katika serikali ambazo bado hazijatumika na moja katika wizara ambayo sasa inatumia mambo hayo ni nydingi kama wizara tatu au nne ndio hazijafikishiwa ule mkonga, na mkonga ni kweli kama alivyosema Mhe. Waziri wa Fedha masuala mapya kwetu. Ukitaka kuujua mkonga ni utizame kama vile mbomba wa maji unaotoka kule Welezo kushuka mjini huku sasa.

Sasa kila hatua unatia *pipe* unapata maji kutumia mbomba unateremka chini. Sasa baada yake kwa hii mkonga, na kwamba mkonga umeeenezwa nchi nzima uko chini ya ardhi kila kinachostahiki sasa panatiwa *pipe* unakuja kwenye wizara na wizara wanatumia. Yaani ule mkonga kazi yake ni kuchukua yale mawimbi yapishe pale kama vile unavyopokea mawimbi kwa kutumia minara ya juu ni kitu kipyta kidogo lakini nadhani Mhe. Haroun Ali Suleiman ndiyo iko chini ya dhamana yake.

Mhe. Spika, huduma za Muungano kwa Taasisi za Zanzibar nimebakisha suala moja au nitamaliza Mhe. Spika. Mhe. Ismail Jussa amezungumza kwa urefu suala la huduma za Muungano kwa Taasisi za Zanzibar. Nadhani hili Mhe. Spika, linatugusa sisi kwenye masuala ya Tanzania *Civil Aviation*. Kunapokuja ndege kutaka kutua Zanzibar inabidi tupate ruhusu ya *TCA*, na *TCA* wanaongozwa na sheria na ile sheria ndio inayotawala taratibu zao. Sasa mara nyengine tunapoomba Serikali ya Zanzibar wao wanatizama sheria inasemaje.

Kwa hiyo, mara nyengine inakuwa tunavutana, wao wanasimama na sheria lakini kwa Zanzibar ni maslahi ya kiuchumi. Kwa mfano, mfano mmoja ambao uko hai na tunaendelea nao na nimefika hatua na ukinishinda nitaurejesha serikalini ndege za *Qatar Airways* wanataka kuja kutua tunabidi tuombe ruhusa, sheria inasema hatuwezi kufanya hivyo mpaka tufanye kitu fulani kwa sababu ya sheria.

Sasa sisi tunasema aah hili si suala tu la sheria, kwetu sisi hili ni suala la kiuchumi. Kwa hivyo, kama ni watu wanaohusiana katika mambo ya Muungano inahitaji sheria ile itizamwe vipi itakavyoweza kuisaidia Zanzibar bila ya kuparaganya utaratibu wowote.

Kwa hivyo, masuala hayo yanaendelea, huo ni mfano mmoja tu lakini kuna na hizo ndege nyengine; kuna ndege hizi za *Italy* miaka mingi hapa zimekuwa zinakuja kama *charter* zaidi ya miaka 20 haiwezekani zaidi ya miaka 20 ndege zinakuja *charter* zinakuwa *charged* kama *charter*, tumeomba kwamba baada yake zionekane sasa kama vile ni ndege zinazokuja kwa *schedule* kama ndege nyengine.

Tumejitahidi tumefanikiwa, Katibu Mkuu wetu ameongoza ujumbe wamekwenda *Italy* kuhusu suala hilo limemalizika. Kwa hivyo, tunakwenda lakini mambo yenye ni ya kisheria.

Mhe. Spika, la mwisho Mhe. Hamza Hassan Juma ameuliza lini *Terminal II* itamalizika. Kwa mujibu wa maelezo tunayoyajua sisi Wizara ya Mawasiliano ilikuwa mwezi wa Oktoba tukabidhiwe kiwanja kile mwaka huu. Sasa hata hivyo kuna uwezekano muda huo ukapita kutokana na matatizo ya kifedha. Lakini suala la matatizo ya kifedha liko Wizara ya Fedha haliko chini ya wizara yangu, na bahati nzuri yeye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Utekelezaji wa mradi huo.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda na nadhani nimejitahidi, na wale wengine wameuliza masuala mengine ambayo tumeyapokea kama maelezo lakini vitu hivi ndivyo niliviyoviona vya muhimu ya kuvitolea maelezo zaidi. Nashukuru sana Mhe. Spika, naomba sana kuwasilisha. (*Makofî*)

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kusema machache juu ya yaliyochangiwa katika ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza napenda kutoa pondezi zangu za dhati kabisa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa agizo alilolitoa la kuondosha mita zote za *TUKUZA* katika visima vya maji. Hii Mhe. Spika, ni ishara kubwa ya imani kubwa aliyokuwa nayo Mhe. Rais kwa wananchi wake anaowaongoza. (*Makofî*)

Mhe. Spika, pili napenda tena kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuiagiza Wizara ya Fedha kulipa deni lote ambalo wanadaiwa *ZAWA* na *ZECO* na ameitaka Wizara ya Fedha ipeleke kila mwezi shilingi milioni mia tano. (*Makofî*)

Kwa kweli hii ni imani kubwa aliyokuwa nayo Mhe. Rais, kwa sababu suala la deni la *ZAWA* lilikuwa kama ni kero, maana kila tukienda kamati hili ni lalamiko, lakini kwa imani kubwa aliyokuwa nayo Mhe. Rais ametoa agizo hilo deni hili litabebwa na serikali. Kwa hiyo, *ZAWA* wafanye kazi zao kwa uaminifu na uadilifu ili walete maendeleo katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mhe. Spika, sasa naomba niwashukuru waliochangia wote. Waheshimiwa waliochangia katika ripoti hizi zetu mbili ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Wizara ya Ardhi.

Pia, naomba niwatambue hawa waliachangia kama ifuatavyo:

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Hamza Hassan Juma
3. Mhe. Abdi Mosi Kombo
4. Mhe. Salim Abdalla Hamad
5. Mhe. Hamad Masoud Hamad
6. Mhe. Hija Hassan Hija
7. Mhe. Farida Amour Mohamed
8. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
9. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais; na
10. Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi.

Naomba niwapongeze sana Mhe. Spika. Michango yao ni mizuri, imelenga kuisaidia serikali yao, wametoa michango pamoja na ushauri. Kwa hiyo, ninachoomba kwa serikali pamoja na wizara husika michango hiyo iliyotolewa wazidi kuifanya kazi na ushauri walipewa waufanyie kazi.

Mhe. Spika michango imelenga katika maeneo yafutayo:

- (1) Ujenzi wa Bandari ya Mpiga Duri, Mkokotoni na bandari nyengine,
- (2) Wajumbe nao wamechangia kuhusu deni la *ZAWA*. Deni la *ZAWA* kwa kweli ndio limeshafutwa hilo,
- (3) Kituo cha daladala,
- (4) Mikataba mbali mbali ikiwemo mikataba ya *Philtex*,
- (5) Ukarabati wa nyumba ya Kengeja,
- (6) Uwekaji wa taa Uwanja wa Ndege Pemba, na
- (7) Usimamizi wa Ardhi, Usajili pamoja na Mahakama ya Ardhi.

Mhe. Spika, hayo ndio niliyaona Wajumbe wengi wamejikita katika kuchangia katika maeneo hayo. Kwa hiyo, mim sina zaidi Mhe. Spika, ninachoomba naiomba wizara na serikali kwa jumla hii michango yote inayotakiwa ifanyiwe kazi zaidi naiomba serikali wizara waifanyie kazi na sisi kama Kamati Mhe. Spika, tutaifatilia kwa

karibu zaidi ili kuona kwamba maagizo haya yanatekelezwa ipasavyo. Baada ya kusema haya Mhe. Spika naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

Mhe. Spika: Mhe. Marina Joel nakushukuru sana, Waheshimiwa Wajumbe sasa kazi kwenu niwahoji wale wanaokubali na kupokea utekelezaji. Najua mna hamu sana, lakini lazima tuyaseme haya ili *hansard* inarikodi nini tumepisha.

Kwa hiyo, wale ambao wanakubali na kupokea utekelezaji wa Wizara ya Ardhi Makaazi, Maji na Nishati pamoja na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, pamoja na Ripoti ya Kamati ya mwaka 2014/15 wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofî*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

Mhe. Spika: Nilikuwa nawasiliana na Mhe. Waziri wa Fedha kujua muda gani atatumia katika kuiwasilisha ripoti ya utekelezaji wa Kamati ya *PAC*, akanambia ni kiasi cha dakika 20 hadi 25 hivi ambazo nimeziona zipo. Tunaendela Katibu.

TAARIFA ZA SERIKALI

Waziri wa Fedha Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza yaliyotokana na Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC) ya Mwaka 2013/14

Mhe. Spika: Naomba sasa kwa heshima nimkaribishe Mhe. Waziri wa Fedha. (*Makofî*)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nasimama mbele ya Baraza lako kwa ajili ya kutimiza wajibu wangu nikiwa Waziri mwenye dhamana ya fedha. Naomba uniruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi kwa kutuwezesha sote kwa pamoja kukutana tena leo hii.

Mhe. Spika, kanuni ya 108 (15) ya Baraza lako hili Tukufu inamtaka waziri wenyewe dhamana ya fedha kuwasilisha mbele ya Baraza hili taarifa ya serikali juu ya utekelezaji wa pendekezo la Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali *PAC*.

Kwa kuwa kwa sasa mimi ndiye waziri mwenye dhamana hiyo ya fedha, naomba nichukue fursa hii kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Baraza la Wawakilishi yaani (*PAC*) kwa mwaka 2014.

Hata hivyo, kabla ya kutekeleza jukumu langu hilo naomba kwanza kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kuiwezesha Kamati ya *PAC* kuweza kufanya kazi zake kwa umahiri na uweledi mkubwa.

Aidha nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hiyo ya *PAC*, na kwa muda maalum Mwenyekiti wake Mhe. Omar Ali Shehe Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chake Chake. Utendaji mzuri wa kamati umeisaidia sana azma ya serikali ya kuimarisha usimamizi wa fedha za Umma ikiwemo Mapato na Matumizi ya Serikali. Niruhusu Mhe. Spika, kuipongeza kwa dhati Kamati ya *PAC* kwa utendaji wake mzuri.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi kwa niaba ya serikali sasa naomba niwasilishe taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma yaliyotolewa kutoptaka na ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2013/14.

Mhe. Spika, katika Ripoti ya mwaka 2013/14 Kamati ya *PAC* ilifuatilia ripoti mbili za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo ni hizi zifuatazo:-

- (1) Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Wizara, Mashirika na Taasisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 2011/12

- (2) Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu wa Miradi ya Taasisi Tasisi za Serikali Ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 2011/12 .

Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, Kamati katika kupitia Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Wizara, Mashirika na Taasisi za Serikali ya mwaka 2011/12 iliweza kuchambua hoja 92 zilizogawanyika katika sehemu kuu tano zifuatazo:-

- (1) Matumizi ya Fedha za Umma yasiyofuata utaratibu wa sheria za fedha na sheria za matumizi ya mwaka 2005.
- (2) Baadhi ya Taasisi kutowasilisha hesabu za mwisho wa mwaka kwa ajili ya ukaguzi.
- (3) Baadhi ya mali za serikali kukodishwa kwa maslahi binafsi na hivyo kukiuka sheria za nchi.
- (4) Kulimbikizwa kwa madeni ya Taasisi za Umma.
- (5) Suala la Ripoti ya *CAG* kuchukua hatua na serikali kabla ya kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi, na hivyo kuzuia utendaji kwa kamati.

Mhe. Spika, kwa upande wa ripoti ya ukaguzi yakinifu kwa miradi ya taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya mwaka 2011/12. Kamati ilifuatilia hoja 18 zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ambazo zimegawanyika katika maeneo makuu sita yafuatayo:-

- (1) Serikali kufuta ukodishwaji wa Ardhi kwa wawekezaji bila ya kufuata utaratibu au kushindwa kwa wawekezaji kuyaendeleza maeneo husika.
- (2) Baadhi ya wawekezaji kupewa ardhi na kutoiendeleza kwa kipindi kirefu.
- (3) Madeni ya ardhi ya muda mrefu kwa miradi ya hoteli na mengineyo ya uwekezaji na serikali.
- (4) Baadhi ya wawekezaji kutumia ardhi bila ya kulipia kodi.
- (5) Kiwango cha Kodi ya Ardhi kutofanyiwa mapitio.
- (6) Idara ya Ardhi kutokuwa na kumbukumbu kwa baadhi ya maeneo yaliyotolewa kwa wawekezaji.

Mhe. Spika, kasoro zilizobainishwa baada ya kupitia ripoti hizo mbili kilicho jitokeza ni kuwa kwa muhtasari, kamati ya *PAC* imebainisha kasoro kuu zifuatazo:-

- (1) Bado kuna ukiukwaji wa taratibu za matumizi ya fedha za umma kwa baadhi ya Taasisi za Serikali.
- (2) Kuna upungufu unaohitaji kurekebishwa katika sheria mbali mbali ikiwemo Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2005, Sheria ya Ununuzi na uondoshaji wa mali za Serikali ya mwaka 2005, Sheria ya Ardhi na Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 2004. Aidha kasoro pia zimejitokeza katika Sheria za Serikali za Mitaa na Sheria za Mitaji ya Umma.
- (3) Uwezo mdogo wa wahashibu wa Serikali za Mitaa yaani Halmashauri na Wilaya na kutokuwepo na wakaguzi wa ndani.
- (4) Matumizi yasiyofuata utaratibu katika fungu la Mfuko Mkuu wa Serikali.
- (5) Uwezo wa Bodi ya Mapato Zanzibar.
- (6) Kusuasua katika Kituo cha Uwekezaji yaani *One Stop Centre* kinachochangia matumizi mabaya ya ardhi.

- (7) Kuwepo kwa wawekezaji ambao ama shughuli zao ni kinyume na maombi ya awali ya muwekezaji au kutojulikana kwa shughuli zinazofanyika nchini.
- (8) Kuwepo kwa madeni ya muda mrefu katika taasisi za umma.
- (9) Udhaifu katika usimamizi wa Sekta ya Ardhi.

Mapendekezo ya kamati ya utekelezaji wake Mhe. Spika, kutokana na kasoro zilizobainishwa Kamati yako ya *PAC* ilioa ushauri kwa serikali kama nilivyosema awali naipongeza sana Kamati ya *PAC* kwa kazi yake nzuri kwa ushauri inayotoa kwa serikali.

Kwa upande wake serikali kupitia Wizara ya Fedha imeyapitia mapendelezo yote ya *PAC* na utekelezaji kwa taasisi zinazohusika upo katika hatua tofauti. Taarifa kamili ya utekelezaji kwa kila pendekezo la Kamati ya *PAC* imeibainisha na naomba iingizwe katika *hansard*, kwa sababu ya wingi wa mapendekezo na haja ya kuzingatia muda.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu nitoe maelezo ya utekelezaji kwa zile kasoro za jumla zilizobainishwa na *PAC*. Maelezo hayo ni kama yafuatayo:-

Kwanza kuchukua hatua za kinidhamu kwa watendaji wanaohusika na ukiukwaji wa utaratibu wa matumizi ya fedha za umma.

Mhe. Serikali tunakubaliana na *PAC* juu ya umuhimu wa watendaji kusimamia ipasavyo mapato na matumizi ya fedha za umma. Tunakubaliana pia kuwa kuna hatua kadhaa zinazoweza kuchukuliwa pindi ikibainika kuwa taratibu za sheria hazikufuatwa ipasavyo na mtendaji, hatua hizo ni pamoja na hatua za kiutawala na kinidhamu na inapobidi kisheria, uamuzi wa hatua gani kati ya hizi zichukuliwe kwa wahusika inategemea sana mazingira na ukubwa wa jambo lenyewe. Iwapo kuna ubadhirifu au ni suala la uelewa na kadhalika. Tunapaswa pia kutilia maanani ukweli kwamba majukumu mengi ya kifedha yanakabidhiwa kwa watendaji ambao kitaaluma sio watu wa fedha.

Mhe. Spika, serikali...

MUONGOZO

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ni utaratibu kwamba jambo linalowasilishwa na likawekwa mezani wajumbe wako tunatakiwa tupatiwe nakala, na hasa katika suala zito kuliko kamati zote, Kamati zinazosimamia hesabu za serikali *PAC*.

Sasa Mhe. Waziri anatusomea majibu ya serikali lakini sisi mpaka dakika hii hatuna nakala yoyote humu ndani. Kwa hivyo, hata mtu unataka kuweka kumbukumbu zako, maana yake wengine uwezo wa kuhifadhi juzuuthalathini umetushinda chuoni hatuwezi kuupata hapa Mhe. Spika.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana Mhe. Spika, kuwa tupatiwe hizo na kama haipo Mhe. Waziri tumruhusu kwanza mpaka tuwe nazo, tukijue anachokisoma ndicho ambacho sisi tunacho huku, naomba muongozo wako Mhe. Spika. (*Makofî*)

Mhe. Spika: Hivi watendaji mnanipeleka wapi, imo na imesomwa hati zimewasilishwa kuonesha kwamba shughuli hii itafanyika mara baada ya shughuli iliyomalizika. Sasa nilifikiria hivi vitu vitakuwa viro, hebu ziko wapi eenh. Sasa zigaiwe.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nadhani tuna haja ya kuwa makini sisi Wajumbe wako. Tulichogaiwa hapa ni maagizo ya mwaka jana ya kamati, ambapo kwa utaratibu kwamba kila mmoja ikifika zamu yake tunapewa maagizo ya mwaka jana kujikumbushe sio ripoti aliyosoma Mhe. waziri. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofî*)

Mhe. Spika: Mhe. Waziri uliichapisha ukaleta ofisini.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, taarifa niliyoipata mimi kwamba ripoti hizi zimewasilishwa lakini nikaambiwa kwamba watu wangu wameambiwa taarifa inasomwa kesho. Nikasisitiza kwamba taarifa tunasoma jioni.

Mimi naomba kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa tuakhirishe turudi jioni tuje tuisome jioni baada ya ripoti kupewa. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Nafikiri ni sababu ya msingi mimi nilitegemea kwa kuwa hati imekwishawasilishwa hapa na mambo yake yatakuwa yako karibu. Kumbe kwa bahati mbaya yalikuwa hayajatayarishwa. Hiyo ni sababu ya msingi ya kutufanya tuahirishe shughuli zetu hadi jioni ili kuhakikisha kwamba taarifa hii inayosema Mhe. Waziri itakuwa Wajumbe wanayo na itakuwa wanaifuatilia wakati anaendelea kusoma.

Kwa hiyo, kwa sababu hiyo nakubali tuahirishe kikao hiki hadi jioni saa 11:00 jioni. Tuhakikishe watendaji ripoti hizo ziko tayari kwa Wajumbe kufuatilia wakati waziri anawasilisha. Tufike saa 11:00 barabara leo.

(*Saa 6:46 Baraza lilahirishwa hadi saa 11:00 jioni*)

(*Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza niombe radhi pale kipindi cha asubuhi mchana pale, mambo yalikuwa hayajakamilika. Kwa hivyo kazi ambayo Mhe. Waziri alianza kuifanya ile ni ajuwari.

Hivyo naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwa kuwa kazi yangu ya mchana ni ajuwari, naomba nianze upya. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena ninasimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kutimiza wajibu wangu nikiwa Waziri mwenye dhamana ya fedha. Naomba uniruhusu nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi kwa kutuwezesha sote kwa pamoja kukutana tena leo hii.

Mhe. Spika, Kanuni Na.108(15) ya Baraza lako Tukufu inamtaka Waziri mwenye dhamana ya fedha kuwasilisha mbele ya Baraza hili, taarifa ya Serikali juu ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali (*PAC*). Kwa kuwa kwa sasa mimi ndiye Waziri mwenye dhamana hiyo ya fedha, naomba nichukue fursa hii kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Baraza la Wawakilishi (*PAC*) kwa mwaka 2013/2014.

Hata hivyo, kabla ya kutekeleza jukumu langu hilo, naomba kwanza kukushukuru wewe binafsi kwa kuiwezesha *PAC* kuweza kufanya kazi zake kwa umahiri na ueledi mkubwa. Aidha, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hiyo ya *PAC*, na kwa namna maalum Mwenyekiti wake Mhe. Omar Ali Shehe Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake. (*Makofi*)

Utendaji mzuri wa kamati umesaidia sana azma ya Serikali ya kuimarisha usimamizi wa fedha za umma ikiwemo mapato na matumizi ya Serikali. Niruhusu Mhe. Spika, kuipongeza kwa dharti Kamati ya *PAC* kwa utendaji wake mzuri.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi kwa niaba ya Serikali, sasa naomba niwasilishe taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma yaliyotolewa kutohana na ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ya 2013/2014.

Mhe. Spika, katika ripoti ya 2013/2014, Kamati ya *PAC* ilifuatilia ripoti mbili za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo ni zifuatazo:-

1. Ripoti ya ukaguzi wa hesabu kwa wizara, mashirika na taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2011/2012.
2. Ripoti ya ukaguzi yakinifu kwa miradi ya taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2011/2012.

Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali:

Mhe. Spika, kamati katika kuitia ripoti ya ukaguzi wa hesabu kwa wizara, mashirika na taasisi za Serikali ya 2011/2012 iliweza kuchambua hoja 92 zilizogawika katika sehemu kuu tano kama zifuatazo:

1. Matumizi ya fedha za umma yasiyofuata utaratibu wa sheria za fedha na sheria za matumizi ya 2005.
2. Baadhi ya taasisi kutowasilisha hesabu za mwisho wa mwaka kwa ajili ya ukaguzi.
3. Baadhi ya mali za Serikali kukodishwa kwa maslahi binafsi, na hivyo kukiuka sheria za nchi.
4. Kulimbikizwa kwa madeni ya taasisi za umma.
5. Suala la ripoti ya *CAG* kuchukuliwa hatua na Serikali kabla ya kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi, na hivyo kuzuia utendaji wa kamati.

Mhe. Spika, kwa upande wa ripoti ya ukaguzi yakinifu kwa miradi ya taasisi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya 2011/2012, kamati ilifuatilia hoja 18 zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo zimegawika katika maeneo makuu sita kama ifuatavyo:-

1. Serikali kufuta ukodishwaji wa ardhi kwa wawekezaji bila ya kufuata utaratibu au kushindwa kwa wawekezaji kuyaendeleza maeneo husika.
2. Baadhi ya wawekezaji kupewa ardhi na kutoiendeleza kwa kipindi kirefu.
3. Madeni ya ardhi ya muda mrefu kwa miradi ya hoteli na miradi mengine ya uwekezaji na Serikali.
4. Baadhi ya wawekezaji kutumia ardhi bila ya kulipia kodi.
5. Kiwango cha kodi ya ardhi kutofanyiwa mapitio.
6. Idara ya Ardhi na kutokuwa na kumbukumbu kwa baadhi ya maeneo yaliyotolewa kwa wawekezaji.

Kasoro zilizobainishwa:

Mhe. Spika, baada ya kuitia ripoti hizo mbili kinachojitokeza ni kuwa kwa muhtasari, Kamati ya PAC imebainisha kasoro kuu zifuatazo:-

1. Bado kuna ukiukwaji wa taratibu za matumizi ya fedha ya umma kwa baadhi ya taasisi za Serikali.
2. Kuna upungufu unaohitaji kurekebishwa katika sheria mbali mbali ikiwa Sheria ya Fedha za Umma ya 2005, Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali kwa mwaka 2005, Sheria ya Ardhi na Sheria ya Uwekezaji ya 2004.

Aidha, kasoro pia zimejitokeza katika Sheria ya Serikali za Mitaa na Sheria ya Mitaji ya Umma.

3. Uwezo mdogo wa Wahasibu wa Serikali za Mitaa (Halmashauri na Wilaya) na kutokuwepo kwa Wakaguzi wa Ndani.
4. Matumizi yasiyofuata utaratibu katika fungu la mfuko mkuu wa Serikali.
5. Uwezo wa Bodi wa Mapato Zanzibar.
6. Kusuasua kwa Kituo cha Uwekezaji (*One Stop Centre*) kinachochangia matumizi mabaya ya ardhi.

7. Kuwepo kwa wawekezaji ambao ama shughuli zao ni kinyume na maombi ya awali ya mwekezaji au ama kutokujulikana kwa shughuli zinazofanyika nchini.
8. Kuwepo kwa madeni ya muda mrefu katika taasisi za umma.
9. Udhaifu katika usimamizi wa sekta ya ardhi.

Mapendekezo ya Kamati na Utekelezaji wake:

Mhe. Spika, kutokana na kasoro ilizobainisha Kamati yako ya *PAC* ilitoa ushauri kwa Serikali kama nilivosema awali, naipongeza sana Kamati ya *PAC* kwa kazi yake nzuri na ushauri inaotoa kwa Serikali. Kwa upande wake Serikali kupitia Wizara ya Fedha imeyapitia mapendekezo yote ya *PAC* na utekelezaji kwa taasisi zinazohusika upo katika hatua tofauti. Taarifa kamili ya utekelezaji kwa kila pendekeso la Kamati ya *PAC* nimebainisha, na ninaomba niingizwe katika *hansard*, kwa sababu ya wingi wa mapendekezo na hoja ya kuzingatia muda Mhe. Spika, naomba uniruhusu nitoe maelezo ya utekelezaji kwa zile kasoro za jumla zilizobainishwa na *PAC*.

Maelezo hayo ni kama ifuatavyo:-

1. Kuchukua hatua za nidhamu kwa watendaji waliohusika na ukiukwaji wa taratibu wa matumizi ya fedha za umma. Mhe. Spika, Serikali tunakubaliana na *PAC* juu ya umuhimu wa watendaji kusimamia ipasavyo mapato na matumizi ya fedha za umma. Tunakubaliana pia kuwa kuna hatua kadhaa zinazoweza kuchukuliwa pindi ikibainika kuwa taratibu za sheria hazikufuatwa ipasavyo na mtendaji. Hatua hizo ni pamoja na za kiutawala, kinidhamu na inapobidi za kisheria.

Uamuzi wa hatua gani kati ya hizo zichukuliwe kwa wahusika inategemea sana mazingira na ukubwa wa jambo lenyewe. Iwapo kuna udanganyifu (*fraud*) au ni suala la uelewa na kadhalika. Tunapaswa pia kutilia maanani ukweli kwamba majukumu mengi ya kifedha yamekabidhiwa kwa watendaji ambao kitaaluma siyo watu wa fedha.

Mhe. Spika, Serikali imepitia mapendekezo ya *PAC* pamoja na kuzingatia kwa kina mazingira ya kila kituo, wakati azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa fedha za umma zinasimamiwa vyema, kinachojitokeza kwa kesi zilizobainishwa ni haja ya kuelimisha zaidi kuhusu utaratibu na usimamizi wa masuala ya fedha kuliko dhamira ya kutenda kosa. Mapendekezo yote ya *PAC* kuliko dhamira ya kutenda kosa.

Mapendekezo yote ya *PAC* kwa suala la kuchukuliwa hatua za kinidhamu yamehusu Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Spika, Wizara ya Fedha imeandaa programu maalum ya kuelimisha watendaji wakuu na maafisa wahasibu hasa wale wasio na utaalamu wa masuala ya kifedha.

Kwa mnasaba huu ili kurekebisha kwa dhati kasoro zilizobainishwa, na kwa kuzingatia kuwa haikudhihirika nia ya kutenda kosa au udanganyifu, hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa zimeegemea zaidi katika upande wa kiutawala kuliko kinidhamu au kisheria.

Pili, Serikali kuchukua hatua za haraka kuzifanya mapitio na kuzifanya marekebisho Sheria ya Fedha, Sheria ya Manunuzi, Sheria ya Ardhi, Sheria ya Uwekezaji na Sheria ya Mitaji ya Umma ili ziendane na mazingira halisi pamoja na sera za Serikali.

Mhe. Spika, Serikali tayari imezifanya mapitio na kurekebisha Sheria ya Fedha za Umma, Sheria ya Manunuzi, Sheria ya Ardhi, Sheria ya Uwekezaji.

Miswada ya marekebisho ya sheria hizi ipo katika hatua za mwisho ya kuwasilishwa Serikalini, ili hatimaye ziwasilishwe katika Baraza la Wawakilishi.

Aidha, Sheria ya Mitaji ya Umma ipo katika mchakato wa kufanyiwa mapitio kwenye mwaka huu wa fedha 2014/2015.

Tatu, kuteua watendaji wa Serikali za Mitaa wenye uwezo na siyo kuangalia kiwango cha elimu pekee.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba utendaji mzuri unahitaji mambo mengi ikiwemo elimu na wataalamu, uzoefu wa kazi na uadilifu. Kwa upande wa Halmashauri za Wilaya tatizo la muda mrefu lililokuwa pia likipigwa kelele na Baraza lako Tukufu ni ukosefu wa wataalamu wenye sifa.

Mhe. Spika, ili kutatua tatizo hilo, Serikali imechukua hatua ya kupeleka wataalamu wenye elimu ya uhasibu na fedha kama ilivyohitajika. Tunaamini kasoro iliyobainishwa kwa Mhasibu kushindwa kufunga hesabu za Halmashauri ilikuwa ya muda mfupi, na tayari kazi hiyo inafanyika ndani bila ya kutumia wataalamu wa nje ya Halmashauri.

Nne, kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha katika fungu la Mfuko Mkoo wa Serikali.

Mhe. Spika, Serikali itaendelea na usimamizi imara kwa matumizi ya Mfuko Mkoo wa Serikali. Kwa suala lililobainishwa kama kasoro, maelezo ya kina yalikwishatolewa kuwa fedha hizo hazikutumika moja kwa moja Mfuko Mkoo. Matumizi yaliyohojiwa yalihusisha fedha zilizopelekwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Redio Bungi. Haya ni kama matumizi mengine yoyote ya Wizara ambayo hutolewa Mfuko Mkoo na kupelekwa katika Wizara au taasisi ya Serikali.

Dhima ya kusimamia matumizi hayo baada ya kutolewa fedha inakuwa kwa Afisa Mhasibu (*Accounting Officer*) na siyo katika Mfuko Mkoo. Kuhusu matumizi mengine ya huduma za Mfuko Mkoo, Wizara imechukua hoja ya Kamati na inaizingatia.

Hata hivyo, inajulikana kuwa matumizi hayo zaidi ni kwa malipo ya mishahara na maslahi ya viongozi wakuu yaliyotajwa katika Katiba. Malipo kwa ajili ya kiinua mgongo na pencheni, malipo ya dharura kadri yanavyojitokeza na malipo kwa ajili ya kuhudumia mikopo mbali mbali ya Serikali kama vile hatifungani na dhamana za Serikali.

Tano, kuijengea uwezo ZRB kwa kuiwezesha kutumia *EFD* katika ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Spika, Serikali inakubaliana pia kasoro zilizobainishwa na Kamati ya *PAC*. Ni kweli kwamba suala ni kwamba ipo haja ya kuisimamia, kuimarisha usimamizi katika utoaji wa risiti, na hivyo kuhami mapato ya Serikali limekuwa likitokeza mara kwa mara katika vikao vya Serikali.

Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza lako Tukufu na katika Baraza lenyewe. Rai ya kuanzishwa utaratibu wa kutumia vifaa vya kutoa risiti (*Electronic Fiscal Device*) *EFD*, lilipendekezwa pia katika maabarasi iliyoangalia namna ya kuimarisha mapato ili kuleta ustawi katika matayarisho ya bajeti ya mwaka jana. Hadi sasa Serikali imeunda Kamati Maalum ya kulisimamia vyema suala la uanzishwaji wa *EFD* hapa Zanzibar, ili kuepuka matatizo yaliyojitokeza sehemu nyengine ikiwemo Tanzania Bara.

Ushauri wa *PAC* wa kuijengea uwezo ZRB kwa kuanzisha matumizi ya *EFD*, kwa hivyo unaendelea kuchukuliwa hatua. Jitihada pia zinaendelea kuchukuliwa kuimarisha matumizi ya Teknohana katika ukusanyaji wa mapato ndani ya ZRB na Serikali kwa ujumla.

Sita, serikali kufanya mapitio ya washiriki katika kituo cha *One Stop Centre* kilichopo *ZIPA* pamoja na sera za uwekezaji ili lengo liendane na uhalisia katika utekelezaji wake.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba muda mrefu sasa dhamira ya kuifanya Mamlaka ya Uwekezaji (*ZIPA*) kuwa kituo kimmo tu cha kushughulikia masuala ya uwekezaji (*One Stop Centre*) haikuweza kufanya kazi. Hali hii imekuwa ikikatisha tamaa wawekezaji wetu, na hivyo kupunguza kasi ya maendeleo.

Mhe. Spika, ili kasoro hii tayari Serikali imefanya mapitio na kuongeza washiriki wa kituo kwa kuwashirikisha Msajili wa Biashara na Mali. Aidha, maafisa wote waliopo sasa ni wale wenye uwezo wa kutoa maamuzi wakiwa katika kituo hicho. Hali ya utendaji wa sasa wa *ZIPA* inatia moyo kwa kuwa dhamira ya kuwa kituo kimmo cha masuala ya uwekezaji inakaribia kutimia.

Saba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkoo wa Hesabu za Serikali aelekeze nguvu katika ukaguzi kwa miradi 547 ya uwekezaji iliyo Zanzibar ili kubaini wawekezaji ambao shughuli ni tofauti na zile zilizomo katika maombi yao walilipia kodi ya ardhi na kodi nyengine.

Mhe. Spika, tunaamini kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameupokea ushauri huu na utauzingatia wakati wa kuandaa mpango wa ukaguzi, japo kwa kufanya ukaguzi huo kwa awamu na kutumia vigezo vya kitaaluma katika ukaguzi (*sampling*).

Serikali haina tatizo na ukaguzi huo, la umuhimu ni ufanyike kwa utaratibu mzuri na usiwajengee hofu wawekezaji.

Nane, Serikali kupitia Hazina kuratibu madeni yote ya taasisi za umma na kuyaandalia utaratibu wa kuyalipa ili kuziondoshea mzigo wa bajeti taasisi za Serikali.

Mhe. Spika, naomba kukiri pia kuwa taasisi nyingi za Serikali zimejitokeza kurudia kurundika madeni. Kwa upande mmoja kasoro hii inajitokeza kutokana na uhaba mdogo wa raslimali fedha katika kuhudumia bajeti ya Serikali na Wizara zake. Hata hivyo, kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Fedha ya 2015 yanayokataza Wizara na Taasisi za Serikali kuingiza (*commit*) Serikali katika madeni, Serikali ilizikataza Wizara na Taasisi hizo kurundika madeni mapya. Mnamo kati kati ya miaka 2000, Serikali ilihamishia Hazina madeni yote ya muda mrefu na kuzielekeza Wizara na Maafisa Wahasibu kuhakikisha kuwa madeni mapya yanahudumiwa na Wizara yenye kuitia bajeti zao na mgao wao wa fedha zinazopata.

Mhe. Spika, ili kuongeza nidhamu ya matumizi, Serikali haikusudii kuhamisha tena madeni hayo Mfuko Mkuu wa Serikali, badala yake itaendelea kusimamia na kuhakikisha kuwa kila Wizara inayorundika deni inalipa deni hilo kupitia bajeti yake.

Tisa, kuimarisha usimamizi wa ardhi kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

1. Kuweka usimamizi makini kwa watendaji wa Idara ya Ardhi.
2. Kurekebisha na kukamilisha kwa sera ya ardhi.
3. Kuharakisha kukamilisha kwa malipo kwa mapitio ya Sheria ya Ardhi.
4. Kuharakisha kukamilisha kwa usajili wa ardhi
5. Kuharakisha kukamilisha kwa *master plan* ya ardhi Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kama ilivyobainishwa na Kamati ya *PAC*, suala la usimamizi bora wa ardhi linapaswa kupewa mkazo wa pekee. Katika muundo wa Wizara inayosimamia ardhi, masuala ya ardhi yalikuwa yamewekwa chini ya Idara tofauti na kuunganishwa kwenye ngazi ya Katibu Mkuu tu.

Suala hili lilionekana ni kasoro mojawapo iliyopelekea pendekezo la Kamati ya *PAC*. Mhe. Spika, ili kurekebisha kasoro hizo na kuendana na ushauri wa Kamati ya *PAC*, Serikali imeonelea vyema zaidi kuweka masuala yote ya ardhi chini ya taasisi moja. Kwa mnasaba huu Serikali iliwasilisha Mswada wa kuanzisha tena Kamisheni ya Ardhi. Ninalishukuru sana Baraza lako Tukufu kwa kukubaliana na mapendekezo ya Serikali na kuridhia kuanzishwa kwa Kamisheni hiyo ya Ardhi.

Ni matumaini yetu sote sasa kuwa Kamisheni hiyo mpya itafanya kazi zake kwa ueledi na uadilifu mkubwa, na kuondoa kasoro zote zilizojitokeza hivi sasa ikiwemo zilizotolewa ushauri na Kamati ya *PAC*.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine Serikali tayari imeshakamilisha mpango mkuu wa matumizi (*Land Use Master Plan*) na ule wa maendeleo kwa maeneo; *special land development plan*.

Mhe. Spika, naomba kuhitimisha kwa kukushukuru tena wewe binafsi, Kamati ya *PAC* na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili kwa mashirikiano tunayoyapata kutoka kwenu. Ni matumaini yangu kuwa ufanuzi nilioutoa utaongeza uelewa kwa Wajumbe katika maeneo ambayo serikali imeyachukilia hatua. Kama nilivyosema awali maelezo hayo ni muhtasari tu kwa yale mambo makubwa yaliyojitokeza katika ripoti ya kamati ya *PAC*, maelezo ya utekelezaji wa kila pendekezo la *PAC* yametolewa katika *matrix*. Hata hivyo, kutokana na ukubwa wake wa muda haitayumkini kuisoma yote hapa na kutoa nakala kwa kila Mjumbe.

Naomba yaliyomo yote yawekwe kwenye kumbukumbu za Baraza, yaani *Hansard* na *matrix* yenye iwepo maktaba ya Baraza kwa kila Mjumbe kuweza kuisoma.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba niseme tena kwamba suala la uimarishaji wa usimamizi wa fedha za umma ni la muda mrefu, tunajivunia mafanikio yaliyopatikana hadi sasa katika mageuzi.

Hata hivyo, bado tunaelewa kuwa wote kwa pamoja kuna kazi kubwa ya kufikia pale ambapo sote tungeridhika, bila shaka kuwa usimamizi wetu ni imara, serikali itaendeleza jitihada zake hadi mageuzi yanayoendelea yatakapofanikiwa kwa kiwango kikubwa na kwa uendelevu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha.(*Makofit*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha, baada ya shughuli hiyo basi sasa naomba nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma.

Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma (PAC): Mhe. Spika, naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia na kutuwezesha kuhudhuria kikao hiki tukiwa wazima wa afya.

Aidha, nikushukuru wewe Mhe. Spika kwa kuniruhusu na kunipa fursa ya kusimama mbele ya chombo hiki kwa nia ya kuwasilisha Ripoti ya Kazi ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa 2014/2015 inayohusu Ripoti nne za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka 2011/2012 na 2012/2013.

Mhe. Spika, kabla ya kufanyakazi niliyoikusudia, naomba kwanza kwa niaba ya Kamati yangu nitoe mkono wa pole kwa Uongozi na Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi, wanafamilia pamoja na wananchi wa Jimbo la Magomeni kwa kuondokewa na kiongozi na mwanafamilia Marehemu Mhe. Salmin Awadh Salmin.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape wote moyo wa subra na amlaze marehemu mahala pema peponi, Amin!

Mhe. Spika, kwa upande wangu binafsi na walio wengi wetu tunamkumbuka Mhe. Salmin Awadh kwa ujasiri wake wa kujenga hoja ndani ya Baraza hili, kuwa ni mtetezi wa mamlaka ya Baraza kama chombo cha wananchi pamoja na uwajibikaji wa Serikali katika chombo hiki. Hatuna neno kubwa zaidi la kuonesha tulivyoguswa na tukio hili zaidi ya kusema “*Innaa Lillahi Wainnaa Ilayhi Raajiun*”.

Mhe. Spika, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma kwa mwaka huu ilizifanyia kazi ripoti nne kama zifuatazo:-

- i. Sehemu ya Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 2011/2012.
- ii. Sehemu ya Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ya mwaka 2011/2012.
- iii. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 2012/2013.
- iv. Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, naomba niitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, licha ya changamoto kubwa ya kibajeti na kitaalamu inayendelea kuikabili Afisi yake, kwa kuendelea na kazi ya kutoa ripoti kwa wakati, pamoja na kuibua maeneo mapya ya ukaguzi na aina mpya ya ukaguzi.

Ni dhahiri kuwa umuhimu wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu unaendelea kufahamika na umuhimu wa kazi ya Mdhibiti kuititia ripoti zake unaendelea kufahamika na kuheshimika mionganoni mwa wananchi.

Mhe. Spika, isingekuwa vyema kufunga ukurasa huu pasi na kutoa pongezi na shukurani maalum kwa Wajumbe wa Kamati hii, kwa mashirikiano na kazi kubwa ya kuzipitia, kuzichambua na kuzifanyia kazi ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu zinazopokelewa na Kamati kutoka kwa Baraza hili kwa kila mwaka. Mimi binafsi nafahamu baada ya kuiongoza Kamati hii kwa kipindi cha miaka miwili na nusu nikiwa Makamo na miaka mitano sasa katika Uongozi wa Kamati hii, juu ya ugumu, uzito na changamoto ya ama kuiongoza au ya kuwa Mjumbe wa Kamati hii kutohana na ukweli kwamba, Kamati inazifanyia kazi Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ambazo msingi wake ni utekelezaji wa Sheria za Fedha, Sheria za Manunuzi, Sheria za Ukusanyaji wa

Mapato na matumizi (*Appropriation and Finance Act*) pamoja na Sheria nyenginezo zinazosimamia taasisi mbali mbali za umma nchini mwetu.

Mhe. Spika, mbali ya ugumu na changamoto ya uelewa wa Sheria na mambo mengine ya kitaalamu yanayohusiana na Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, jambo jengine ambalo limekuwa ni tatizo kwa Kamati na hata Wajumbe wa Baraza hili ni uhaba wa muda wa kufanya kazi kwa Kamati ukilinganishwa na wingi wa ripoti ambazo huambatana na uhalisia wa jambo la uchunguzi.

Mhe. Spika, hapa naomba ikumbukwe kuwa, mwaka jana (2014), Kamati yangu iliwasilisha sehemu ya Ripoti ya Ukaguzi ambayo leo hii tunakamilisha sehemu ya ripoti hiyo iliyobaki. Ukiachia mbali suala hilo naomba niliarifu Baraza kuwa hata Ripoti ya mwaka 2012/2013 ambayo tulikabidhiwa mwaka jana mwezi Julai kwa tatizo la muda wa kufanya kazi litokanalo na uwezo wa Baraza kifedha, kamati hii imeshindwa kukamilisha kuifanyia kazi kwa ujumla wake na hivyo sehemu ya Ripoti hii, hasa Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu wa Mazingira, itakamilishwa na kuripotiwa kwa Baraza Jipyala 2016 *Inshaallah*.

Mhe. Spika, utaratibu au mwenendo huu wa ripoti moja kufanyiwa kazi nusu nusu na ikaripotiwa nusu nusu si tu haipendezi, bali pia haikubaliki kutokana na ukweli kwamba; -

1. Wajumbe waliopo sasa kama baadhi yao hawakurudi hawatoweza kujua hatma ya ripoti waliyoanza kuifanyia kazi;
2. Wajumbe wapya hawatoweza kufahamu msingi wa hoja, majibu ya mapendekezo na hatua zilizochukuliwa na Serikali; na
3. Baraza kushindwa kukabiliana na kasi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ya uandaaji wa ripoti kwa kila mwaka na kwa kila kipindi inapotokezea CAG kufanya Ukaguzi Maalum.

MAENEKO YA HOJA ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU NA UCHUNGUZI WA KAMATI

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kueleza awali kuwa Ripoti nne za Mdhibiti ambazo Kamati ilizifanyia kazi, ziligawika katika maeneo yafuatayo;

1. Eneo la mapato na matumizi ya Wizara na Taasisi nyenginezo za Umma;
2. Ukiukwaji wa taratibu za malipo yanayofanywa na Wizara, Mashirika na Taasisi nyenginezo za Umma;
3. Miamala ya madeni katika Taasisi za Umma;
4. Ufungaji wa Mahesabu katika Taasisi za Umma;
5. Hali ya Mashirika na Taasisi za Umma zinazojitegemea;
6. Ukaguzi Maalum wa Viinua Mgongo;
7. Ukaguzi Yakinifu wa Mali na Miradi ya Maendeleo; na
8. Ukaguzi wa uharibifu wa mazingira.

I UKAGUZI WA MAPATO KATIKA MAWIZARA NA SEKTA NYENGINE ZA UMMA

Mhe. Spika, moja kati ya kazi muhimu inayofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni utekelezaji wa makusanyo ya kodi na yasiyo ya kodi yanayofanywa na Taasisi mbali mbali za umma, ikiwa ni sehemu ya makusanyo ya mapato ya kibajeti, kama yanavyoidhinishwa na Baraza hili wakati wa Bajeti kuitia Sheria ya Matumizi (*Appropriation Act*).

Uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa; -

1. Asilimia 85 ya Taasisi ziliweza kufikia malengo kati ya asilimia 90 – 100 ya makadirio ya makusanyo;
2. Asilimia 7 ya Taasisi zilivuka lengo kati ya asilimia 105 – 140 ya makadirio yaliyowekwa; na
3. Asilimia 8 ya Taasisi zilikusanya chini ya lengo kwa asilimia kati ya 50 – 84 ya makadirio yaliyofanywa.

Kwa upande wa makusanyo ya ndani ya jumla yanayosimamiwa na Bodi ya Mapato kama Wakala wa Serikali, hali inaonesha kutokutengamaa kwa kipindi cha miaka mitatu ambapo mwaka 2011/2012, jumla ya Tsh.119,858 bilioni zilikisiwa kukusanywa ambapo makusanyo halisi yalifkia jumla ya Tsh. 120,544 bilioni, sawa na asilimia 100.57.

Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 jumla ya Tsh. 171,350 zilikisiwa kukusanya na hadi kumalizika kwa mwaka jumla ya Tsh. 177,723 sawa na asilimia 103.72.

Mhe. Spika, licha ya hali ya makusanyo ya mapato kuonekana kuvuka lengo kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ikilinganishwa na asilimia 87.46 kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Uchunguzi wa Kamati yangu umebaini kuwa, makusanyo yanayokusanya na kufikia ama kuvuka lengo, hayana uhalisia kwa vile hadi sasa serikali haijawa na kipimo sahihi cha kuweza kufahamu uhalisia na uwezo wa makusanyo kwa mujibu wa vyanzo stahili vya mapato tulivyonavyo nchini na katika kila taasisi. Sababu inapelekea kuwepo kwa udhaifu katika kufanya makisio ya juu ya mapato (*maximum level*), pia sababu inayopelekea kuwa na udhaifu katika zoezi lenyewe la ukusanyaji wa mapato hayo.

Hali hii kwa mujibu wa uchunguzi wa Kamati unasababishwa na baadhi ya mambo yafuatayo:-

1. Serikali kutokuwa na uwezo na vigezo katika ukadiriaji wa mapato yatokanayo na vyanzo tofauti katika sekta za umma na zile za watu binafsi. Hii ni pamoja na ukadiriaji wa viwango vya kodi ya mapato yenye.
2. Serikali kushindwa kudhibiti magendo ya mafuta.

Mhe. Spika, hapa naomba ifahamike athari itokanayo na magendo ya mafuta kwamba kila lita moja ya mafuta, kodi ya serikali ni Tsh. 500. Kwa hivyo, tunaporuhusu magendo ya mafuta kiasi gani serikali hupoteza fedha kupitia magendo ya mafuta, ikiwa tumepambana na magendo ya karafuu kwa nini tushindwe kwenye magendo ya mafuta.

3. Udhaifu katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na shughuli za Mahoteli ya Kitalii kutokana na watendaji wa Bodi ya Mapato (*ZRB*) kutokuwa na uwezo wa kitaalamu na kiteknolojia ya kuweza kukagua mifumo ya kihasibu, hali inayopelekea wenye mahoteli kudanganya juu ya uhalisia wa kodi inayostahiki kulipwa serikalini.
4. Kuwepo kwa ulegevu katika matumizi ya risiti za malipo pamoja na mifumo ya ulipaji wa kodi ama mapato.
5. Athari ya kuwepo kwa mamlaka mbili za ukusanyaji kodi (yaani *TRA* na *ZRB*) katika nchi moja.
6. Uwezo mdogo wa Bodi ya Mapato kiutendaji.
7. Serikali kushindwa kubuni vyanzo vipyta vya kodi sambamba na kuendeleza vilivyopo.

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi ya serikali hali inaonesha kuzidi kuelemewa na ukubwa wa matumizi yasiyolingana na mapato yanayokusanya katika kila mwaka wa fedha. Ripoti ya Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2012/2013 inaonesha hali mbaya ya uingizwaji wa fedha katika taasisi za umma kama ifuatavyo:-

1. Asilimia 10 ya Taasisi ziliingiziwa fedha wastani wa asilimia kati ya 90 – 98.
2. Asilimia 70 ya Taasisi ziliingiziwa fedha wastani wa asilimia kati ya 55 – 90.
3. Asilimia 20 ya Taasisi ziliingiziwa fedha wastani wa asilimia kati ya 45 - 54.

Mhe. Spika, jambo hili linadhihirisha hali mbaya ya upatikanaji wa fedha katika taasisi za umma, hali itokanayo na udhaifu wa uchumi, udhaifu katika ukusanyaji wa mapato na udhaifu katika usimamizi wa mipango mbali mbali ya serikali.

USHAURI WA KAMATI KWA SERIKALI

Mhe. Spika, baada ya Kamati kufanya uchunguzi wake inashauri kwa Serikali mambo yafuatayo:-

Kwa upande wa ukusanyaji wa mapato;

1. Serikali haina budi kuwekeza katika kuimarisha uwezo wa Bodi ya Mapato katika kujenga uwezo wa watendaji wa Bodi ili waweze kukagua mifumo ya kiuhasibu katika miradi ya kitalii. Hii iwe ni pamoja na udhibiti wa matumizi ya mifumo ya kiuhasibu katika maeneo hayo.
2. Serikali iharakishe uingizaji wa matumizi ya mashine za *EFD* pamoja na matumizi ya risiti katika mauzo ya bidhaa na malipo ya huduma mbali mbali serikalini.
3. Kuna haja kubwa na ya haraka kwa serikali kudhibiti magendo ya mafuta.
4. Kuna haja kwa serikali kupitia wataalamu wa kodi kufanya utafiti juu ya viwango vya kodi pamoja na kufahamu wigo wa mapato kwa kila taasisi.

5. Serikali kuona haja na umuhimu wa Zanzibar wa kuwa na chombo kimoja cha kukusanya kodi. Utafiti unaonesha kuwa uwepo wa vyombo viwili vya ukusanyaji wa kodi, mbali ya kusababisha usumbufu kwa walipa kodi, lakini pia imekuwa ni chanzo cha uvujaji wa mapato hasa kwa bidhaa za nje zinazoanza kuratibiwa zikiwa nje ya nchi na *TRA* na kumaliziwa na kodi na *ZRB*.
6. Ili kukuza uchumi na kuongeza ukusanyaji wa kodi, kuna haja kubwa kwa Serikali kubuni na kuvumbua vyanzo vipyta vya kiuchumi kama vile uendelezaji wa maeneo huru ya kiuchumi, utekelezaji wa sera ya Bandari Huru, Uvuvi wa Bahari Kuu, uchumi wa eneo la mafuta na gesi, uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo na kadhalika.
7. Uimarishaji, uendelezaji na ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika ujenzi wa uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi ya serikali. Hali inategemea upatikanaji wa fedha ambapo kabla tuliona kuwa hairidhishi wakati ambapo matumizi ya serikali yanaongezeka kila mwaka. Hata hivyo, hali ya kutotosheleza kwa bajeti katika matumizi ya serikali yanasaababishwa na;

1. Ukubwa wa serikali yenye mapungufu ya usimamizi, ubadhirifu na udhaifu katika utoaji wa huduma muhimu kwa wananchi.
2. Kuweko kwa matumizi ya serikali yasiyozingatia vipaumbele (hasa katika uwekezaji katika miundombinu ya uchumi na sekta ya elimu).
3. Uhaulishaji wa mafungu ya fedha usiofuata utaratibu.
4. Matumizi yasiyozingatia thamani ya fedha na tija.
5. Malipo ya matumizi hewa yanayofanywa na watendaji wa Serikali na ubadhirifu wa mali na fedha za umma.
6. Ucheleweshaji wa uingizwaji wa fedha katika mafungu kama yalivyoidhinishwa na Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, Kamati baada ya uchunguzi juu ya matumizi makubwa ya Serikali inashauri mambo yafuatayo:-

1. Serikali inapaswa kuwajibika kwa kuwachukulia hatua za kisheria na kinidhamu viongozi na watendaji wanaobainika kufanya ubadhirifu wa fedha na mali za umma.
2. Serikali inapaswa izingatie nidhamu katika kufanya matumizi na yaendane na mafungu kama yalivyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi.
3. Serikali inapaswa iwe makini katika kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo hazikutumika mwisho wa mwaka.

Mhe. Spika, naomba kurudia; serikali inapaswa iwe makini katika kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo hazikutumika mwisho wa mwaka zinarudishwa Hazina. Kinyume na utaratibu wa sasa wa baadhi ya taasisi “kuzihifadhi” fedha zinazobaki katika ‘Account’ binafsi.

MATUMIZI YA FEDHA ZA UMMA YASIYOFUATA TARATIBU

Mhe. Spika, kazi ya msingi yaani (*core function*) inayofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ni kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha baada ya kuidhinishwa na Baraza pamoja na kutoa kibali cha utolewaji wa fedha hizo, baada ya kuridhika kwamba fedha hizo ni zile zilizoidhinishwa na Baraza katika mafungu husika, na shughuli iliyoidhinishwa. Aidha, matumizi ya fedha hizo hutakiwa yafanywe kwa kuzingatia matakwa ya sheria za fedha, sheria za manunuzi na kadhalika.

Mhe. Spika, katika kipindi kirefu kilichopita Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu amefanya kazi kubwa ya kutoa ripoti za kila mwaka zikiainisha kasoro na dosari mbali mbali za matumizi ya fedha za umma.

Aidha, kamati hutoa mapendekezo kwa serikali katika kuona kuwa hatua madhubuti zinachukuliwa dhidi ya kukabiliana na vitendo vya ukiukwaji wa taratibu, ubadhirifu/wizi wa fedha na mali ya umma.

Sehemu ya Ripoti ya Ukaguzi wa kawaida ya mwaka 2011/2012 na ripoti ya mwaka 2012/2013 taasisi zilizoainishwa ama zilihusika na ukiukwaji wa taratibu za matumizi kwa kutoambatanishwa kwa viezelzo husika vya matumizi (*Supporting Document*) ama vifaa vilivyonunuliwa havikuingizwa ghalani, ama baadhi ya vifaa havikuoneshwa thamani halisi inayohusika ni kama zifuatazo:-

1. Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo;
2. Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.
3. Wizara ya Nchi, (AR), Ikulu na Utawala Bora;

4. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko;
5. Kikosi cha Valantia;
6. Wizara ya Kilimo na Maliasili;
7. Wizara ya Mifugo na Uvubi;
8. Bodi ya Mapato;
9. Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA);
10. Mamlaka ua Uvubi wa Bahari Kuu;
11. Hoteli ya Bwawani;
12. Chuo cha Maendeleo ya Utalii;
13. Chuo cha Uandishi wa Habari;
14. Mamlaka ya Mafunzo ya Amali;
15. Wizara ya Afya;
16. Wizara ya Nchi, (AR), Kazi na Utumishi wa Umma;
17. Wizara ya Nchi, (AR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ;
18. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano;
19. Mkoo wa Kaskazini (Unguja);
20. Baraza la Manispaa;
21. Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini “B”; na
22. Halmashauri ya Wilaya ya Kati

Mhe. Spika, Ripoti za Ukaguzi zimeainisha kuwa jumla ya Tsh. 16,282,137,509.77 matumizi yake hayakufuata utaratibu wa kisheria. Kamati yetu baada ya uchunguzi imejiridhisha kwamba:-

1. Ni kweli kwa sehemu kubwa (takriban asilimia 75) ya matumizi ya fedha hizo hazikufuata utaratibu;
2. Ni kweli kuwa sehemu ndogo (takriban asilimia 25) ya matumizi ya fedha hizo yalitumika sahihi, ila kasoro ilitokana na mawasiliano kati ya wakaguzi na wakaguliwa hasa katika kikao cha maagano (*Exit Meeting*).

Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe wafanye rejea katika Hoja ya Mdhibiti, majibu ya Watendaji na uchambuzi wa Kamati kama inayonekana katika Ripoti Kuu ya Kamati yetu.

Mapendekezo ya Kamati

Mhe. Spika, inaonekana kwamba utaratibu wa ukiukwaji wa taratibu za matumizi ya fedha za umma umezoleka na hauoneshi dalili za kupungua kama si kumalizika licha ya ukaguzi unaofanywa kila mwaka na makemeo ya Kamati na Wajumbe kila unapofika msimu kama huu wa uwasilishaji wa ripoti katika Baraza hili.

Mhe. Spika, hapana shaka sote tunafahamu athari ya vitendo hivi vinavyofanywa na watendaji wenye nia ovu ya kujitajirisha kwa njia za mkato na kwa kuwaibia wananchi. Bado pamoja na juhudhi zote mambo yanakwenda kama yaliyozoleka (*Business as usual*).

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena, Kamati ya PAC haijachoka na inaendelea kutoa mapendekezo yafuatayo:-

1. Serikali haina budi kuchukua hatua za wazi kwa watendaji wanaobainika kukiuka na kuiba fedha za wananchi;
2. Serikali ianzishe Idara ya Wakaguzi wa Ndani kama ilivyoahidi;
3. Serikali haina budi kuanzisha Kitengo cha Manunuzi ya Umma;
4. Serikali ifanye mapitio ya marekebisho ya baadhi ya Sheria zake zitakazojumuisha Ripoti ya Mdhibiti na Kamati ya PAC kuwa ni sehemu ya ushahidi unaoweza kutolewa Mahakamani;
5. Serikali iharakishe kufanya mapitio na marekebisho ya Sheria ya Fedha na Manunuzi ili ziendane na wakati;
6. Serikali kupitia Idara ya Hazina haina budi kuwa makini katika utoaji wa fedha kwenye Taasisi zake na fedha hizo zitolewe kwa wakati uliopangwa;

7. Serikali kuwa makini katika suala zima la uhaulishaji wa fedha katika mafungu. Suala hili limebainika kuwa ndio sababu kubwa ya kutokea matumizi yasiyofuata utaratibu;
8. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutilia nguvu ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa kuzingatia matumizi yanayolingana na thamani ya fedha (VFM); na
9. Serikali kuiwezesha Afisi ya Mdhibiti kuwa na uwezo wa kufanya ukaguzi wa wizi wa mtandao (*Cyber crime*).

Uwepo wa Madeni na Yanavyoathiri Ufungaji wa Mahesabu na Utekelezaji wa Bajeti

Mhe. Spika, Ripoti za Mdhibiti pamoja na mambo mengine huainisha pia uwepo wa madeni katika Taasisi za Umma na wakati mwengine katika taasisi za Watu Binafsi. Uwepo wa madeni katika Taasisi za Umma si tu unaathiri katika utekelezaji wa bajeti ambapo sehemu ya bajeti ya mwaka unaofuata hutumika kulipia madeni hayo lakini pia huathiri sana ufungaji wa hesabu hasa katika Taasisi zinazojitegemea kama vile Mashirika ya Umma.

Mhe. Spika, Taasisi zilizoainishwa katika ripoti hizo kuhusika na madeni (ama kudai au kudaiwa) ni hizi zifuatazo:-

1. Wizara ya Fedha;
2. Idara ya Mikopo (Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto);
3. Wizara ya Katiba na Sheria;
4. Ofisi ya Mrajis Mkuu (Wizara ya Katiba na Sheria);
5. Mamlaka ya Maji (ZAWA);
6. Shirika la Bandari;
7. Shirika la Magazeti;
8. Mamlaka ya Viwanda vya Ndege;
9. Chuo cha Utawala wa Umma;
10. Chuo cha Kilimo Kizimbanii;
11. Shirika la Magari;
12. Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana (Wizara ya Katiba na Sheria);
13. Wizara ya Afya; na
14. Shirika la Umeme (ZECO).

Mhe. Spika, ukaguzi umebaini jumla ya Tsh. 14,132,690,760 zimekuwa ni fedha zinazoonekana katika ufungaji wa hesabu katika Taasisi zetu lakini fedha hizo hazipo/hazitumiki kiuhalisia kwa vile ni fedha hewa (madeni). Nilisema kabla kwamba athari yake zaidi ni kwa Taasisi zinazojitegemea pale zinapochukulia kwamba hesabu hizo ni sehemu ya mtaji wa Taasisi hizo. Kwa upande wa athari kwa Taasisi za Umma zinazotegemea bajeti kutoka Hazina, athari kubwa ni katika kuziathiri bajeti zao katika kulipia madeni ya nyuma ambayo hayakuwa ni sehemu ya bajeti inayotumika.

Mhe. Spika, uchunguzi wa Kamati yangu umebaini kuwa moja kati ya sababu zinazopelekea kuzalisha madeni ni ukosefu wa nidhamu katika matumizi ya fedha za umma pamoja na kutokuingizwa kwa fedha katika taasisi kwa wakati uliopangwa.

Ushauri wa Kamati

Mhe. Spika, Kamati ya PAC inashauri mambo yafuatayo:-

1. Serikali na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya uhakiki wa madeni yote ambayo yamepitwa na wakati na yasiyolipika (*Bad Dept*) na kuyawasilisha mbele ya Baraza kwa lengo la kufutwa kama matakwa ya sheria yalivyo.
2. Serikali kupitia Idara ya Hazina kuchukua haina budi kuchukua dhamana ya ulipaji wa madeni yote yanayotokana na utoaji wa huduma muhimu kwa wananchi kama vile malipo ya umeme kwa huduma za afya na maji, malipo ya wagonjwa nje ya nchi.

3. Serikali kupitia Idara ya Hazina kubeba madeni yatokanayo na kitendo cha kutokuingizwa kwa fedha katika Taasisi ambazo tayari zimeshaidhinishwa fedha na Baraza la Wawakilishi.

Ukaguzi Maalum wa Viinua Mgongo

Mhe. Spika, kama tujuavyo kuwa sehemu kubwa ya fedha zinazotengwa katika bajeti kama ni sehemu ya matumizi ya kazi za kawaida, kutumika katika ulipaji wa mishahara na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF). Kwa mfano, jumla ya bilioni 183.6 hutumiwa kwa mwaka kwa malipo ya mishahara na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambayo ni sawa na asilimia (50%). Vile vile, sehemu kubwa ya fedha inayotengwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kila mwaka, yaani bilioni 2,232 kwa mwaka sawa na bilioni 186 kwa mwezi, hutumiwa kwa ulipaji wa viinua mgongo na pencheni kwa wafanyakazi wanaostaifu. Kiwango cha mafungu haya hutegemea sana na idadi ya wafanyakazi wanaostaifu.

Mhe. Spika, mfanyakazi anapostaifu hulipwa kiinua mgongo kulingana na muda aliofanyakazi pamoja na kiwango cha mshahara wa mwisho anachopokea. Hesabu kama hiyo hutumika katika kutengenezea malipo ya pencheni ya mfanyakazi huyo kwa kipindi chote cha uhai wake.

Mhe. Spika, nimeeleza hivi ili ifahamike namna gani Serikali inavyotumia fedha nyangi kwa ajili ya malipo ya viinua mgongo, lakini pia, kuonesha mahusiano ya kima cha malipo ya kiinua mgongo kinavyoathiri wingi wa fedha anazolipwa mstaifu kama pencheni katika kipindi chote cha uhai wa maisha yake kwa kila mwezi. Inapotokezea watendaji wakafanya michezo yao katika eneo hili la ulipaji wa viinua mgongo, tunapaswa tuone ni kwa kiasi gani, Serikali humoteza mamilioni kwa kila mwezi kwa malipo ya viinua mgongo hewa na pencheni ambayo hulipwa kwa kipindi chote cha uhai wa maisha ya mstaifu.

Mhe. Spika, mfumo wa ulipaji wa viinua mgongo huhusisha Taasisi tatu kuu kama ifuatavyo:-

1. Taasisi ya muajiriwa ambayo huhusika kwa kutayarisha taarifa za mtumishi kama vile; tarehe ya kuajiriwa, mwenendo wa nyongeza za mshahara pamoja na kiwango cha mshahara wa mwisho cha mtumishi huyo anayestaifu;
2. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo jukumu lake ni kuhakiki na kuthibitisha taarifa za mstaifu huyo na kutoa kibali cha malipo kwa Idara ya Hazina baada ya kuhakiki na kuridhika kwamba anastahiki kulipa.
3. Idara ya Hazina ambayo hufanya malipo baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Mdhibiti na mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, ukaguzi maalum uliofanywa na Mdhibiti umeonesha namna gani Serikali inavyopoteza na kuibwa Mamiloni ya Shilingi kila mwezi kupitia viinua mgongo na pencheni na kila mwaka. Kwa mfano; ukaguzi maalum uliofanywa kwa njia ya ‘sampling’ ya Taasisi 5 kama zifuatazo:

1. Chuo cha Mafunzo	-	8
2. Mkoa wa Mjini Magharibi	-	5
3. Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)	-	8
4. Wizara ya Elimu	-	22
5. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano	-	22

umeonesha mafaili 65 sawa na watendaji 65 ambao wametumia jumla ya Tsh. 131,717,898 kama ni nyongeza ya malipo ya kiinua mgongo kwa wastaafu hao, ambapo waliongezewa fedha kwa viwango tofauti. Kuna wengine waliongezewa kwa asilimia 100, wengine asilimia 50 na wengine asilimia 20 inategemea makubaliano yaliyofanyika baina ya mstaifu na ofisa waliyehusika.

Mhe. Spika, tunachozungumza hapa ni upotevu/ ama wizi wa fedha nyangi za umma zitokanazo na ulipaji wa mafao ya kiinua mgongo tu, tukilizungumza hili, ni vyema pia tukajumuisha na wizi wa fedha za umma zitokanazo na ulipwaji wa mishahara hewa. Mheshimiwa Spika, kwa mara nyengine tena sina budi nimpongeze kwa dhati Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kufanya zoezi la ukaguzi maalum wa malipo ya mishahara kwa Taasisi zote za umma ambapo baada ya ukaguzi huo haidhuru na yeche Ofisi yake iliusika katika sakaba hili la kini kwa baasisi zote za umma baada ya ukaguzi huo na ripoti kutolewa imedhihirisha kuwa, kiasi cha bilioni 1.8 kuibwa kila mwezi kupitia mishahara hewa.

Mhe. Spika, ni masikito ya Kamati yangu na kila anaeguswa na jambo hili kwamba, hadi sasa ripoti hiyo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imedhibitiwa na Serikali na imeshindikana kuletwi mbele ya Baraza ili Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi waweze kujua ukweli wa jambo hili na matumizi ya kodi zao kupitia malipo ya mishahara hewa kwa watumishi wa umma.

Mapendekezo ya Kamati

Mhe. Spika, kutoptaka na Serikali kuendelea kupoteza fedha nyingi za wananchi kupitia zoezi la malipo ya viinua mgongo na pencheni Kamati yangu inapendekeza hatua zifuatazo kwa Serikali; -

1. Wale wote waliohusika na wizi wa fedha katika ukaguzi uliofanywa ambao ni kutoka Taasisi zilizohusika pamoja na maofisa wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wachukuliwe hatua za kisheria na kinidhamu.
2. Serikali haina budi kuandaa au kuimarisha *data base* ya wafanyakazi wote wa sekta ya umma ambapo taarifa zake zitapatikana kwa Taasisi zote muhimu ikiwa ni pamoja na Taasisi husika, Wizara inayohusika na utumishi wa umma, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Wizara ya Fedha.

Ufungaji wa Hesabu kwa Taasisi za Umma

Mhe. Spika, kila mwisho wa mwaka wa fedha ni matakwa ya kisheria yanayowalazimisha Maofisa Masuul (*Accounting Officers*) kufunga hesabu na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaduzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya miezi mitatu tangu siku ya mwisho wa mwaka wa fedha kumalizika.

Mhe. Spika, ufungaji wa hesabu una umuhimu mkubwa sana kwa Taasisi za Serikali kwa vile hupelekea kufahamika:-

1. Fedha zilizotumika na zilizobakia mwisho wa mwaka katika mafungu;
2. Madeni, faida na hasara; na
3. Thamani ya mali kama mtaji wa Serikali.

Mhe. Spika, Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu zimeonesha maendeleo makubwa yaliyofikiwa ya ufungaji wa hesabu kwa wakati kwa Taasisi za Umma nchini. La kufurahisha zaidi ni lile suala la Taasisi zinazojitegemea ambazo kwa kipindi kirefu tumekuwa tukizilalamikia kwamba haziwasilishi hesabu zao katika Afisi ya Mkaguzi sasa tatizo hilo kwa kiasi kikubwa limetatuliwa, hivyo, Taasisi hizi zinawasilisha hesabu zao kwa Madhibiti kama Sheria za nchi zinavyoolekeza.

Mapendekezo ya Kamati

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamati ya Kudhibiti na Kuchunguza Hesabu za Serikali inapendekeza mambo yafuatayo:-

1. Kwa kuwa moja kati ya tatizo linalopelekea kukwamisha zoezi la ufungaji wa hesabu ni kutokuwepo kwa wathamini (*valuers*) wa mali pamoja na kutokuwepo kwa sera ya ushukaji wa thamani (*Depreciation Policy*). Kamati yangu inaishauri Serikali kuajiri wathamini wa kutosha katika Idara ya Uhakiki Mali.
2. Serikali iandae muongozo ama mfumo mmoja wa ufungaji wa hesabu kwa Taasisi zote za umma kati ya ule uliozoleka (*Cash Basis*) na ule wa kisasa (*Actual Basis*).

Hali na Mwenendo wa Mashirika ya Umma

Mhe. Spika, madhumuni makubwa ya uundwaji wa Mashirika ya Umma ni katika utoaji wa huduma bora na za uhakika kwa wananchi, kutoa ajira pamoja na kutoa mchango wa faida kwa Serikali.

Mhe. Spika, mwenendo wa Mashirika ya Umma umeonesha kusuasua katika miaka ya nyuma hadi hivi karibuni. Sura hii inatokana na ufungaji wa hesabu kwa Mashirika hadi miaka ya 2011 ambapo ilioneshi:-

1. Kutokufungwa kwa hesabu ya mwisho wa mwaka;
2. Kutokuwepo kwa Daftari la Mali (*Asset Register*);

3. Wingi wa madeni; na
4. Kuwepo kwa hasara na kutokulipwa kwa mgao Serikalini.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2012 – 2014 Mashirika mengi yameonekana kupata uhai (kupata faida) na kuanza kutoa mgao w faida kwa Serikali. Kwa mfano;

1. Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*);
2. Shirika la Bima;
3. Shirika la Bandari;
4. Shirika la Meli.

Mhe. Spika, kwa mafanikio hayo ya Mashirika, naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Fedha na Mawaziri wengine kutokana na umakini wao wa usimamizi, ufuutiliaji na uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ambao wametoa mchango mkubwa katika mafanikio hayo. Ni imani ya Kamati kuwa iwapo hatua zaidi zitachukuliwa na Serikali za;

1. Kuongeza mtaji hasa kwa Benki ya Watu wa Zanzibar;
2. Kuteua Wajumbe wa Bodi wenye uwezo zaidi kitaaluma;
3. Udhhibit wa matumizi holela; na
4. Kuwepo kwa menejimenti makini na adilifu.

Mhe. Spika, hapana shaka kuwa Mashirika yatapiga hatua zaidi na hivyo kuleta tija iliyokusudiwa ambayo ni kutoa huduma bora, ajira kwa wananchi na mgao wa faida Serikalini.

UDHIBITI NA UTUNZAJI WA MALI ZA UMMA

Mhe. Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa miaka mitatu sasa anaendelea kufanya Ukaguzi Yakinifu kwa kukagua udhibiti na utunzaji wa mali za umma kama vile samani, vyombo vya moto, majengo nakadhalika. Kamati yangu inafahamu umuhimu zoezi la udhibiti na utunzaji wa mali za umma kutokana na ukweli kwamba;

- 1) Asilimia 100 ya fedha zinazotengwa katika bajeti ya maendeleo na wahisani zinakwenda katika maeneo ya manunuvi ya huduma, mali na ujenzi; na
- 2) Asilimia 49 ya fedha zinazotengwa katika bajeti ya matumizi mengineyo zinatengwa kwa ajili ya manunuvi ya vifaa mbali mbali na huduma za uendeshaji wa shughuli za serikali.

Mhe. Spika, kwa maana hiyo tunabaini kuwa wastani wa asilimia 75 ya Bajeti Kuu inaelekezwa katika matumizi ya manunuvi.

Mhe. Spika, Kamati inapongeza kwa juhudhi iliyoanza kuchukuliwa ya kutayarisha madaftari ya mali (*Asset Register*) kwa baadhi ya Mawizara pamoja na uuuzwaji wa mali chakavu lakini changamoto iliyopo na inayoendelea kutukabili ni pamoja na;-

- 1) Kutokuwepo kwa uendelevu wa zoezi la kutayarisha madaftari ya kuhifadhi mali kwa baadhi ya Mawizara na Taasisi nyengine za umma; na
- 2) Kutokutengwa ama kutokutumika kwa mafungu ya matengenezo ya vifaa na majengo.

Mhe. Spika, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali inaishauri Serikali kuwa makini sana katika suala zima la utunzaji na udhibiti wa mali za umma kwa sababu ile ile kuwa hili ni eneo linalotumia fedha nyingi za wananchi kila mwaka. Serikali itakapolimudu hili itapelekeea kuokoa fedha nyingi za wananchi na hivyo Serikali itaweza kuzielekeza fedha hizo katika uboreshaji wa huduma za kijamii kama vile sekta ya afya, maji, elimu na kadhalika.

HITIMISHO

Mhe. Spika, Zanzibar kama ilivyo nchi nyengine za dunia ya tatu bado tunaendelea kuwa na tatizo kubwa la uchumi. Tatizo hili linapelekeea umasikini kwa wananchi wetu na huduma dhaifu za kijamii kama vile elimu, afya, maji safi, makaazi, usafiri na kadhalika, licha Zanzibar kuwa na vivutio kuwa na rasilimali nyingi sana.

Mhe. Spika, hali hii inachangiwa sana na mambo mengi, lakini msingi mkubwa unasababishwa na Serikali kutokuwa na uwezo wa usimamiaji wa utekelezaji wa shughuli zake, kuwa na sera zinazotekelzezeka, uwajibikaji kwa baadhi ya wenye dhamana, wizi na ubadhirifu wa mali za umma, ukosefu wa maadili kwa baadhi ya viongozi na kadhalika.

Mhe. Spika, hali ya kuongezeka kwa mapato katika miaka ya karibuni ni ushahidi tosha kuwa nchi yetu ya Zanzibar ina uwezo mkubwa wa kukusanya mapato ya ndani na ina fursa pana ya kutengeneza vyanzo vyengine vikubwa vya mapato iwapo tutakuwa na mamlaka ya kusimamia uchumi wetu. Sambamba na hayo, kuwa na viongozi makini, kuwa na viongozi waadilifu na kuwa na sera zinazotekelzezeka pamoja na kuipa nguvu na uwezo wa kibajeti Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo ndio yenye dhamana ya kudhibiti na kukagua matumizi ya fedha za umma.

Mhe. Spika, naendelea kuipongeza Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali licha ya changamoto mbali mbali zinazoikabili Afisi hiyo kibajeti na kitaaluma, lakini pamoja na hayo bado Afisi inaendelea kufanya ukagazi na kutoa Ripoti kwa wakati pamoja na kufanya ukagazi katika maeneo mapya kama ilivyofanya kwa Ukaguzi Maalum wa viinua mgongo, sekta ya ardhi, mazingira na kadhalika.

Mhe. Spika, Kamati inamshauri Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutupia macho kwa kufanya Ukaguzi Maalum katika maeneo mengine kama vile ukagua mikataba hasa katika maeneo ya ujenzi, ukagazi katika misamaha ya kodi, ukagazi katika mikopo ya ndani na nje, ukagazi katika miradi mbali mbali kama vile TASAF, ukagazi kama wa miradi wa ZUSP na kadhalika.

Mhe. Spika, tunatambua uwezo na changamoto nyengine zinazoikabili Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukagazi katika maeneo hayo. Hata hivyo, tunazidi kuiomba Serikali kuzidi kuwajengea uwezo kimaslahi Wakaguzi na Wataalamu wake kwa ujumla ili Ofisi iweze kutekeleza majukumu hayo kwa manufaa ya Taifa.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine tumeona mapungufu ya uwezo wa Baraza letu namna lilivyoshindwa kuziwezesha Kamati zake kutekeleza majukumu yake ya kikatiba ipasavyo ya kusimamia Serikali kuititia Kamati hizo. Kamati ya *PAC* kushindwa kukamilisha kazi ktika Ripoti ya mwaka 2012 ni ushahidi tosha kuwa Baraza haikuwa muda wa kutosha Kamati hii muda ambao ungetuwezesha kumaliza Hoja zilizomo kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hata hivyo, pamoja na tatizo hilo, kama ilivyo kwa umuhimu wa Serikali kujengea uwezo Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, ndivyo ilivyo kwa umuhimu kwa Baraza kujengea uwezo Kamati ya *PAC* ili iweze kuzitafsiri vyema na kuzifanya kazi Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa niaba ya Baraza.

Mhe. Spika, mengi tuliyofanya katika Kamati na kuonekana Kamati kuwa na uwezo wa kumudu shughuli zake, kulitokana na mafunzo tuliyopewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika miaka ya mwanzoni mwa Baraza hili la 8 pamoja na utashi wa Wajumbe wenyewe wa Kamati kujifunza mambo mbali mbali. Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kwa mara nyengine tena kumpongeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hatua ya kujengea uwezo Kamati yetu, uwezo ambao uliipelekea Kamati kuweza kumudu kutekeleza wajibu wake na hivyo kujengea heshima kubwa Baraza letu mbele ya macho ya wananchi.

Pamoja na yote ni vyema tukakubaliana na ukweli kwamba, ukagazi ni taaluma inayobadilika kwa kasi kubwa sana kila uchao kutoptana na mabadiliko ya teknolojia. Hivyo, Baraza lina wajibu wa kulizingatia jambo hili muhimu.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kukushukuru wewe kwa mara nyengine tena kutokana na miongozo na maelekezo yako ya mara kwa mara kwa Kamati yetu, miongozo iliyoisaidia sana Kamati kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Vile vile, natumia fursa hii kumshukuru sana Katibu wa Baraza kwa kuwezesha na kutupa ushauri uliokuwa ukitupata katika kipindi ambacho Kamati ilikuwa ikizifanya kazi ripoti hizi.

Katika shukurani zangu za pekee, niwashukuru pia watendaji wa Serikali kuanzia Makatibu Wakuu wa Wizara, Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma, Wakuu wa Taasisi mbali mbali, Makamanda wa Idara Maalum za SMZ, Wakuu wa Mikoa, Maofisa Tawala wa Mikoa na Makatibu wa Halmashauri na Mabaraza ya Miji. Aidha, napenda pia kumshukuru Mhasibu Mkuu wa Serikali, Wahasibu wa Wizara na taasisi husika, Wakaguzi wa Ndani na wale wote wanaotoa huduma katika sekta ya fedha, Manunuvi na Uingizaji na Utoaji wa vifaa

maghalani ma-store keepers hawa nao pia wamo katika taasisi zote za Umma. Wote tunawashukuru sana kwa mashirikiano yao kwa Kamati yetu.

Mhe. Spika, mwisho na si kwa umuhimu, katika kumalizia ukurasa huu wa shukurani, naomba kutoa shukurani maalum na za kipekee kwa Wajumbe wanaounda Kamati hii ninayoiongoza mimi, Omar Ali Shehe wajumbe wenyewe ni:-

1.	Mhe. Fatma Mbarouk Said	-	Makamo Mwenyekiti.
2.	Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	-	Mjumbe
3.	Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	-	Mjumbe
4.	Mhe. Rufai Said Rufai	-	Mjumbe
5.	Mhe. Salim Abdalla Hamad	-	Mjumbe
6.	Mhe. Salma Mussa Bilali	-	Mjumbe
7.	Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	-	Mjumbe

Aidha, kwa niaba ya Kamati, nitoe pia shukurani kwa Sekretarieti ya Kamati yenye watendaji wafuatao:-

1.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
2.	Ndg. Othman Ali Haji	-	Katibu
3.	Ndg. Asha Foum Makame	-	Afisa Sera, Wizara ya Fedha.
4.	Ndg. Hurina Said Mohamed	-	Afisa Bajeti, Wizara ya Fedha
5.	Ndg. Khalid Bakar Hamran	-	Afisa Sera, Wizara ya Fedha
6.	Ndg. Mfaume Mohamed Mfaume	-	Afisa wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu.

Kwa hakika Sekretarieti imetoa mchango mkubwa sana katika kufanikisha kazi za Kamati kwa kipindi chote cha kazi za Kamati.

Mhe. Spika, naomba pia niwashukuru Wenyeviti wenzangu wote wa Kamati za Kudumu za Baraza hili kwa mashirikiano na mashauriano ya karibu sana katika utendaji wa Kamati zetu. Nimalizie kwa kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza kwa usikivu na umakini mkubwa katika kufuatilia hotuba hii.

Ni imani yangu kuwa, Waheshimiwa Wajumbe wataichangia kwa nia ile ile ya Kikatiba ya kuisimamia Serikali dhidi ya matakwa ya wananchi. Aidha, ikiwa ni pamoa na kuunga mkono kwa dhati, mapendekezo ya Kamati kwa Serikali.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nikushukuru sana kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia ripoti hii ya *PAC*, kwanza niwapongeze sana Kamati ya *PAC*. Lakini mimi leo ningekuwa kama *professor* na nimo katika kusainisha mitihani basi ripoti iliyosomwa na Mhe. Waziri ningempa *marks* ya ziro. Kwa sababu tangu asubuhi nimekaa sana kuzijadili kuna ripoti zaidi ya tatu hapa, ya kitabu hii na hii haina *cover* na hii ina *cover* ya *red* kwa hivyo tayari keshajipiga kadi nyekundu mwenyewe, kwa hivyo nimepata shida sana.

Mhe. Spika, mimi nilitarajia leo Mhe. Waziri angetwambia sasa hivi wako 5, 6 Kinua miguu kwa watu amba walioiba fedha za wananchi tena za wavuja jasho na kama ingekuwa ni hivyo basi ningempandisha *credit* leo Mhe. Waziri. Lakini hata udhaifu wa juu unaonesha kule kuna watu watatu na Wizara hii kubwa sana na hasa leo ni siku ya ukaguzi, lakini labda inawezekana wamekimbia wameogopa *PAC* au mvua imenesha ndani ya chumba kilichonyesha mvua. Kwa hivyo Mhe. Spika, inasikitisha sana sana na nimeona nitoe kwa masikitiko makubwa na unyonge.

Mhe. Spika, *PAC* imefanya kazi nzuri sana inafaa utoe shahada fulani ya kuonesha hawa *PAC* ili watambulikane na wao kama wanavyotambulikana wale waasisi. Kwa sababu wamepita hata katika zile Kamati Teule za Ardhi wamepita mule mule, wametuonesha zimo humu. Wametuonesha jinsi gani mawazo yao walioota katika mambo ya ardhi yamo mengi tu na wameonesha jinsi gani hizi fedha ambazo za kinua mgongo mamilioni sio kimilioni kuanzia 35 milioni kuendelea mbele, ukizipiga *total* hizi basi mimi sidhani kama tutasikitika na bajeti finyu hata siku moja kumbe tunafanya bajeti finyu kwa makusudi.

Tunaoneana haya, hatuko *serious*, hiyo tuseme hivyo kwa sababu mambo hayo yanayofanywa ukionesha hasa ni udhalilishaji tosha, kwa sababu leo wananchi wetu huko nje wanapata tabu sana ndio hizi fedha ambazo tunaingia katika kuchangia kodi hii wanayotoa wananchi, tukisema kodi ifike kwa wananchi haifiki ndio kama na sisi tunakatwa katwa humu.

Mhe. Spika, sasa tufike pahali tusiogopane tuambizane ukweli tu kama kweli tuna nia ya kuwasaidia wananchi, baada ya wiki wapelekee kinua mgongo watu wala usione tabu kinua miguu. Mhe. Spika, kinua miguu apeleke watu sio kinua mgongo maana yake kinua mgongo kimo humu wala si vibaya, kinua mgongo ndio pesa chungu nzima zimeliwa humu kumbe ilikuwa naelekeza nichangia kiinua mgongo.

Kweli kinua mgongo humu watu wanajiongezea wanavyotaka wao tu. Sasa mimi ningeomba sana Mhe. Waziri pamoja na umahiri wake, Mhe. Waziri ni *credit* yake ya kuzungumza vizuri na ni mpangaji mzuri, kwanza hanuni tabia ya kununua yeye hana ni mzungumzaji mzuri sana na mpangaji wa *plan* mzuri sana. Lakini anaharibiwa na watendaji, Mhe. Waziri anapanga programu nzuri na makatibu wake lakini watu wanamharibu. Mheshimiwa usicheke nao hamna shemegi yako hata mmoja.

Unajua nchi za wenzetu wanapoharibu watendaji Waziri anajiuzulu, sisemi kama ujiuzulu hiyo *for example* tu mimi sitaki ujiuzulu bado *still* unaweza ku-work vizuri. Lakini natahadharisha isije ikatokea hivyo, Mheshimiwa bado unaweza una *spirit* nzuri. Jana umetupa vitu vitamu sana hapa, watu wote walishangaa, ilibidi hansard ziwe biashara wewe hujui. Lakini *hansard* watu wamezichukua kibao kabisa wa nje, wa ndani, umepanga vizuri sana *wallahi* nimeridhika jana. Lakini leo humu *nothing* hamna kitu, yale yote uliotupangia kwenye *hansard* jana humu leo hamna kitu. Sasa mimi hapa ndio nikashangaa sana.

Mheshimiwa ilitufafanulia jinsi ya mishahara, jinsi fedha zinavyogawika, jinsi fedha zinakwenda mpaka ukatufikisha kwenye madeksi, ukatufikisha unapotaka lakini leo kwenye ripoti hii nyepesi. Mheshimiwa ukasema nani kazitafuna tumtafute sisi, wajumbe wote washamjua nani aliyekula pesa za madeksi hapa wala si Waziri, kuna mtu huyu mmoja wanamuogopa watu kumsema na ndio huyo aliyekula ndio pesa zote katafuta za madeksi, waziri wala hazijui fedha.

Tusimuonee waziri lakini mtu huyu amechukua joho maana yake si Katibu, hajulikani cheo gani wala si waziri, lakini yeye anajifanya ndio *fantastic* wa kuweza kugawa mambo hayo. Mheshimiwa tunamzubaisha na ndio maana hii kucheka kucheka na watu hii ndio inayomuharibia mtu sifa. Mimi nikikwambieni mawaziri siku zote muwe *serious* na watendaji wenu nyinyi mnafikiria *just joke* mimi sina *joke* nao, mimi nasema kilicho ukweli kwa sababu ndio tunayaona tutamwandama waziri bure maskini kumbe mtu huyu mmoja ndio anasababisha waziri aandamwe. Nyinyi mnachekelea, nyinyi mnaachia Mheshimiwa muondoe mtu huyo nani, kitendawili Mhe. Waziri utamjua mwenyewe.

Mhe. Spika, niende katika masuala ya ardhi. Mimi niungane nao mkono na Mhe. Waziri wa Ardhi anakuwa mkali sana katika maeneo haya lakini ninamwambia tena bado yapo mahotelii hayalipi kodi, *serious* kabisa wala si mchezo. Kuna watu wamezuia viwanja mpaka leo hawalipi kodi wala hawajengi vipo tunaoneana haya, je nimto paka kwenye gunia. Mhe. Spika, bahati mbaya hizi hati leo ziko ndogo nimesahau miwani lakini ningemsema hapa, naomba niachieni kwenye bajeti.

Mhe. Spika, ninaomba sana kuna ripoti iliyokuwa nzuri sana ingetuongoza kama Mhe. Ali Mzee, ile ingetusaidia zaidi na ndio *PAC* wamepita humu humu katika sehemu hiyo. Mheshimiwa hii kuongeza muda nayo inatu-cost, ni nzuri lakini ni mbaya kwa sababu wengine hawako na kutaka kufanya lile suala wamechukua kuekeza kutafuta bei tu kuuza. Sasa anakwambia kila siku anaomba muda yuko katika matayarisho kujenga amezuiliwa, sijui na nini nalo hili Mheshimiwa naomba sana lina utata wake, lina matatizo yake, linatupotzeza mapato. Hoteli hiyo haishi tu kila siku. Mimi naomba Mheshimiwa hili suala nalo tulione kwa ukamilifu kabisa.

Jengine Mheshimiwa niseme bado iko haja ninafikiria hivi karibuni tulikuwa na hoteli nimesema inaitwa *VENTA CLUB*, Mhe. Waziri hebu njoo nambie hivi hoteli hii kapewa nani na mpakaleo huyo mtu aliyepewa ina miaka mingapi muda huo mpaka leo hii. Na mpaka leo still kulikuwa kuna majengo na leo kuna mwitu tu, hebu njoo unambie nani aliyepewa na kwa nini mpaka leo hajaendelea Mhe. Waziri Ramadhan apate kufuta, tunapeana wenyewe kwa mlango wa nyuma ukweli tuseme jamani.

Tunapeana watu waliokuja hawana uwezo wa kujenga mahotelii tunafichiana siri, nitahamaki mimi Mhe. Spika, ili tuje kuambizana ukweli hapa, tuje kununiana maana yake tumo humu humu, lakini tutanuniana. Lakini ukweli itafika pahali tutasema.

Mhe. Spika, lengo kuleta mradi, lengo kukusaidia Mhe. Waziri. Mhe. Waziri mengine niite kwa siri nitakwambia. Na tena siku hiyo kama Mhe. Jaku alisema kuwa anapokwenda na Wizara ende na televisheni na mimi siku hiyo nataka twende na televisheni nikakuuneshe wizi wako, nitakwambia hawa hapa. Mhe. Spika, inasikitisha kweli mtu anaanza kazi leo asubhi jioni ana nyumba kumi, hebu nambie anaanza kazi leo jioni ana nyumba kumi amezipata wapi hizo pesa? Na ile sheria vipi ile ya madini hajatiwa saini tu, inachelewa Mhe. Spika, kabisa maana yake ile ingeondoa utata wote, kwa sababu ile hajamuweka mtu.

Mhe. Spika, vile vile nawashukuru sana *PAC* kuna mambo mengine wametoa *well and good* wameridhika na watendaji katika sehemu nyengina kama shirika. Kwa mfano, hapa nimeona Shirika la *ZECO* nao wamesema hawana madeni yoyote, nashukuru sana kwa hilo na wengine bado wamesema kwamba waendelee aidha kupewa maeneo au kusaidiwa katika serikali kupewa nguvu zaidi. Nalo hilo mimi nalikubali kwa sababu wameenea sehemu zote katika hali halisi.

Mhe. Spika, ukweli usiojificha na huu lazima tuuseme, tuisipousema mheshimiwa inafika pahali mnatupa tabu sana. Mhe. Spika, barabara zetu hazina viwango ni kweli, nakubaliana nalo na moja kuwa hazina viwango na utata unaotufika barabara zetu hazina viwango, maana yake niseme hazina umbile la kuonesha vituo maalum. Kwa hiyo, tunafanya barabara zinakuwa *one way* haioneshi sehemu ya kuonesha kituo maalum nalo hili ni tatizo, pia hili linatuletea msongamano. Hata hiyo mipango miji, mipango miji si kazi yake kutengeneza barabara, ye ye kazi yake *ku-settle* tu mji ukae *view* ya aina gani. Lakini nani anayehusika kutengeneza barabara, barabara zetu ndio maana vituo viko ovyo ovyo tu, havitambulikani halafu leo tukiwakamata hawa tutakuwa tunawaonea wenye madaladala kusema ukweli, kwa sababu hatujaweka vituo maalum kutokana na barabara zetu.

Kwa hivyo, naomba sana usimamizi huu wa barabara lazima uwe na viwango, kwanza tuwe na michoro maalum. Hebu mimi niulize kweli tunakuwa tuna michoro Mhe. Spika? Mhe. Waziri hebu niambie tangu hatujaanza kujenga tunakuwa tuna ramani ya barabara au basi tu kata hapa ondoka hapa tia lami tuondoke, inawezekana kwa sababu tungekuwa tuna ramani maalum Mhe. Spika basi tusingekuwa na tabu ya kuwa barabara zetu haziweki. Wewe kaangalie Bumbwini unaanzia Mjini mpaka Bumbwini panakuunesha wapi kama hapa pana alama ya kituo, hebu niambie.

Tunakwenda International hii Zanzibar tunataka iwe *half* London bwana, lazima twende na wakati, lazima tugeuke tukitaka tuisitake tunajirudisha wenyewe nyuma Zanzibar tunajirudisha. Inasikitisha sana eeh, Mwenyezi Mungu anijaalie iko siku na mimi niwe Rais kwa sababu nitaweka viwango tu ya *ground* ya Zanzibar hii, ukweli tuseme.

Mhe. Spika, unajua inakuja ile katika raha ya kuzungumza kwa sababu waziri ana *level* ya kuweza kufanya zile kazi zake, lakini waziri anakuwa *general* wa Zanzibar nzima. Sasa mimi nitakuwa natoa ile *view* ya kuonesha hali halisi ilivyo. Mhe. Spika, naendelea usinipigie simu.

Mhe. Spika, kwa haya machache ninaunga mkono Kamati ya *PAC* asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru naomba nichangie ripoti hii ya kaka yangu Mhe. Omar Ali Shehe kwa niaba ya Kamati ya *PAC*, na nianze kwa kumpongeza sana Mwenyezeki wa Kamati ya *PAC* pamoja na kamati yake kwa ujumla kwa jinsi ambavyo wamewasilisha ripoti fupi lakini nzuri, ripoti iliyo wazi na ripoti ambayo inawaelimisha Wazanzibari jinsi gani fedha yao inatafutwa bila ya hisia.

Mhe. Spika, mimi nitatofautiana sana na Mhe. Makame Mshimba juu ya ripoti ya Mhe. Waziri wa Fedha, naona ni ripoti nzuri ameitoa na naomba niweke wazi kwamba ripoti hii ya *PAC* si ripoti ya Wizara ya Fedha peke yake, ni ripoti ya serikali nzima. Kwa hiyo, isionekane kwamba Waziri wa Fedha ndiye aliyewasilisha kwa niaba ya serikali, lakini ilipaswa kwamba mawaziri wote na watendaji wote wa Serikali ya Zanzibar wawepo leo hapa kusikiliza ripoti ya *PAC*. Na isionekane tu kwamba watendaji wa Wizara ya Fedha ndio wanaopaswa kusikiliza tu.

Hii ni dhahiri kuonekana kwamba hali ya serikali yenewe baadhi ya wizara hawajui kama ripoti hii ni ripoti ya serikali nzima na inapaswa wao wasikilize serikali nzima nini inaambiwa, ndio maana juu hao umaona watendaji wa Wizara ya Fedha tu na pengine watendaji wachache wa Ofisi ya Rais wengine wanajisahau kama kwamba hii ripoti sio ripoti yao.

Mhe. Spika, na nini maana yake? Maana yake ni kwamba wao wanachojua ni kuharibu tu lakini hawajui kwamba ni wajibu wa kulinda matumizi ya serikali.

Mhe. Spika, kwa hivyo ripoti hii ya *PAC* si ripoti ya Wizara ya Fedha peke yake au Ikulu ni ripoti ya serikali nzina na watendaji wote Makatibu Wakuu wa Wizara zote walipaswa leo wawepo wasikilize nini wanaambiwa na *PAC* na nini wameharibu.

Mhe. Spika, nianze kusema kwamba *page* ya mwanzo ya kitabu hiki cha Kamati ya *PAC* wamezungumza jinsi walivyoshindwa kufanya kazi juu ya ukaguzi mbali mbali ambapo wameonesha wazi kwamba wameshindwa kukagua maeneo ya viinua mgongo, miradi ya maendeleo na ukaguzi wa hesabu za mawizara na taasisi mbali mbali.

Mhe. Spika, ukaguzi huo wameshindwa wenzetu hawa kwa sababu ya mambo matatu muhimu.

La kwanza, wameshindwa kwa sababu ya uchache wa fedha;

La pili, wameshindwa kwa sababu ya uchache wa muda; na

Na tatu, wameshindwa kwa sababu ya ukosefu wa wataalamu hasa katika ukaguzi wa mambo yakinifu kwa maana ya *value for money*.

Mhe. Spika, *value for money* ikifanyika lazima ipatikane wataalamu wa kila eneo, wapatikane *ma-engineer*, wapatikane wataalamu wa mahesabu, wapatikane wataalamu wengine. Kwa hivyo, wenzetu hawa wa *PAC* wameshindwa kufanya ukaguzi kwa maeneo mengine hayo yaliyobakia kwa sababu ya fedha, muda na wataalamu wachache kwenye taasisi yetu ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, hii nini maana yake? Maana yake imetufunza kwamba ile sheria ya Mhe. Hamza ambayo kila siku anapiga makelele ya utawala wa Baraza ndio hii ingetatua hoja hizi tatu. Ingetatua fedha kwa maana ya Baraza, ingetatua muda maalum kwa maana ya kujipangia na ingetatua ukosefu wa wataalamu ndani ya Baraza athari yake sasa ndio imeonekana kwamba kumbe *PAC* inashindwa kufanya kazi kwa sababu ya ukosefu wa kuwepo sheria ya utawala ndio ambayo imetukwanza.

Mhe. Spika, na ndio maana leo bila kuona aibu Zanzibar tumekuwa na Bunge legelege, kwa sababu ya sheria ya utawala wa Baraza imeshindikana kutujenga Wajumbe Wawakilishi wako na kwa msingi huo ndio maana tukawa na serikali legelege serikali ambayo inaabudu mipango ya wizi kwa watendaji mbali mbali.

Mhe. Spika, *page* ya pili ambayo nataka nichangie ni maeneo ya upotevu wa mapato. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* ametuonesha kwamba mapato yamekuwa yakiptoea kwa njia mbili kubwa ambazo Mhe. Mwenyekiti ametuonesha.

Njia ya mwanzo ni magendo ya mafuta ambapo ametwambia lita moja ya mafuta inaigharimu shilingi mia tano. Kwa hivyo, mia tano ikipotea kwa lita moja lita nyingi zikipotea maana yake mabilioni ya pesa yanapotea kwa njia ya magendo ya mafuta. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nakubaliana na hoja ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* kwamba serikali ijenge njia madhubuti ya kudhibiti magendo ya mafuta ili kuokoa fedha mia tano kwa lita moja.

Mhe. Spika, lakini njia ya pili ambayo Mwenyekiti ametuashiria ni misamaha ya kodi. Mhe. Spika, misamaha ya kodi ni moja katika njia ambayo inapoteza mapato ya serikali na lazima tukubaliane na Kamati ya *PAC* kwamba misamaha ya kodi isiwe lazima, lazima idhibitiwe kwa lengo la kudhibiti mapato ya serikali.

Mhe. Spika, hoja ya tatu ambayo Mhe. Mwenyekiti ametubainisha ni matumizi yasiyozingatia samani.

Mhe. Spika, nakubaliana mimi na Mhe. Mwenyekiti wa *PAC* kwamba matumizi mengi ya serikali hayazingatii samani halisi ya vifaa vilivyonunuliwa. Kwa mfano, mimi nimeshuhudia utafiti mmoja mdogo *printer* ambazo zimenuliliwa ndani ya taasisi ya serikali, *printer* nane zimelipiwa mara nne ya gherama halisi ya soko, vipi nilijuaje? Niliona ile *invoice* ya bei nilimpigia simu Mkurugenzi wa kampuni inayouza nikajifanya kama ni mteja, akaniambia bei tofauti. Bei tofauti ile aloniambia mimi ni mara nane ya bei ambayo serikali imeuziwa, *printer* ile ile thamani mara nane. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba serikali imeibiwa ndani ya manunuza ya mambo ya serikali, na hili njia pekee ya kutatua ni kuweka udhibiti wa matumizi ya serikali kama Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* alivyopendekeza ili kuokoa matumizi ya serikali ambayo sio halali.

Mhe. Spika, eneo la nne ambalo nataka nichangie matumizi yasiyofuata sheria, Mwenyekiti wa *PAC* ametwambia hapa kwamba bilioni 16.3 zinatumika kwa matumizi mbali mbali ya serikali, lakini bilioni 25 tu ndizo ambazo zinatumika kwa njia halali. Na hii maana yake nini? Samahani asilimia 25 ndio matumizi halali hiyo maana yake nini? Bilioni 16.3 maana yake ni bilioni 4.1 ndio serikali inatumia kihalali, kwa maana ya kufuata sheria za manunuzi, sheria za fedha. Na asilimia 75 ni sawa sawa na bilioni 12.2 hutumika kwa njia isoyokuwa halali.

Mhe. Spika, serikali ikisikia hatua hiyo ikiwa robo ya matumizi ndio halali, robo tatu ya matumizi ya serikali ni matumizi ya wizi. Leo Mhe. Jussa jana anatuuila hapa ni kwa nini mapato yanaongezeka hatuendi mbele, hili ndio jibu lake kwamba yanaongezeka Wizara ya Fedha wananaambia mapato lakini matumizi yake sio halali.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe na wananchi kwa ujumla kwamba kwa nini mapato yanaongezeka kufikia bilioni 30 kwa mwezi, lakini jibu lake ni kwamba matumizi yanayotumika ni robo tatu ya matumizi yetu sio matumizi halali. Kwa maana manunuzi yanayotumika ni manunuzi ambayo watu wanajinufaisha na ndani ya mifuko yao.

Mhe. Spika, hoja ya tano ambayo nataka nichangie ni ukaguzi maalum wa viinua mgongo. Ili viinua mgongo vikamiliye Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* ametwambia lazima taasisi tatu zihusike. Lazima kuwe na muajiri, Afisa Muajiri lazima ahusike na kwa sababu alikuwa mfanyakazi husika, kuwe na ukaguzi wa Ofisi ya *CAG* na kuwe na ushiriki wa Idara ya Hazina kwa maana ya Afisa Muhasibu Mkuu wa Serikali. Sasa ni kwa nini wizi hutokezea? Wakati wote hawa watu watatu ndio watu wenye dhamana ya kumlipa kiinua mgongo mwajiri husika. Kwa nini wizi unatokezea?

Hili naomba Mhe. Mwenyekiti wa *PAC* uje unijibu ni kwa nini wataalamu hawa hufanya kazi ipasavyo lakini bado wizi unatokezea. Ni jibu ambalo naomba Mhe. Mwenyekiti wa *PAC* uje unisaidie. Lakini kwenye *sampling* ambayo imefanywa ya *ma-file* 65 imegundulikana kwamba milioni 131.7 milioni zimetafunwa tofauti na utaratibu wa sheria. Sasa hawa ni wafanyakazi 65, Ofisi ya Muhasibu Mkuu wa Serikali itwambie kwa mwezi wafanyakazi wangapi au kwa mwaka wanastaifu ikiwa wafanyakazi 65 wamegharimu gharama za serikali, wametia hasara milioni 31 je, wafanyakazi 100 watagharamu shilingi ngapi kwa mwaka pale wanapostaafu.

Mhe. Spika, nina mfano mzuri amba Mhe. Mwenyekiti ametuonesha ni suala zima la wizara mbili tofauti. Wizara ya Miundombinu *page* ya 11, wafanyakazi watano tu wameongezewa milioni 22.4 ilikuwa walipwe milioni 31, lakini wamelipwa milioniu 53 watu watano tu. Serikali imeibiwa milioni 22.4 kwa watu watano Wizara ya Miundombinu. Lakini wizara hiyo hiyo watu tisa walipaswa walipwe milioni 58.3 wamelipwa milioni 106, wameongezewa milioni 48.6 kwa watu tisa. Sasa watu 14 wa wizara moja maana yake wametuibia milioni 71, watu 14 watu mia 100 wa serikali nzima wanaidai serikali milioni ngapi?

Mhe. Spika, nilipoangalia walijotajwa kwenye wizi huu wa viinua mgongo ni wale wale amba Kamati ya Uchunguzi ya Kamati Teule ikiongozwa na Mhe. Hamza na Mhe. Omar Ali Shehe mara tofauti walipewa adhabu kama hii wakahamishwa Wizara ya Miundombinu, hatimae serikali hii hii ikawarejesha kwa mlango wa nyuma. Wafanye nini humu wametajwa bwana Ali Hassan, Kamati Teule sisi huyu alifikuzwa miundombinu, huyu huyu akarejeshwa tena hatimae amefanya yale yale.

Sambamba na yule ambaye miundombinu Kamati Teule tulimfukuza sitaki nimtaje ndiye aliyepewa *Coordinator* wa Mradi wa *ZUSP*. Yule yule ambaye aligharimu mabilioni ya pesa Kamati Teule ndiye serikali hii hii imemteua kumpa *Coordinator* wa Mradi wa *ZUSP*, mnatarajia nini Mhe. Spika.

Kwa hivyo, serikali hii Mhe. Spika nataka kusema kwamba ni serikali ambayo inalinda mafisadi kwa makusudi, jambo ambalo kwa kweli mimi sipendi kusema hivyo, haiwezekani kwamba Kamati tatu zimemsema huyu ni mkorofu halafu mnamatuea kumpa mradi wa mabilioni ya pesa mnakusudia nini. Kwa hiyo, Mhe. Spika na niwaambie kabisa kwamba ukaguzi wa mishahara hewa hasa Wizara ya Elimu Mhe. Mwenyekiti wa *PAC* amesema hapa kwamba 1.8 bilioni zinapotea kila mwezi serikalini kwa mishahara hewa.

Mhe. Spika, mishahara hii inaongoza Wizara ya Elimu, jana Waziri wa Fedha anatwambia Wizara ya Elimu hiyo hiyo inapoteza mabilioni ya pesa za madeski (vikilio), Wizara ya Elimu hiyo hiyo ndio inayoongoza kwa mishahara hewa ya walimu. Kwa kweli na nina hakika Mhe. Spika, Mhe. Ali Juma Shamuhuna waziri haya hayajui.

Kwa hivyo, Mhe. Mshimba anasema hapa kwamba mtu mmoja huyo huyo ndio amekuwa waziri, mtu mmoja huyo huyo ndio amekuwa Rais, mtu mmoja mmoja huyo ndio amekuwa Mahakama, hatuwezi kwenda katika utaratibu huu. Kwa hiyo, Mhe. Spika na niwaambie kabisa Waheshimiwa Wajumbe adhabu ambayo imetolewa na serikali hii Muhasibu aliyekuwa Wizara ya Elimu naapa kwa dini ya Mungu amehamishiwa wizara nyengine. Ni aibu Muhasibu anaharibu 1.8 bilioni za serikali adhabu yake anahamishiwa wizara nyengine aende akaharibu kwengine, ni aibu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, na ndio maana ripoti ya ukaguzi yakinifu ya mishahara hewa serikali wameikalia, na Mhe. Mwanasheria Mkuu nikuombe sana hoja ilipokujia mwezi wa Januari ultwambia serikali wataleta ripoti hiyo Barazani, nikuombe sana utuletee ripoti ile Barazani. Kazi yako wewe ni kulinda sheria, sheria inapovunjwa wewe utetee kulinda sheria. Kwa hiyo, haiwezekani kwamba wananchi wanalamika na niwaambie wenzangu Wizara ya Fedha inatoa fedha kila mwezi wala mawizara wasiisingizie kwamba ceiling ndogo, fedha wanapewa wanatafuna. Na mimi nitakuwa wakili mzuri kwa Wizara ya Fedha kwamba Wizara ya Fedha wanatoa fedha kila mwezi kwa mujibu wa uwezo wetu, lakini mawizara wanatafuna fedha.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, niwaombe wenzangu kwamba tumwambie Mhe. Shamuhuna kwa heshima kubwa bajeti hii ajitayariske kuja na majibu sahihi juu ya fedha ambazo zinatafunwa Wizara ya Elimu. Hatuwezi kulinda fedha kutafutwa huku tukiacha wananchi wakihangaika huku serikali ikitukanwa kumbe wanaotafuta fedha wanajuulikana.

Mhe. Spika, baada ya hoja zangu hizo naunga mkono ripoti hii na kuunga mkono Mhe. Waziri wa Fedha kumwambia kwamba umefundika tandu watakumaliza, nakushukuru sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuturuzuku neema zake tukawa hai na tukaendelea na shughuli zetu humu ndani tukiwa wazima, *Alhamdulilah*.

Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hoja hii ya kamati ya Hesabu za Serikali *PAC* pamoja na ripoti ya Utekelezaji ya mwaka uliopita ya ripoti kama hii iliyotolewa na Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Spika, kusema kweli muda hautoshi kuchanganua hoja nyngi ambazo zimo katika ripoti hii, lakini nianze kwa kusema kwamba utaratibu uliotumika leo nadhani si utaratibu sahihi Mhe. Spika. Asubuhi nilisimama kuzungumzia kuhusu kusomewa hotuba ya Mhe. Waziri wakati sisi hatuna nakala hiyo, tumepatiwa jioni. Lakini jioni nayo ripoti hii imeeleza muhtasari sana na ikasema mchanganuo wa hoja nyngi ambazo zimo katika kabrasha hili Mhe. Spika umo katika matrices ambayo haikuweza kusomwa hilo naweza kulielewa, lakini hata wajumbe hatukupewa kopi tunaambiwa itawekwa Maktaba anayetaka akasome.

Mhe. Spika, sasa tukimaliza mjadala huu utatuhoji hapa walioridhia, tutaridhia nini *matrix* zinawekwa Maktaba, inataka tutosheke, turidhike ndio turidhie hapa Mhe. Spika. Sasa hili mimi nasema tuna tatizo halioneshi umakini wa serikali. Mimi nilipata bahati muda mfupi kukaa Bungeni kule na hapa hapa Barazani tumeshaletewa makabrasha yenyе viambatanisho, kurasa nyngi sana. Kwa nini katika suala kubwa ambalo ndio kiini cha kuwepo Baraza kama hili katika nchi yoyote la kusimamia na kuchunga fedha za walipa kodi, kwenye ripoti kama hii, unaambiwa kuwa imewekwa maktaba, tunatakiwa tukajisomee. Tukajisomee saa ngapi, hili mimi nasikitika nalo sana. Ninavyotafsiri mimi ni aina nyengine ya kutufumba macho juu ya Baraza, ili tusiweze kuichangia ipasavyo na kubainisha uchafu uliokuwepo serikalini.

Mhe. Spika, nikizitizama hizi mimi niseme leo kidogo kaka angu Mhe. Waziri wa Fedha kani-*disappoint*, naam, tafauti na jana. Jana nilimpongeza sana. Ikiwa ni watendaji wake basi wamemuangusha sana.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 4 hadi wa 5 wa taarifa yake alipokuwa akizungumzia kuchukuwa hatua za kinidhamu kwa watendaji waliohusika na ukiukwaji wa taratibu wa matumizi ya fedha za umma Mhe. Waziri ametwambia kwamba zaidi kagundua kwamba ni kutokuelewa, kwa hivyo atatoa elimu. Atachukuwa hatua za kiutawala kuliko hatua za kinidhamu na kisheria.

Sasa Mhe. Spika, hili mimi limenisikitisha sana, tulioptia angalau a,b,c ya sheria tunajua kwamba tunaambiwa kama hakuna adhabu, hakua motisha ya watu kufata sheria. Watu watashawishika kufata sheria ikiwa wanajua ukikiuka sheria kuna adhabu. Lakini serikali leo inatwambia kwamba watu hawaelew tu mambo haya wizi wa mabilioni, kwa sababu kunataka kutolewa elimu, lakini si kwa sababu kuna sababu ya kuchukuwa ya hatua za kinidhamu na za kisheria.

Ndio maana Mhe. Spika, hatusongi mbele. Leo kuna kijana kaandika katika mitando ya kijamii baada ya kufanya mjadala wetu wa asubuhi wa Baraza la Wawakilishi. Akasema, "Baraza la Wawakilishi linaendeshwa kirafiki zaidi" kaandika maneno hayo tu na watu wetu Mhe. Spika, leo wanalinganisha wanapoonwa uwajibikaji unaofanywa na Bunge dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na uwajibishaji wetu katika Baraza la Wawakilishi. Tunachekeana na hapa na kuwa wakali dakika moja mbili, na mwisho inakuwa hadithi ya funika kombe Mwanaharamu apite.

Mhe. Spika, nitakuomba univumilie kwa sababu kama nilivyosema kwamba masuala haya yako mengi na najaribu sana kuyafupisha. Mimi nitaomba nijikite katika maeneo matatu kama uliovyosema muda hautoshi sana.

La kwanza ambalo nataka nzungumzie ni matumizi ya fedha za umma yasiyofata utaratibu wa sheria za fedha ya matumizi za mwaka 2005. Mhe. Spika, katika hili kuna mambo mengi ambayo yanahitaji maelezo na jana nilipokuwa namshukuru Mhe. Waziri wa Fedha kwa ile *summary* ambayo ametupa katika hotuba yake ya majamuisho, kuna baadhi ya mambo katwambia Mhe. Spika. Mimi nadhani tukioanisha ripoti hii, sasa tunahitaji maelezo na mimi nimwambie Mhe. Waziri wa Fedha katuwezesha sana Wajumbe jana kama alivyotwambia anatupa *tips*, tutazitumia vilivyo katika bajeti inayokuja baada ya miezi miwili, tukijaaliawa Mhe. Spika.

Kwa mfano nikisoma ripoti hii ya *PAC* ikinukuu ripoti ya *CAG* inataka katika eneo hilo la matumizi linalofanya utaratibu Mhe. Spika, kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwenye safari za Viongozi kuna matumizi ambayo yameshinda kutoa maelezo ya shilingi mia mbili tisini tano milioni laki tisa sabini na saba elfu, kwenye safari za viongozi.

Jana Mhe. Waziri katwambia katika fedha ambazo anatoa kila mwezi ni wastani wa shilingi milioni mia tano kwa safari za viongozi za ndani tu. Nimefanya hesabu za haraka haraka hesabu yake sahihi milioni mia tano kwa mwezi maana yake kwa mwaka ni shilingi bilioni sita. Mhe. Spika, napata wasi wasi kama hivi ndivyo vinavyotumiwa fedha za wananchi na kasema jana kwamba ni Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais zaidi sawa. Mimi nimuombe ajiandae mara nyingi suala likiulizwa huwa linapigwa chenga katika bajeti, aje atutolee mchanganuo wa kila mmoja wao anatumia kiasi gani wa safari za ndani na safari za nje.

Mhe. Spika, katwambia pia safari za nje zinatumia mia saba thalathini na mbili milioni, kwa wastani kwa mwezi alivyotwambia jana. Hiyo maana yake kwa mwaka ni bilioni nane nukta saba nane nne kwa safari za nje. Lakini pia nimepata mshtuko kuambiwa kwamba yale waliomwambia jana kweli watendaji wake ni sahihi kwamba, kwa mwezi kwa wagonjwa walioko nje tunatumia milioni mia tatu thalathini na tano. Nimefanya hesabu Mhe. Spika, kwa mwaka maana yake ni bilioni nne nukta ziro mbili. Kweli fedha hizi zitalipwa katika kuhudumia wagonjwa walioko nje?

MHe. Spika, baadae wizara itakuja kutujibu hapa ikifika bajeti. Tutakuja kulinganisha majibu tuliyopewa jana na Waziri wa Fedha na majibu ya wizara moja moja, hapatatosha hapa katika Kikao cha Bajeti Mhe. Spika. (*Makofi*)

Jengine Mhe. Spika, katika eneo hilo hilo kuna eneo moja ambalo halikutajwa humu na mimi niliwahi kulizungumza mara moja na nikanukuu mpaka kifungu cha sheria, mpaka leo limekuwa donda ndugu. Sheria ya *Public finance* inamtaka Waziri wa Fedha kutuletea hapa mchanganuo wa fedha zote za matumizi katika miradi ya maendeleo, sheria iko wazi kabisa. Aliwahi kunukuu mpaka kifungu humu ndani.

Sasa leo tunapopokea ripoti ya Ulaguzi Yakinifu kuna maswali mengi, lakini ndani ya kupokea ripoti za kamati tafauti tangu tumeanza hapa humu tumetaja mradi wa *Terminal II* na maoza oza yake, tumezungumza mradi wa *ZUSP* na maoza oza yake mpaka jana Waziri wa Fedha katukubalia hali ilivyo. Kila mradi mkubwa unaozungumzwa humu umezungumzwa mradi wa *E-government* humu, serikali imetoa majibu Wajumbe wengi hawakuridhika kwa sababu hakuna majibu ya kutosheleza na kila kwenye mradi mkubwa

Mhe. Spika, sasa najiuliza huku ndiko kwenye mabilioni yanayotafunwa. Sasa najiuliza kwa nini serikali haitaki kutekeleza Sheria ya Fedha kwa kutuletea mchanganuo Baraza linapoleta mradi wa maendeleo kama Sheria ya

Fedha ya Umma inavyotaka, hilo jengine. Nasema na nasema tusiishie kupiga ndaro Barazani tu wananchi wanataka kuona hatua ili waiamini serikali yao kweli kwamba iko makini katika kuchunga pesa zao, *otherwise* kuna wananchi wanatwambia baadhi yenu pale mnatufanyia usanii tu. Wanatwambia hivi hivi maelezo mengi lakini hakuna hatua inayochukuliwa na ndio maana *business as usual*. Na katika hili Mhe. Spika, nitoe mfano wamesema wezangu hapa kwamba moja katika wizara amabayo imetajwa sana katika matumizi haya mabaya Wizara ya Elimu hasa katika suala la mishahara na mambo mengine.

Leo aliyejekuwa muhasibu baada ya kumchukulia hatua unamuhamishia Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kesho toka Wizara ya Kilimo kunafichwa nini Mhe. Spika, na tunalindwa na nani.

Kuna jengine humu humu ndani imetajwa kadhia nyengine na katajwa hasa muhusika katika Chuo cha Utawala wa Umma kwamba ndugu Hafidh Ali Hassan mshika fedha alikuwa anakusanya fedha za ada anawapa risiti bandia zake mwenyewe mfukoni. Kakusanya sitini na moja milioni laki tano sitini na tano elfu baada ya kubainika na kubanwa na chuo ndio tunaambiwa kuwa kazirejesha katika *account*. Kumbe alikuwa anazo kazirejesha hamsini na tano milioni na elfu tisini na tano.

Sasa Mhe. Spika, baada ya yote ripoti inatwambia kwamba kakabidhiwa mamlaka ya Chuo Kikuu na hoja iliyotolewa hapa kwamba hizi ripoti hazimiliki kama ushahidi kunangojewa nini, tena mtu kakamatwa mpaka kafika kurejesha fedha kwamba kakiri kama alizichukuwa halafu unaambiwa kuwa taratibu zinaendelea. Wananchi wanapoteza imani na serikali kwa sababu wanaona kwamba haiko *serious*, inalinda watu wanaohusika na matumizi mabaya ya fedha.

Mhe. Spika, katika hayo hayo kinachosikitisha zaidi leo ni kwamba hata fedha zilizotolewa kwa mayatima maafa *MV. Spice Islanders* zimetafutnwa nimesoma humu ndani ingawa mimi sihusiki na ripoti hii. Ukisoma ukurasa wa 21, 22 inazungumzia kadhia hii kwamba tarehe ni moja kwa matumizi yaliyokuwa yamelipwa kwa muda wa miezi mitatu, lakini tarehe ya malipo inaonesha inaonesha tarehe moja tu *true*.

Hapa mimi kiogdo kamati nitaomba akija ndugu yangu Shekhe Omar Yussuf Mzee, aje anisaidie kwa nini wamefunika kombe katiki hili wakaridhika, wakasema huko mbele mambo haya yasijirejee sijui kwa nini haya ndio *business as usual*. Sasa kama inafanya na baadhi ya watu na kutaka kuyafunika funika Mhe. Spika, tunarudi pale pale mambo haya hayataisha.

Hapo hapo Mhe. Spika, nitoe mfano mwengine katika masuala haya ya matumizi ukurasa wa 34 mradi wa *MACEMP*, mia moja thalathini na sita milioni katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika mradi wa *MACEMP* zimetumika visivyo, bado tunaambiwa kwamba wamepewa agizo kwamba wajirekebishe kwa siku za mbele, hizi thalathini na sita milioni zilizotumika humu na nyengine na nyengine imeshakuja mifano mingi hapa mabilioni Mhe. Omar Yussuf Mzee katwambia hapa katika *summary* yake kwamba anakisia bilioni kumi na sita zimetumika bila ya kufata taratibu za serikali katika masuala ya serikali. katika masuala ya matumizi ya fedha. (*Makofsi*)

Sasa Mhe. Spika, katika hali kama hiyo tutegemee kweli tutaweza kuwashudumia wananchi tuisidanganyane, Mhe. Spika, leo hata taasisi ambayo tunaitegemea, zingekuwa ni kioo katika maadili taasisi inayotoa elimu Chuo Kikuu *SUZA* Makamu Mkuu wa Chuo ananunuliwa gari sabini na nne milioni thamanini na nne elfu hakufata taratibu za manunu. Tunalindana tu, mna matumizi Mhe. Spika, kwenye kikosi cha Valantia wamelipwa sijui mia mbili hamsini na mbili milioni laki sita ishirini na tano elfu, wametakiwa watoe vielelezo, hakuna vielelezo.

Mhe. Spika, zaidi najiuliza suala jengine katika haya matumizi ambayo hayafati taratibu. Kwamba kumekuwa na utaratibu na naushuhudia leo mwaka wa tatu namaliza Mhe. Spika, katika Baraza lako hili kila mwaka inajirudia. Naishukuru kuna baadhi ya maeneo naipongeza *PAC* imekataa kwamba kamati inapokwenda kukagua hakuna vielelezo lakini ikifika *PAC* vielelezo vinakuwa vimepatikana, vilikuwa havipo siku ya ukaguzi. Sheria imetaka vielelezo vипатикane wakati wa ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. (*Makofsi*)

Leo Mhe. Spika, katika hilo pana kuhoji matumizi ya shilingi mia nne arubaini na tatu milioni katika Shirika la Magazeti, *ZRB* Bodi ya Mapato yenyewe kuna matumizi ya milioni mia tisa na kumi na tano laki saba thamanini na nne elfu mia saba kumi na mbili hazikufata taratibu na kama nilivyosema mwanzo safari za viongozi vile vile mia mbili na sitini na tano.

Sasa katika hali kama hii Mhe. Spika, tutawezaje kuleta ufanisi ikiwa hatuchukuwi hatua. Tunasema jawabu letu ni kwamba watu hawana elimu tu tuwaelimishe lakini tusielekeze katika kuchukuwa hatua za kinidhamu na kisheria.

Mhe. Spika, kuna suala la mchanganuo wa thamani *asset* nimeshituka mimi katika eneo hili katika ripoti za mashirika. Hoteli ya bwawani kuna *asset* tu zenyet thamani ya bilioni sita mia moja thalathini na saba milioni laki mbili sitini na sita elfu hazina vielelezo hazikuwekwa katika rikodi ipasavyo, zinaweza zikapotea hizi hakuna atakaekuwa na ushahidi wowote kwa sababu hakuna vielelezo.

Shirika la Magezi linasema kuwa kuna mia nne arubaini na tano milioni, Chuo cha Utalii kuna bilioni moja mia tatu na mbili milioni thamani ya *asset* hazina rikodi. Chuo cha Uandishi wa Habari mia moja kumi na tisa milioni laki nne sitini elfu hazina maelezo. Sasa haya kusema ukweli yanakinaisha, yanatapisha kabisa kwa jinsi ambavyo kila mwaka yanaendelea hakuna hatua ambazo zinachukuliwa.

Mhe. Spika, nihitimishe maelezo yangu kwa kusema kwamba hali hii tusipochukuwa hatua itaendelea huku mwananchi mnyonge masikini wa nchi hii ataendelea kuambiwa achangie elimu, akienda hospitali hakuna dawa, maji kupatikana kwa zamu, mtihani. Lakini huku fedha zinatafunwa namna kama hiyo, hakuna maelezo za msingi juu ya kuachiwa watu hawa kuendelea kutafuna fedha namna hii.

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Ismail Jussa Iadhu: Mhe. Spika, zinanitosha kabisa Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika hili mimi masema jana Mhe. Waziri wa Fedha alitwambia kwamba tumsaidia sana Baraza hili katika suala la kuziba mianya ya ukusanyaji wa mapato. Lakini nadhani kwenye matumizi bado tuna tatizo kubwa sana na hili si kama Baraza halijafanya kazi yake, ushahidi wa *hansard* za miaka mitano hii zingetosha kuonesha mambo mengi yaliyokuja kuthibitika. Tulieleza humu ndani serikali ikakinga kifua kweli kweli, mawaziri wakali wanatetea watendaji wao baadae yamethibitika haya.

Sasa hili si kama Baraza halijasaidia serikali haikutaka kusaidiwa. Kwa hiyo, mimi nina tatizo moja ni ama Mawaziri nao ni sehemu ya utafunaji huu Mhe. Spika, au wanajua wenyewe sababu za kuwakingia watendaji wao. Kwa sababu haya mambo yameibuliwa humu ndani.

Kwa hiyo, nasema siri ya haya iko kwa serikali yenyewe kujikita katika suala la kuchunga matumizi holela na kuheshimu michango inayotolewa humu ndani, kwamba lengo letu ni kusaidia serikali si kukomoa ni kumsaidia mwananchi mnyonge, masikini ambaye anaona huduma za msingi hazimfikii na msingi wa kulipa kodi katika nchi yoyote.

Mhe. Spika, tunalipa kodi wananchi kwa sababu tupewe huduma ya serikali. Sasa huduma zinapokuwa hazitolewi kwa mwananchi si elimu, si afya, si maji kila kitu kina matatizo lakini huku mabilioni kama haya yanatafunwa tu na watu Mhe. Spika, hii hali haipendezi hata kidogo.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa ni suala la ardhi, sikuridhika hata kidogo na nimeligusa hapa kwa sababu katika ripoti ya kamati limegusiwa hili katika ukaguzi yakinifu, kwamba bado kuna matatizo ya msingi katika ardhi na jinsi wakubwa wanavyotumia nafasi zao kujilimbikizia ardhi. Yale majibu ya mkato leo ya Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi nimwambie kabisa. Majibu yale hayatakuja kunifanya mimi hata kama Mjumbe wa Kamati yake nikaja nikaidhinisha bajeti yake hapa, alitwambia humu ndani kwamba kuna wakubwa wamechukua ekari zaidi ya tano zile achilia mbali alizonambia tano leo, nataka aje atupe maelezo ya kina wakati ukifika.

Mhe. Spika, suala la kufanya utumishi wa umma kupewa dhamana ya uongozi ikawa si kutumikia watu badala yake ni kujinufaisha wewe, familia yako na marafiki zako lazima tuukomeshe katika nchi hii. Kama hatukukomesha hilo maisha tutakuwa tunakuja kuzungumza hapa upotevu wa mali, lakini hakuna litakalokuwa.

Kwa hivyo, nasema tena nashukuru, naipongeza kamati kwa kuleta masuala haya yatatusaidia sana. Hii ni nyezo na silaha muhimu sana Mhe. Spika wakati wa bajeti tukijaaliwa. Nataka niambilie serikali yale mambo kwamba wao walikuwa wanaimba wimbo kila siku hakuna *business as usual* lakini tunachokiona ni *business as usual*. Sisi kama Baraza la Wawakilishi la wananchi wa Zanzibar hatutolikubali hata siku moja.

Mhe. Spika, nakushukuru sana ahsante. (*Makofî*)

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia machache na yatakuwa ni machache tu. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa utekelezaji wake wa mapendekezo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2013/2014.

Pia nimpongeze Mwenyekiti wangu wa Kamati ya *PAC* kwa ripoti yetu ya mwaka 2014/2015 kwa muhtasari aliyoutoa. Mwisho nimpongeze *CAG* na nimpe pole sana, niseme kwamba nitachangia machache na nikienda moja kwa moja nifafanue kwa zile nchi zenyé demokrasia pana na zinazoheshimu utawala wa sheria.

Serikali inakuwa na jukumu la kupanga mipango na bajeti zake ikisha Bunge likachukua jukumu la kuidhinisha mipango na bajeti. Bajeti hizo baada ya serikali kufanya matumizi Bunge linapata fursa nyengine ya kupitia, kufuutilia na kuchunguza kama matumizi hayo yamefanyika kama yalivyoidhinishwa au laa, hapa ndipo tunapoona kama ua jibikaji kwa mihimili yote miwili ya dola Serikali na Bunge umetekelizwa ipasavyo au laa.

Wakati bajeti inapotekelezwa na baada ya kutekelezwa hesabu zote za serikali zitakaguliwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuzingatia matakwa ya kifungu Nam.143 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kwa upande wa Tanzania. Kwa upande wa Zanzibar hufanya kwa mujibu wa kifungu cha 112 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Spika, mambo yanayobainika katika ukaguzi yanajumuisha pamoja na mambo mengine kuhusu matumizi halisi ya fedha za umma yanayolingana na kitu chenyewe kilichonunuliwa, *value for money* na ni kwa jinsi gani sheria za matumizi ya fedha hizo yamezingatiwa. Ni kweli kwamba tumeona kuwa kuna mambo au matumizi ya fedha hizo hazikutumiwa.

Mhe. Spika, vile vile kwa uzoefu ambao tumeona kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kazi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni kazi moja ngumu, yenye lawama, yenye uhasama, kuogopwa na kadhalika. Ni kazi ambayo haikupi nafasi ya kutengeneza marafiki, inakulazimu kuishi kwa wasi wasi wa kudhuriwa. Yote haya yanababishwa na ukweli kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kueleza wajibu wake ipasavyo kugusa maslahi ya watu, kugundua makosa ya uandishi wa vitabu au kugundua wizi na ubadhirifu na raslimali za taifa. Hali ambayo watendaji wangependa isifahamike.

Mhe. Spika, uzoefu ni kwamba Bunge au Baraza la Wawakilishi kuptia kamati zake za kudumu lina nafasi kubwa sana katika kuchangia kuhusu juu ya uwajibikaji na utawala bora. Lakini maafisa wengi kutokjua kwa undani majukumu yao inapohusi usimamizi wa raslimali za umma.

Pia, viongozi wa kisiasa kwa makosa kuamini kuwa yanapokuja mambo yanayohusu fedha na raslimali za umma kuwa siyo jukumu lao. Mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu na uandishi wa vitabu vyá hesabu na ipo hasa kwenye Serikali za Mitaa. Na hayo ni mambo ambayo tumeyaona kwamba kuna udhaifu huo.

Pia mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu na uandishi wa vitabu vyá hesabu dhaifu hasa kwenye Serikali za Mitaa, ndiyo hasa ni jambo ambalo ni sugu ingawaje sasa hivi kidogo kuna mambo ambayo yamerekebishwa.

Usimamizi dhaifu wa sheria, kanuni na taratibu zinazohusu uwajibikaji wa utawala bora hapa nchini. Viongozi kuijingiza kwenye mambo au shughuli zinazoleta migongano wa kimaslahi (*conflict of interest*), utaratibu wa uteuzi wa viongozi wa juu ambao unasababisha mgongano, utengaji kama Wabunge, Wawakilishi kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi, nayo pia hili ni tatizo.

Baada ya hayo niseme kwamba baada ya haya mengi ambayo nimeyaona, lakini vile vile niseme kwamba kuna mambo muhimu ambayo yanatakiwa yazingatiwe na nishukuru kwamba haya ni mambo muhimu ambayo juzi

tu nilikushukuru Mhe. Spika, uliniteuwa nikenda kwenye mkutano wa 22 wa Wahasibu uliofanyika pale Dar es Salaam.

Kwa kweli Mhe. Spika, nimesoma mengi na niseme kwamba ni mambo ambayo muhimu ya kuzingatia ambapo kwenye mkutano ule ambao hufanyika kila mwaka, ikiwa Zanzibar ni moja katika wanachama. Na dheme yake ilikuwa ni *Strengthening Public Finance Management For Social Economic Development*. Kwa hivyo hili ni jambo ambalo ni la kusimamia maendeleo ya kiuchumi katika jamii.

Mhe. Spika, kwa kweli kule kulikuwa na mada nyingi ambazo zimezungumzwa ambayo moja inasema, "*The support needle to enforce the transparent and effective management of public procurement*" ambao unasema msaada unaohitajika kutekeleza kuimarisha uwazi na ufanisi katika kufanya manunuzi ya umma. Hiyo ni moja ambayo ni mada kuu ambayo zimezungumzwa katika mkutano ule wa 22 ambao Zanzibar pia ni mwanachama wa jumuiya zile. (*Makofî*)

Kwa kweli pale palikuwa ni mkutano wa 22 ambao ni unajumuisha *Eastern Southern African Development* ambayo imezungumzia mambo hayo ya kuhusu namna ya bajeti zinavyofanywa na usimamizi na mambo mbali mbali, utayarishaji wa *procurement system*, mpango wa manunuzi ya umma kupitia *public procurement system* ambayo inakufanya kwamba ni *u-make sure kwamba economical, efficient and effective*, uhakishe kwamba manunuzi unayafanya yawe ya kiuchumi. Maana ya kusema hivyo ni kwamba yowe zaidi yanatizama hayatumii pesa nyingi na yowe ya kiufanisi, yenyé kuleta athari ya muonekano.

Mhe. Spika, kwa kweli tujifunze mengi na mkutano huu ulikuwa wa Wahasibu Wakuu wa Zanzibar, walikuwa wameshiriki mkutano huu. Kwa kweli sasa hivi tuijandae na kwamba kila jambo katika mambo ya hesabu Wahasibu wetu watakuwa haya mambo wanayalewa vizuri. (*Makofî*)

Vile vile, kulikuja suala la kwamba *what do elected officials want to serve citizens*, viongozi waliochaguliwa wanataka na wanataka nini. Maelezo ya kuchanganua wananchi wanataka maendeleo, uwajibikaji na usimamizi mzuri wa fedha. Pia, hii *internal auditor*. Kwa kweli vile vile kulikuwa na *internal auditor* ambayo nayo pia ilikuwa ni mada kubwa. *Internal Auditor for Better Public Performance Management Rules*, ukaguzi wa ndani kwa ajili ya kuboresha mazingira mazuri na kudhibiti kasoro ambazo zinaweza kujitokeza. (*Makofî*)

Halkadhalika, kulizungumziwa kuhusu *full audit institution, invested public confidence*, taasisi kuu za ukaguzi kuimarisha imani ya umma. Kwa hivyo vile kusema kweli ni kazi ambayo ni muhimu na *CAG* anafanya kama ni wajibu wake katika Katiba. Watu wengi wanaamini wanapotoa ripoti zao, wananchi wanaamini kwamba fedha zao zinatumika ipasavyo.

Vile vile, ikaonekana kwamba sekta za umma ni kwamba ilionekana kuwa sekta za umma ni kiwanja chenye mbolea ya udanganyifu na rushwa ni tofauti na sekta za binafsi. (*Makofî*)

Mhe. Spika, kwa hivyo, baada ya hayo niseme kwamba ni nafasi yangu kusema haya machache kwa sababu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na ripoti ya Kamati ya *PAC* imesema mengi, na kwa sababu na mimi ni mmoja ya wajumbe wa kamati hii. Kwa hivyo sina mengi ya kusema isipokuwa nilikuwa nioneshe tu namna gani hali ya fedha na upotevu wa pesa na kutokutumika ipasavyo kwa kufuata zile sheria za manunuzi pamoja na hii mitaji ya umma.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kuunga mkono ripoti hii kwa mujibu wa wananchi wangu wa Jimbo la Amani, naunga mkono ripoti asilimia mia kwa mia.

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Fatma Mbarouk Said. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Subeit Khamis Faki na baada ya hapo tumsikilize Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, ninakushukuru sana kunipa fursa na mimi kuchangia ripoti hii ya *PAC* ambayo kuwa ni ripoti ya Kamati ya Kuchunguza Mahesabu ya Serikali.

Mhe. Spika, kwanza ninapenda niwapongeze sana wajumbe wa kamati hii kwa kazi nzuri ambayo wameifanya, wamefanya wajibu wao kama wanavyofanya, wamefanya wajibu wao kueleza kwa uwazi kabisa na bila ya kigugumizi, kuonesha penye kasoro, kuelekeza Serikali, kuikosoa ambayo ni wajibu wetu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kufanya kazi hiyo.

Mhe. Spika, mimi nina masikitiko sana kwa sababu Baraza lako la Wawakilishi pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na yeye pia anafanya wajibu wake. Lakini masikitiko yangu mimi ni kwa Serikali.

Serikali bado haijataka kutimiza wajibu wake, kwa sababu kamati za Baraza la Wawakilishi zinafanya kazi kwa ajili ya kuchunguza na kuona kodi za wananchi zinatumwiwa ipasavyo. Kama hivyo ndivyo, mimi masikitiko yangu ni kwamba Serikali tunafanya kazi kikamilifu kila siku, lakini bado Serikali haijataka kutimiza wajibu wake.

Mhe. Spika, naona sisi tunakuwa tunakuja tukisema kama tunaoimba. Na kama ni kama tunaoimba siamini kama kuna mtendaji yeoyote wa Serikali ambaye atakuwa na wasi wasi na maelezo au ripoti zinazotolewa katika Baraza la Wawakilishi. Sisi tunakuwa kama tunaimba tu kwa sababu tunafanya kazi Serikali haitaki kuwajibika kwa kufanya kama inavyopaswa.

Mhe. Spika, kwa nini Serikali inawalinda watu ambaao wanafanya *forgesies* katika matumizi ya fedha za umma. Leo Mhe. Spika, ripoti imeeleza na si mara ya kwanza, kuna ripoti ambazo tumezungumza; kuna ripoti za Kamati Teule ngapi zimekuja zimesoma ripoti zake lakini utekelezaji unasuasua, sijui kwa nini. Hivyo kwa kweli tunajua fedha za umma kwa kamati hizi, halafu utekelezaji wake unakuwa hauonekani kwa nini Mhe. Spika.

Mhe. Spika, tumeelezwa hapa katika ripoti hii ya Kamati ya *PAC*, zimepotea fedha bilioni sita ambazo kuwa kwa mwezi mmoja zinapotea bilioni moja na milioni mia nane (1,800,000,000). Tukija humu Baraza la Wawakilishi tunafanya kazi, tunakopwa hatulipwi, tunafanya kazi za kamati hatulipwi kwa sababu fedha hazipo, kumbe fedha zinapatikana watu wanatia mifukoni mwao. Lakini leo Serikali kuwajibisha watu hawataki. (*Makofî*)

Mhe. Spika, tunafanya kazi, tumekuja hapa tumetolewa Pemba kuja kuitia Miswada, tumekuja kwa fedha za kukopa mpaka leo tumeshindwa kulipwa na Serikali fedha inatwambia kama kodi inakusanywa lakini leo malipo hayapatikani, watu fedha wanatia mifukoni mwao munawatizama tu hivi. (*Makofî*)

Mhe. Spika, hivi mpaka lini tutakuwa hapa tunapiga kelele lakini kuwajibisha. Serikali munalindana kwa nini. Hivi munawalinda watu ambaao kuwa ni wahujumu fedha za watu na kila siku huwa ninasema mimi hapa. Juzi tumepitisha Sheria ya Maadili ya Viongozi kwa ajili ya kuwajibisha wale ambao wanakiuka, wanaharibu fedha, wanafaja vitu vya watu. Tuna sheria tumepitisha juzi ya wahujumu uchumi hapa. Tunafanya kazi ya kuitish sheria nyingi na kuwajibika ni vitu mbali mbali. Tuna sheria nyingi nzuri Zanzibar lakini uwajibikaji haupo, kwa sababu bado Serikali haijawa tayari. Serikali haipo tayari kuwajibisha watu. (*Makofî*)

Mhe. Spika, tumeona hapa kamati imetueleza kama kuna mapato yanavuja, makusanyo yanavuja na ni ukweli yameelezwa. Kamati imetoa maelekezo yanavyovuja mapato. Kwa nini Serikali inakuwa kaidi kusimamia. Mshaambiwa fedha zinapotea kwenye mahoteli, kuna fedha nyengine zinavuja hazikusanywi vizuri na si mara ya kwanza leo kuja kusemwa humu Barazani. Lakini Serikali inakuwa sisi tunapiga muziki lakini wachezaji hamna. (*Makofî*)

Mhe. Spika, tunapata taabu kweli sisi na maisha hii tutakusanya bajeti, tutapitisha bajeti halafu bajeti yetu itakuwa ni hewa. Kwa sababu fedha za kuendeshea Serikali zipo lakini fedha hizo zinakusanya ndivyo sivyo na hizo zinazokusanya watu wanatafuna mifukoni mwao. Hivi Mhe. Spika, tunakwenda hivi mpaka lini. Maisha haya tusimamie, tusubiri wafadhili watusaidie baadae wafadhili hawajatusaidia bajeti haitekelezeki na wakati vianzio vya fedha viro na makusanyo yanakusanya, lakini Serikali haitaki kusikia. Inawalinda watu wezi. (*Makofî*)

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limezungumzwa na kamati, limezungumzwa suala la kuanza vyengine vya mapato. Na vianzio vya mapato kamati imeeleza kama jamani vianzio vya mapato, kuna uvuvi wa bahari kuu tusimamie, kuna maeneo huru tusimamie, imeeleza kuwa na bandari huru tusimamie. Lakini Serikali haitaki kufuata kila inaloiezwa.

Mhe. Spika, sisi tunafanya kazi kuisaidia Serikali lakini Serikali inayosaidiwa haitaki. Jamani tutapata kazi kweli kweli na tuna kazi kweli kweli. Waheshimiwa Baraza letu linakwenda kwa kusuasua. Juzi tumeona wenzetu kule Tanzania Bara, baada ya tatizo lile la *Escrow*, kuna watu wameshawajibishwa, ijapokuwa ni kidogo hawajawajibishwa wote lakini nusu tayari wamewajibika. Lakini sisi tupo tunalinda tu, basi fedha zitaendelea kuibiwa na kutafunwa na Serikali maisha tutakuwa tunakusanya hatuna tunachokifanya. Kwa sababu vile vianzio vya fedha zinazokusanya fedha zinavuja na hizo zisingevuja. Kwa nini hivi sasa watu wa

mishahara, kuna ripoti hapa tulitaka iletwe mpaka leo Serikali imeibana ripoti hawataki kuileta, kwa nini hailetwi.

Mhe. Spika, kuna ripoti ya mishahara hewa hailetwi. Kwa nini Serikali ina taabu kutuletea ripoti na ripoti hii kama imeshafanyiwa kazi na iletwe Barazani tuione, lakini Serikali imeibana hivi hivi. Kwa sababu kuna watu wanalindwa. Mhe. Spika, tutalindana hivi hivi mpaka lini. Basi mimi ninasema ukilinda sana na ukificha ubaya sana baadae unakuja juu.

Kwa sababu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tunampa kazi afanye, anafanya kazi anakuja na ripoti zake lakini zinatiwa mivunguni basi imekwisha, tukishakuja kusoma humu tukishapitisha basi. Tutakwenda hivi mpaka lini. Waheshimiwa tunapiga kelele tunazungumza, tunaelekeza lakini maelekezo yetu hayasikilizwi. (*Makofî*)

Mhe. Spika, kuna suala la magendo ya mafuta. Hili suala kamati nalo imelizungumza. Hivi basi Waheshimiwa Serikali inashindwa hata kudhibiti hayo magendo ya mafuta na wameshashindwa kuyadhibiti au kuna wakubwa wanafanya kazi. Kama munalindana hata magendo ya mafuta, magendo ya karafuu yamedhibitiwa *alihamdulillah* lakini magendo ya mafuta, hivi hamujui kama kuna mapato mengi ya Serikali yanavuja. Hayo makusanyo ya hizo fedha nyinyi hamutaki kodi ya hayo mafuta. Mafuta yale yanayopita mlango wa nyuma, kodi zake zinakwenda wapi, hazionekani.

Mhe. Spika, kwa hivyo Serikali tunaelekeza kwa faida ya wananchi pamoja na Serikali yenewe. Waheshimiwa ninawaomba sana na Serikali tunaiomba sana isikie vilio vyetu, tusije kupiga kelele humu tu, watendaji hawaogopi tena. Wameshajua sisi tunakuja Baraza la Wawakilishi tunapiga makelele tukishamaliza makelele yetu, wao wanatia fedha zao wanatumia. (*Makofî*)

Mhe. Spika, basi kama Serikali imeshakubali hivyo, haya pata mpatae, atakayepata agaiwe. Ndiyo achue mtu aktia afanye anavyotaka mwenyewe. Kwa sababu tunasema hatusikilizwi. Hebu Serikali na muwajibishe watu wawili. Kwanza huu uwajibishaji wa mtu kuondolewa hapa akapelekwa hapa, siyo uwajibikaji huo. Leo mtu kishafanya makosa anahamishiwa Wizara hii, anapelekwa Wizara hii, achukuliwa huku anapelekwa huku. Hivi ndiyo uwajibikaji huo. (*Makofî*)

Mhe. Spika, naomba sana na kuiomba sana Serikali iangalie ripoti hii na ifanyiwe kazi na tuone imefanyiwa kazi. Na zile ripoti ilizozificha Serikali tupewe zile ripoti ambazo kuwa ni za kuletwa hapa Barazani tupewe. (*Makofî*)

Mhe. Spika, baada ya hayo machache, mimi ninaunga mkono ripoti hii na naomba sana na Serikali ifanye wajibu wake. (*Makofî*)

Mhe. Spika: Ninakushukuru Mhe. Subeit Khamis Faki. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, ninakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikazungumza machache sana katika ripoti hii ya Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*.

Mhe. Spika, mimi kwanza ninataka nianze na masikitiko. Sisi wenyeviti tunatakiwa tuunge mkono hizi ripoti za kamati, kwa sababu sawa sawa na Mawaziri wanapofanya kazi katika ile *collective responsibility*, uwajibikaji wa pamoja. Sasa na sisi tunatakiwa tuwe na uwajibikaji wa pamoja. Lakini sitaki kumwambia Mwenyekiti mwenzangu kwamba ripoti yake nitaikataa. Lakini pamoja na umakini wake katika kazi, kama alivyosema Mhe. Makame Mshimba, kwamba leo Mhe. Waziri wa Fedha kamvunja moyo, lakini na mimi Mwenyekiti wangu kidogo kanivunja moyo. Kwa nini nikasema hivyo?

Mhe. Spika, haiwezekani sisi tukawa walalamikaji siku zote, wakati katiba ya Zanzibar imetupa nguvu. Leo tunakuja hapa sisi kazi yetu kulalamika tu, wananchi wanalamika, wawakilishi wanalamika na serikali inalamika, yaani tumekuwa kama tumechanganyikiwa kidogo. (*Makofî*)

Sasa Mhe. Spika, nataka niikamate katiba ya Zanzibar ambayo katiba hii ulinikabidhi wewe, na siku hiyo ulinikabidhi katiba ya Zanzibar na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na msahafu.

Mhe. Spika, maelekezo ya Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Dk. Abrahman Kinana, serikali ni lazima tuisimamie sisi wawakilishi wa CCM na tusimuonee haya mtu yejote mbadhirifu, mwizi na anayekiuka utaratibu. Hayo ni maelekezo ya Chama cha Mapinduzi na tusiwfumbie macho watu kwa kujificha ndani ya

bendera ya Chama cha Mapinduzi wakatafunu nchi halafu nchi inaangamia, wananchi wanapata tabu hawapati huduma bora. (*Makofi*)

Mhe. Spika, katiba ya Zanzibar kifungu cha 112, Mhe. Mwenyekiti mwenzangu wa kamati ya *PAC* inaonesha hukukisoma. Leo unalalamika serikali hajatuletea ripoti ya mishahara hewa, katiba hii hapa nakusomea. Kifungu cha 112 ibara ya 4 na 5 nakusomea hivyo tu, inasema hivi;

Kifungu cha 112 ibara 4:

"Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kila mtumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar aliyeruhusiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, atakuwa na haki ya kuchunguza vitabu nya kumbukumbu, hati za maelezo, taarifa na hati nyenginezo zote zinazohusika na hesabu za aina yoyote zinazotajwa katika kifungu cha 3 cha kifungu hiki.

Ibara ya 5:

"Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (3)(c) cha kifungu hiki baada ya kupokea taarifa hiyo, Rais atawaagiza watu wanaohusika waiwasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Baraza la Wawakilishi kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo, na itabidi aiwasilishe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kilipoanza kikao hicho, iwapo Rais hatachukua hatua za kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Baraza la Wawakilishi, basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi au Naibu Spika, ambaye ataiwasilisha taarifa hiyo kwenye Baraza la Wawakilishi".

Hayo sio maneno yangu, ni maneno ya katiba ya Zanzibar. Ibara ya 6 inasema;

Ibara ya 6:

"Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, atakuwa pia na jukumu la kutekeleza kazi na shughuli nyengine na atakuwa na madaraka mengine ya namna mbali mbali kama itakavyoelezwa na sheria kuhusu hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au Hesabu za Mashirika na Makampuni ya Umma ya Zanzibar".

Sasa Mhe. Spika, kifungu hiki kimeshaeleza kwamba iwapo Rais hatachukua hatua ya kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Baraza la Wawakilishi, basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataiwasilisha taarifa hiyo kwa Baraza la Wawakilishi au Naibu Spika, ambaye ataiwasilisha taarifa hiyo mbele ya Baraza la Wawakilishi.

Sasa Mhe. Spika, siku saba hazijapita, taarifa haijaletwa. Sasa sijui una madaraka gani. Lakini kawaida sisi kanuni zetu zinasema, mtu anapopewa *summon* na Baraza hajaenda. Basi Mhe. Spika, unamuagiza Kamishna wa Polisi amchukuwe amlete hapa. Sasa ripoti hii muda umeshapita. (*Makofi*)

Kwa hivyo, sitaki kusema umtume Kamishna akamkamate Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali amlete hapa kwa pingu, lakini kama hajatuletea ripoti. Mhe. Spika, tumia kanuni zetu, hili sio suala la kuilaumu serikali. Serikali kazi yake imeshamaliza wamepelekewa taarifa hii wameikalia Mdhibiti anatakiwa ailete hapa, sasa tena serikali tutailaumu ya nini. Mdhibiti atuletee ripoti hapa. Mhe. Spika, hii ndio katiba ya Zanzibar, Mwenyekiti nakutoa kosa kwa hili tu, lakini yaliyobakia yote nakuunga mkono. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba kama kusema tumeshasema. Kawaida unaposema na kumwambia mkubwa wako kama hakusikilizi, Waswahili wanamsemo wao wanasesma; "*Asiyesikia la Mkuu Huvunjika Guu*". Huu ubadhirifu, upotevu wa fedha na ukiukwaji wa taratibu ndio guu lenyewe kuvunjika hili. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sisi tumeshauda kamati nyingi na kamati hizi, mimi naishukuru sana serikali siku hizi wanakaa kwenye bango kitita, lakini inaonesha ripoti hii ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, kwenye bango kitita hii haikaliwi, kama ingekuwa inakaliwa ripoti hii basi manyago yasingetokea, kwa sababu yanayotokea ndio yale kwa yale. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba wenzangu wamesema tusubiri bajeti. Bajeti hii inayokuja, hapa tunakuja kupiga porojo tu. Kwa sababu huyo uliyemwambia wewe halafu hujijui kama upo au hupo, unatakiwa utowe agizo ulisimamie mwenyewe. Sasa mimi nataka kuna mambo yafanyike ndani ya wakati huu kabla ya bajeti. Tunamtaka, sio tunamuomba. Tunamtaka *CAG* afanye ukaguzi wa kina katika mradi wa *ZUSP*. Hili suala tulilizingumza, lakini inaonesha kama walivyosema wenzangu tunaonekana kama *comedy* hapa, tunasema halafu tunawacha hivi hivi.

Leo tumeunda kila kitengo, *TAKUKURU* tumeshaunda Tume ya Maadili, sijui ripoti gani lakini mambo ndio yale yale. Mhe. Spika, mradi huu watu wameshatajirika, lakini wananchi wa *Kwamtipura* wanazama.

Mhe. Spika, mradi wa *ZUSP* moja katika *component* yake ni ujenzi wa mitaro. Leo inaonesha hatuna kipaumbele, kipaumbele katika mradi wa *ZUSP*, una *component* ya ununuvi wa magari, ujengaji wa *slab*, ununuvi sijui wa nini yale ndio yaliyokuwa kipaumbele, lakini ile mitaro ambayo wananchi mvua zikinyesha watu wanazama sio kipaumbele imewekwa mwisho kila siku tenda kesho mara keshokutwa, lakini hayo yaliyofanywa kipaumbele manyago matupu.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali nenda katufanyie *audit*, tena tukimaliza tu kama una vitabu vingapi hujamaliza, hilo wacha ukaguzi maalum, tunataka hii ripoti tunapokuja kwenye bajeti tuipate. (*Makofî*)

Mhe. Spika, nina ushahidi wa Kinyamwezi, uchakachuaji katika ununuvi wa magari hayana viwango. Mhe. Spika, katika *component* ile kuna ujenzi wa *slab* sijui na vidude vyengine vikontena vyakusema kubebesi taka. *Ehe!* aibu vimetengenezwa Fuoni hapo, Mkaguzi katufanyie ukaguzi, kwa sababu tukisema sisi tunaonekana kama aah! watu wanawaonea watu. Lakini tunamuambia Mkaguzi ambaye ametajwa kwa mujibu wa katiba na yeze ndiye anayetakiwa aeleze serikali, haya ndio mambo yenye.

Mhe. Spika, wenzangu wamezungumza, katika miradi mikubwa yote kwa kweli, ambapo miradi ile ndio ingekuja kuondoa umaskini ndio katika hiyo programu ya *MKUZA*, miradi hiyo ndio inayotumia pesa nyingi, inaiingizia serikali madeni, halafu miradi yenye haionekani faida yake. Kama huu mradi wa *e-Government*, mradi huu tumeshausema sana na kama huu mradi ungefanikiwa vizuri basi ungeingizia fedha mpaka serikali.

Mhe. Spika, hivi karibuni naishukuru serikali mlitutuma huko duniani katika mukutano wa maafa. Huko moja ya kitu nilichokisoma ndio hizi *priority*, *political will* inatakiwa katika masuala ambayo yanaathiri maisha ya wananchi, ndio huo ujenzi wa mitaro, yaani kuna vitu ambavyo viko katika *shadow*, Mwenyezi Mungu kaweka *shadow* hasa.

Sasa zile *shadow* ambazo Mwenyezi Mungu kaziweka *original*. Kwa mfano, mvua za masika zinajulikana kila unapofika mwezi Machi mpaka mwezi May mvua za masika. Leo badala ya kwenda kujenga mitaro tumeuka kununua magari mabovu na vitu vyengine ovyo ovyo tu, kwa hivyo tunamuomba Mkaguzi aende akafanye kazi.

Sasa huko duniani Mhe. Spika, nilipokwenda, yaani ukifungua *Internet*, nilikuwa nawaambia wenzangu, jamani nasikia redio, *TBC* naisikia, *Redio One* naisikia, Redio Adhana naisikia, mbona Redio Zanzibar siisikii, maana yake nilikuwa nataka nisikilize vipindi vyakusema *laptop* zao au *computer* zao. Kazi siku hizi zinafanywa kiganjani. Leo saa nzima mtu anasubiri *file* lifunguke, kwa sababu gani, e-Government tulitegemea mradi huu ungesaidia kufungua mawasiliano kwa haraka ungeanzisha biashara na serikali ingepata mapato, mpaka leo mradi unasinzia.

Kwa hivyo, na hili Mhe. Spika, naomba vile vile tujaribu kuliangalia. Mhe. Waziri nilimsikia alipokuwa akisoma ripoti yake, nilikuwa sijafika nilikuwa kwenye gari, lakini nilikuwa nafuatilia. Tunamshukuru amefanya *reform* katika uongozi wa ile *ZIPA* yenye. Sasa Mhe. Spika, tulikuwa tunasema *ZIPA* ni *one stop centre*, kama ni *one stop centre* ina maana mwekezaji akija, anatakiwa ndani ya wiki moja ajuwe kapata au kakosa.

Mhe. Spika, hapa kwetu ni nenda rudi mpaka watu wanakimbia na ndio maana tunapata hawa wawekezaji wababaishaji ambao hawana viwango. Mtu bwana mwenye pesa yake au mwenye uwezo wake hawezi kuja hapa ukamuweka anahangaika na nyinyi, ye ye anataka kuwekeza nyinyi mnambungusha zungusha.

Mhe. Spika, wenzetu Rwanda pale hebu kawaangalieni. Tena naomba ZIPA, Kamati ya Fedha na Uchumi Mwenyekiti yuko wapi, Kaimu Mwenyekiti. Naomba waende Rwanda Kamati ya Fedha na Uchumi wakaangalie kile chombo ambacho kinafanana na ZIPA kule Rwanda vipi kinafanyakazi. Kule mwekezaji kila kitu kiko online, unaangalia mradi wako unaotaka ku-*invest* majibu unapata ndani ya wiki moja umeshamaliza kila kitu. Hapa kwetu nenda rudi, nenda rudi. Mwekezaji wa maana kwa hali hii hatutompatta.

Nashukuru kwa hii *reform* mliyoifanya, lakini nilikuwa naomba suala moja Mhe. Waziri, ambalo mimi nilifika pahala nikasema aah! sasa tena kusema sema sana Barazani iwe basi, sasa hivi angalau katika zile *key issues* niwafuate mawaziri ofisini angalau tuangalie utaratibu wa kuzitattua.

Mhe. Spika, suala la uwekezaji wa Chelezo, mzalendo Mzanzibari ameamua kuwekeza mradi mzuri wa Chelezo mpaka ripoti ile ya mazingira amefanya *assessment* kila kitu kiko *ok*, mpaka leo umekwama, mtupe taarifa na kama hauvezekani basi mumwambie. Mhe. Spika, nilikuwa naomba suala hili.

Mhe. Spika, leo kuna miradi. Nina rafiki yangu mwekezaji na Mhe. Makame Mshimba shahidi, kuna miradi hata haijafanyiwa *assessment* ya mazingira imeshapewa vibali. Lakini leo kuna mradi umeshafanyiwa *assessment* ya mazingira *certificate* tayari wameshatoa *ok* lakini mpaka leo nendarudi, nendarudi, Mhe. Spika, hili sio jambo zuri sana.

Suala la mfuko mkuu. Mhe. Spika, na mimi nampongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha, sijui umetishwa au vipi. Maana yake sisi mnakuwa mnatuambia aah! katishwa jamaa, leo kasema kesho kaufyata, katishwa. Sasa Mhe. Waziri wa Fedha sijui umetishwa, *speed* yako ya jana, *spirit* yako ya jana na leo imekuwa tofauti, wewe ni mwenzetu ni lazima tukuambie. Jana umefunua kombe leo umelifunika.

Mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyevitii, Mwenyekiti wa Kamati inayosimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, jana umenitia aibu. Leo matumizi ya safari za ndani ambazo hazzoneshi tija. Mhe. Spika, kwa bahati mbaya sana, tena naomba utaratibu huu tuangalie sheria zetu tubadilishe, fedha hizi za safari. Unajua sio vizuri kuwataja mamama, lakini ni lazima tuwataje kwa sababu wametajwa, zije katika bajeti ya wizara zisitoke mfuko mkuu, kwa sababu mfuko mkuu kule ufuatiliaji wake ni mgumu mheshimiwa.

Mhe. Spika, leo safari mtu anakwenda kutia hina kwao, milioni 500. Safari moja milioni 500, milioni 50 samahani. Kasafiri katoka hapa kenda Pemba kenda kutia hina milioni 50, ndio safari za wake wa viongozi au anakwenda kufanya nini, anakwenda kufanya nini sijui katika harambee, yaani ukiangalia thamani ya kazi anayokwenda kuifanya na tija iliopatikana ni vitu viwili tofauti ni lazima tuweke bajeti maalum.

Isiwe tena kwamba hizi zinatoka mfuko mkuu wa serikali, ni lazima tuweke katika bajeti zao za wizara. Ndio maana nikasema jana Mhe. Waziri kwa kweli umenifunua kote, maana sio nguo, umenifunua kote, maana yake shati nilibakia nalo, ndio maana nasema sasa hesabu za kina mama hawa niletewe kwenye bajeti ya wizara, kwa sababu tukishamuwekea haya mama hizi atasafiri atakwenda wapi, zikishamaliza ataendea wapi. Lakini sasa kama mfuko mkuu wa serikali Mhe. Spika, kule anajua mimi nikisema nakwenda huku, haya.

Unawajua tena kina mama na unatujua na sisi kina baba, akisema anataka kwenda kutia hina unaogopa hata kumwambia usiende. Samahani sitaki kusema kwamba wanakwenda kutia hina, maana unajua watu wanawenza wakaichukua vibaya, lakini katika zile shughuli ambazo sio rasmi.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe tumia dakika tano, zilizobaki ili dakika tano nyengine nina kazi nazo muhimu sana hapa. Kwa hivyo, dakika zako 20 imebakia dakika tano.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Hii! Haya. Basi mimi naomba kama alivyooleza Mhe. Mwenyekiti, mifumo ya ukusanyaji wa kodi, hasa katika mahoteli Mhe. Waziri mimi nampenda sana na ninampenda kwa sababu ni mkweli, anasema waheshimiwa mnapoona mianya niambieni, sisi wengine hatusubiri Barazani.

Mhe. Waziri nilikuletea mwekezaji aliyetapeliwa, yule Mfaransa na kwa sababu alitapeliwa na mwekezaji mwenzake ilibidi afunuwe kila kitu, akatuonesha wizi wa wawekezaji wenye mahoteli wanaoibia nchi. Wageni wanakuwa Zanzibar wanaingia ndani ya hoteli, lakini fedha zinalipwa Italy au Austria, maana yake angalau wale *package tour*, wale Wataliano pia haijambo, hao ni watalii wa kawaida. Kwa hivyo, ina maana hapo watendaji

wetu wa *ZRB* wakienda hawaoni kitu, fedha zimeshalipwa huko watu wanafungua miradi mingine kwa fedha ambazo ziliwu zilipiwe kodi.

Namshukuru Mhe. Waziri hakunidharau, nilizungumza naye nikamwachia yule mwekezaji, tumempeleka *ZRB*, tumempeleka *TRA*. Nawaomba watendaji wa *TRA* na *ZRB* wafuatilie na yule jamaa alisema yuko tayari kuishauri serikali hata kama mtamfanya kama *consultant*, kwa sababu yule huko Poland aliko ni *consultant* wa Serikali ya Poland, lakini na yeze huko ni mwekezaji, na alisema yuko tayari atatusaidia namna gani wawekezaji wanavyoziibia nchi hizi za Kiafrika ambazo hawajataalamuka. Naomba sana ile kazi mheshimiwa muiendeleze.

Vile vile kuhusu magendo ya mafuta. Mhe. Spika, hili wala sio la kusema Zanzibar leo kuwe na magendo ya mafuta kweli, kisiwa chenyewe kimekaa kama mkono magendo ya mafuta yanapotokea mnajua. Sasa hili mimi nafikiri ndio yale yale tunaonekana kama *comedy* maana tunasema magendo ya mafuta yanapouzwa unayajua, hatuna hatua yoyote tunayoichukua.

Mhe. Spika, kuhusu suala la ukaguzi maalum wa viinua mgongo, nafikiri hili nimeshalitolea maagizo kwa *CAG*, tuletewe hiyo ripoti kwa sababu sio suala tena la serikali, serikalini kwa mujibu wa katiba limeshaondoka. Kwa hivyo, mimi nafikiri ni suala la kulifanyia kazi.

Mhe. Spika, kwa kuheshimu hizo dakika zako tano, naomba sana kuna madeni ambayo Mhe. Waziri wa Fedha ambayo mmekubaliana na mawizara, hasa madeni yale ya miaka ya nyuma. Kuna madeni ambayo mliyabeba serikali na kuna madeni mliowaachia wenye we wizara. Naomba basi yale madeni yaliyordhiwa yaliyochukuliwa na serikali walipwe wenye we, kwa sababu tatizo letu Mhe. Spika, hawa wananchi wetu wanaoikopesha serikali inapokuwa kidogo haina fedha na wao fedha zile wanazipata katika njia tofauti; nyengine wanazikopa wanaingia katika mabenki wanatolewa riba. Kwa hivyo, fedha zile zinapochelewa kulipwa Mhe. Spika, hawa tunakuwa tunawafilisi, kwa hivyo ni kitu ambacho namuomba sana Mhe. Waziri aweze kutusaidia.

Vile vile, Mhe. Spika, nilikuwa naomba Mwenyekiti wa Kamati ya PAC. Mhe. Spika, suala hili ndio namalizia, kama alivyosema Mhe. Hija Hassan, tatizo la kuwa na sheria yetu ya utawala wa Baraza unatukosesha sisi wataalamu wa kutusaidia kazi ya kuichunguza serikali, na serikali mswada wetu wanaukalilia kwa sababu wanajua Baraza lako likiajiri wataalamu amba wanaweza kuichunguza serikali. Serikali itakuwa haiwezi kufanya tena manyago. Sasa tatizo tulilokuwa nalo, mfano *CAG* ina maana akishafanyakazi awape kamati ya *PAC*.

Kuna ukaguzi wa *technical audit*. Leo unaambiwa kama hivyo vibeseni vya kuzolea taka vilivyochochongwa, waangalie je, ile *thickness* ya ile *plat* na ule umadhubuti, itaweza ku-*survive* kwa muda wa miaka mingapi. Leo zile *plat* zimenunuliwa Mlandege, zimepelekwa pale Fuoni.

Mimi nataka niwaambie wizi wa Zanzibar, wasitufikirie sisi hatujui. Sisi bwana tumezaliwa shamba. Mimi nimezaliwa Chaani, lakini nimekulia mjini, tunajua kila mnachokiiba, lakini tatizo ni serikali yetu ndio inayowafumbia macho.

Sasa Mhe. Spika, naomba usije ukonisema ili siku ya pili usije ukainyima naomba niishie hapa, hizo dakika zangu nyengine utanipa kesho. Ahsante. (*Makofii*)

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa mchango wako huo. Kuna taarifa mbili, lakini kwanza tuenze na taarifa ya kwanza ambayo ina umuhimu ndio zile dakika tano ambazo nimesema tuzitumie. Naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

TAARIFA

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba uniwie radhi nisome taarifa fupi inayohusu kuendelea kwa kikao chetu cha Baraza lako tukufu na hii Mhe. Spika, inatokana na muda. Kwa kuwa mkutano huu wa kumi na tisa wa Baraza la Nane la Wawakilishi, ambaa ulianza shughuli zake tarehe 11 Machi, 2015 tayari umechukua muda wa zaidi ya wiki mbili na endapo Baraza lako halikuchukua hatua za dharura za kumaliza mkutano huu mapema zaidi, mkutano huu unaweza kuchukua zaidi ya wiki tatu za kazi.

Mhe. Spika, mbali na shughuli za mukutano huu Baraza lako tukufu bado limekabiliwa na shughuli nzito zaidi ya kuzingatia bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ndani ya muda mfupi sana kutoka sasa. Lakini kabla ya hatua hiyo kamati za kudumu za Baraza zitawajibika kufanya shughuli zake za kawaida na pia shughuli za kupitia bajeti za wizara za serikali kabla ya kuwasilishwa mbele ya Baraza.

Mhe. Spika, shughuli zote hizi muhimu na zinahitaji muda wa kutosha wa kuweza kufanya, muda ambao unaweza usipatikane bila ya kujipanga vyema kuuokoa muda zaidi wa kutumika kwenye mukutano huu wa Baraza.

Mhe. Spika, pamoja na ukweli huo kwa upande wa serikali, muda wote wa mukutano huu wa Baraza shughuli nyingi zinazohusu mawaziri wa serikali nje ya Baraza, zimeahirishwa ili kutoa nafasi kwa Waheshimiwa Mawaziri kushiriki kwenye mukutano huu.

Mhe. Spika, ilikuwa ni imani ya serikali kuwa kama ilivyokawaida ya mukutano huu ungeweza kumalizika si zaidi ya tarehe 31 Machi, 2015 na kwa hivyo serikali ilijipangia shughuli ambazo haziwezi kuepukika kama waziri wake kutekeleza nje ya Baraza kuanzia tarehe 01 April, 2015.

Mhe. Spika, kwa kuamini kuwa endapo Baraza lako tukufu halitochukua maamuzi makini kuhusu matumizi ya muda uliopo kwa kuendelea na shughuli za Baraza, basi mambo mengi ya utekelezaji wa shughuli za Baraza na pia kwa serikali yanaweza yasiende kama ilivyopangwa.

Mhe. Spika, kutohana na sababu hizo naomba kutoa hoja Bazara lako tukufu liridhie kuweka kando kanuni ya 24 ya kanuni za Baraza, ili Baraza liweze kuendelea na shughuli zake siku ya Jumamosi ya tarehe 28 Machi, 2015 kwa lengo la kutoa nafasi kwa Baraza kumalizia shughuli zake za tarehe 31 Machi, 2015 bila kukosa.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja, ili Baraza lako liweze kufanya shughuli zake siku ya Jumamosi ili tuweze kumudu muda wa kumaliza shughuli zetu tarehe 31 Machi, 2015. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe, hiyo ndio taarifa moja muhimu sana na kama mtakumbuka nilikuwa mara kwa mara nasema kwamba tuko nyuma ya muda ambao tumejipangia na shughuli zetu ambazo zinapaswa ziende kwa umakini sana. Nashukuru tumejitahidi kufanya hivyo, lakini bado kuna shughuli hizo ndio maana Mhe. Waziri amekuja mbele yetu kutoa hoja hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya maelezo hayo ambayo Mhe. Waziri ameyatoa, naomba sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mikono. Waliokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu akitujaalia shughuli zetu zitaendelea siku ya Jumamosi kama kawaida. Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wale ambao walipanga panga safari kidogo watusamehe kwa sababu ya umuhimu wa shughuli hizi.

Taarifa nyengine ya pili Waheshimiwa Wajumbe, ni kwamba inahusu maadhisho ya siku ya Mashujaa Karume day, tarehe 07/04/2015. Waheshimiwa Wajumbe kama tunavyofahamu kwamba kila ifikapo tarehe 07 Aprili ya kila mwaka nchi yetu huadhimisha siku ya Mashujaa Zanzibar yaani Karume day, kwa kusoma hitma dua maalum ya kumuombea Rais wa Kwanza wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Marehemu Sheikh Abeid Aman Karume, pamoja na waasisi na viongozi wengine wa Mapinduzi ya nchi yetu kwa ujumla.

Kwa mwaka 2015 hitma na dua hiyo itafanya siku ya Jumanne ya tarehe 07 Aprili, 2015 katika ukumbi wa Ofisi Kuu ya Chama cha Mapinduzi Kisiwandui, kuanzia saa 3:00 za asubuhi. Kwa taarifa hii Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, inawaalika Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, kuhudhuria katika shughuli hiyo muhimu ya kitaifa. Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuwasilisha taarifa hiyo.

Taarifa ya pili ni kukumbusha tu, taarifa ya arubaini ya mwenzetu Marehemu Salmin Awadh Salmin. Tunakumbushwa kwamba familia ya Marehemu Salmin Awadh Salmin, inawaalifu Waheshimiwa Wajumbe na watendaji wote wa Baraza la Wawakilishi, arubaini ya Marehemu Salmin Awadh Salmin, itakayofanya siku ya Jumamosi tarehe 28 Machi, 2015 baada ya sala ya Alfajiri huko nyumbani kwao Mpenda, sote tunaombwa kushiriki katika shughuli hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe, hizo ndio taarifa mbili kwa leo, naomba radhi sana nimezisoma nikiwa nimekaa, kwa sababu ya dharura inayofahamika. Nashukuru sana.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya taarifa hizo nichukuwe nafasi kuwashukuru tena, kwa kazi nzuri tuliyoshirikiana kuendesha shughuli zetu za Baraza la Wawakilishi. Sasa naomba niahirishe kikao hiki mpaka kesho tarehe 27 Machi, 2015 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 1:44 usiku Kikao kiliakhirishwa mpaka tarehe 27/03/2015 saa 3:00 za asubuhi)